# Nipashe

Alhamisi Juni 20, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579949

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper




## Wanahabari wahoji maofisa NEC kuwa makada wa CCM


UKURASA 2




UKURASA 13

# Wadaiwa sugu mabilioni serikali waanikwa juani

**WAMO** wafanyabiashara, wanasiasa maarufu, watakiwa kulipa mara moja vinginevyo... *Endelea ukurasa wa 2*



Hashim Rungwe



Mohamed Dewji



Stephen Wassira



Yusuf Manji

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

**ADAIWA KUMUUNGUZA MJUKUU WAKE KISA KUKOJOA KITANDANI**

MTOTO wa kike mwenye umri wa miaka mitano, mkazi wa Lukobe Manispaa ya Morogoro, amelazwa...

UKURASA WA 5

**NAIBU SPIKA AMTETEA MBUNGE ALIYECHANA HOTUBA UPINZANI**

NAIBU Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, amesema Mbunge wa Kasulu Vijijini, Augustine Vuma (CCM)...

UKURASA WA 21

**MHANDISI ALIYEKUWA NA KESI ADAIWA KUJINYONGA**

MHANDISI wa Majengo wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya, Aswile Msika (37), amekutwa...

# Serikali yasema mbu wa dengue ni sugu

UKURASA 2

## Magufuli ang'ara jarida la Forbes

UKURASA 3

**MICHEZO** PIGO STARS, MORIS BASI TENA AFCON UK. 32

MAONI, KATUNI UK.6

# Wahoji maofisa NEC kuwa makada CCM

**Romana Mallya na Enock Charles**

MWENYEKITI wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Jaji Semistocles Kaijage, amesema tume anayoiongoza haina shabiki, kada wala mwanachama hai wa chama chochote cha siasa na walikuwapo imebaki kuwa historia.

Vilevile, kiongozi huyo wa NEC pia amesema tume hiyo haitatumia wakurugenzi wa halmashauri kwenye usimamizi wa uchaguzi kutokana na uamuzi uliotolewa hivi karibuni na mahakama wa kuzuia viongozi hao wa serikali kusimamia uchaguzi.

Jaji Kaijage aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam katika semina ya wahariri na waandishi wa habari iliyoandaliwa na tume hiyo kwa lengo kuhusu uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura unaotarajia kufanyika kuanzia mwezi ujao.

Moja ya maswali ambayo washiriki wengi walitaka kupata majibu kutoka NEC ni namna tume hiyo ilivyojipanga kuhakikisha hakutatokea malalamiko dhidi yake kuwa inafanya upendeleo kwa baadhi ya vyama kwa kuwa ndani yake kuna makada, hasa wa Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Washiriki hao walitaja majina ya maofisa wa NEC wanaoamini ni makada wa CCM kuwa ni pamoja na Mkurugenzi wa tume hiyo, Dk. Athumani Kihamia na Kamishna wa Tume, Ramadhan Omari Mapuri, aliyeteuliwa hivi karibuni.

"Kwenye tume ninayoiongoza, hakuna mwanachama hai wa chama chochote cha siasa kwa sababu NEC inatekeleza majukumu

INAENDELEA UK. 8

# Wadaiwa sugu mabilioni serikali waanikwa juani

**Na Gwamaka Alipipi**

WIZARA ya Fedha na Mipango imetoa orodha ya wadaiwa sugu 15 waliokopeshwa na serikali kupitia mpango wa 'Commodity Import Support (CIS)' ikiwa na majina ya wafanyabiashara wakubwa nchini wakiwamo Mohamed Dewji 'MO' na Yusuph Manji.

Katika tangazo lililotolewa jana na Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Doto James, ilielezwa kuwa madeni hayo ni mkopo wenye masharti nafuu uliotolewa kwa taasisi, kampuni, viwanda na wafanyabiashara kupitia programu hiyo.

Ilielezwa katika tangazo hilo kwamba wakopaji walitakiwa kurejesha mikopo bila kutozwa riba katika kipindi cha miezi 18 tangu walipopewa mikopo hiyo.

Kwa mujibu wa tangazo hilo, wanufaika wa mikopo hiyo ni pamoja na Manji aliyepatiwa mkopo kupitia kampuni za Farm Equipment Tanzania Ltd, Quality Group Ltd, Dunhill Motors Ltd, Quality Seed Ltd, Quality Garage Ltd.

Wengine MO aliyepatiwa mkopo kupitia kampuni za 21st Century Textiles Ltd na Afritex Ltd, S.S Rashid aliyenufaika kupitia kampuni za Pwani Tours and Safari Ltd, Pwani Investment Ltd, na Isaack Bugali aliyepatiwa mkopo kupitia kampuni za Dar es Salaam International School Trust Fund na Upoloto Farm Ltd.

Wengine ni Prof. Bernard Kirei aliyepewa mkopo kupitia kampuni ya K.B Medicare Ltd, Stephen Wasira kupitia Kampuni ya Siza Cold Storage Co.Ltd, Martha Lyimo kupitia Kampuni ya Sorority Co. Ltd na Kampuni ya 21st Century, Afritex Ltd.

Wengine ni Bokeye Kangoye aliyenufaika na mkopo huo kupitia Kampuni ya Kichonge Miller, Ahiya Lukumayi kupitia Kampuni ya Rela Investment Company Ltd, Hashim Rungwe kupitia Kampuni ya Bahari Motor Co Ltd, Andrew Richard Kisenge kupitia Kampuni ya Andrew Traders Co Ltd, Boniventure Boniventure kupitia Kampuni ya Oth Investment Co Ltd, na Dk. Kingu kupitia Kampuni ya Kiomboi Kisiriri Pharmacy Ltd.

"Mkopaji akichelewa kulipa katika kipindi cha miezi 18 tangu kupatiwa mkopo, atapaswa kulipa riba ya asimilia sawa na kiwango kinachotozwa na Benki Kuu ya Tanzania (BoT) inapoikopesha serikali katika kipindi husika. Zaidi ya kampuni 980 zilikopeshwa chini ya utaratibu huu," ilielezwa katika tangazo hilo.

Katika miaka ya 1980 na 2000, wahisani walitoa fedha za kigeni kwa Serikali ya Tanzania kupitia mpango maalum uliofahamika kama 'Commodity Import Support (CIS)' kwa lengo la kuipa serikali uwezo wa kuimarisha uchumi kwa kuzipatia taasisi, kampuni, viwanda na wafanyabiashara uwezo wa kuagiza bidhaa na malighafi kutoka nje ya nchi.

Hatua hiyo ilichukuliwa kutokana na nchi kukabiliwa na upungufu mkubwa wa fedha za kigeni.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama (kulia), akijadili jambo na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu (kushoto), na Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Dk. Faustine Ndugulile, bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: OWM**

# Serikali: Mbu wa dengue ni sugu

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

SERIKALI imetoa tahadhari kuhusu kasi ya maambukizo ya homa ya dengue nchini, ikieleza kuwa mbu aina ya Aedes wanaoeneza ugonjwa huo ni sugu na hawafi kirahisi kwa dawa zinazotumika kuua mazalia ya mbu. Imeeleza kuwa mbu hao weusi wenye madoa meupe, hupendelea kuuma hasa wakati wa asubuhi, mchana na jioni.

Tahadhari hiyo ilitolewa jana bungeni jijini Dodoma na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, alipojibu swali la nyongeza la Mbunge wa Ilala (CCM), Mussa Azzan Zungu.

Mbunge huyo alitaka kujua sababu za serikali kutogawa dawa za chenga kwa viongozi wa serikali za mitaa ili wazimwage kwenye maeneo yao kuua mbu na mazalia yao.

"Tayari suala hili linafanyiwa kazi katika maeneo mbalimbali ya Dar es Salaam na siku mbili zijazo, serikali itatoa tamko bungeni kuhusu taratibu mbalimbali za kupambana na dengue.

"Pia, tumeanzisha kikosi cha wataalamu wa kuangamiza mbu ili pamoja na mambo mengine, wataeleze kama dawa tunazotumia zinafaa au hazifai.

"Tumeshawakusanya wataalamu kutoka sehemu mbalimbali kwa ajili ya kuangamiza mbu hawa na kuangalia njia mbadala za kupambana na mbu, lakini inaonekana mbu hawa ni sugu," Ummy alisema.

Kwa mujibu wa waziri huyo, tayari dawa mbalimbali zinatumika katika kudhibiti ugonjwa huo kwa sasa.

Wakati akiuliza swali la msingi, Zungu alisema ugonjwa wa dengue katika Mkoa wa Dar es Salaam bado ni changamoto na kuhoji kama serikali iko tayari kutoa dawa za chenga ili kuzimwaga kwenye maeneo mbalimbali kutokomeza mazalia ya mbu hao.

Kwa mujibu wa Waziri Ummy, dalili za ugonjwa huo ni pamoja na homa ya ghafla, kuumwa na kichwa hususan sehemu za macho, maumivu ya viungo na uchovu ambazo huanza kujitokeza kati ya siku ya tatu hadi 14 tangu kuambukizwa virusi vya dengue.

## HABARI KITAIFA




Mfanyabiashara James Rugemalira, anayekabiliwa na kesi ya kutakatisha fedha na kuisababishia serikali hasara ya USD 22, 198,544.60 na Sh. bil. 309, akiwa chini ya ulinzi wa askari Magereza, wakati akitoka katika Mahakama ya Rufani jijini Dar es Salaam jana, kuiomba itengue uamuzi wa Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam uliomnyima dhamana kwa sababu haikuwa sahihi katika uamuzi huo. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# JPM ang'ara jarida la Forbes

**Na Mwandishi wa**
MAELEZO

RAIS John Magufuli, ameendelea kukubalika kimataifa baada ya jarida maarufu duniani la Forbes kubashiri kwamba ataivusha Tanzania na kuwa nchi yenye kipato cha kati kupitia ajenda yake ya Tanzania ya viwanda chini ya mpango wa maendeleo wa 2025.

Jarida hilo la Forbes Afrika la Julai mwaka huu, ambalo lilikuwa mahsusi kwa ajili ya kelezea mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Tano na uongozi wa Rais Magufuli, imeelezwa maono yake kama kiongozi wa nchi yameifanya Tanzania kupiga hatua kubwa za maendeleo na inatarajiwa kuwa miongoni mwa nchi chache sana za Afrika zenye maendeleo yanayoonekana na yanayopatikana kwa muda mfupi.

Kwa mujibu wa jarida hilo ambalo limemwelezea Rais Magufuli kama 'Tingatinga' katika kusimamia kile anachokiamini, miongoni mwa mambo makubwa yanayomfanya ang'ae kimataifa ni pamoja na ujenzi wa reli ya kisasa ya Standard Gauge (SGR), upanuzi wa bandari na ujenzi wa miundombinu ya barabara zinazounganisha nchi nzima ambazo ni kichocheo kikubwa cha maendeleo hapa nchini.

Aidha, Rais Magufuli, ameelezewa kuwa ni mtu asiye na masihara katika kusimamia masuala ya maendeleo, mfano jinsi alivyosimamia na kuhakikisha Uwanja wa Ndege wa Julius Kambarage Nyerere (JNIA), terminal three, unakamilika kwa wakati na kwa kiwango cha kimataifa.

Jarida la Forbes limeendelea kumwelezea Rais Magufuli kuwa, mafanikio mengi anayopata ni kutokana na kuongozwa na mpango wa maendeleo wa 2025 pamoja na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya 2015.

Miradi mingine iliyoainishwa kuonyesha utendaji wake ni ile ya umeme ya Kinyerezi, awamu ya kwanza, ya pili na ya tatu, pamoja na mradi mkubwa wa kuzalisha umeme katika maporomoko ya Mto Rufiji maarufu kama Stieglers Gorge, ambayo lengo lake ni kumaliza kabisa tatizo la umeme nchini hasa kwa wananchi wa vijijini.

Kuhusu ukuaji wa uchumi, Jarida la Forbes, limeelezea kuwa katika kipindi cha utawala wake tangu aingie madarakani mwaka 2015, uchumi umeendelea kukua kwa kasi kwa kiwango cha asilimia saba ambao ni ukuaji wa mfano na wa kuridhisha kwa nchi za Afrika ikilinganishwa na miaka mingi iliyopita.

Katika uwekezaji Rais Magufuli amenukuliwa akiwahakikishia wawekezaji na dunia kwa ujumla kwamba, Tanzania ni nchi salama kwa uwekezaji na akawakaribisha kuja kuwekeza kwa kuwa ameendelea kufanya mapinduzi makubwa katika uwekezaji lengo kuu ikiwa ni kuvutia wawekezaji wengi zaidi. Mahojiano ya Rais Magufuli yaliyotolewa na Jarida la Forbes Africa, yalifanyika mapema mwaka huu na jarida hilo lilikuwa na toleo maalum la Tanzania kuhusiana na mambo mbalimbali yanayotekelezwa na serikali.

# Adaiwa kumuunguza mjukuu wake kisa kukojoa kitandani

**Na Idda Mushi,**

MOROGORO

MTOTO wa kike mwenye umri wa miaka mitano, mkazi wa Lukobe Manispaa ya Morogoro, amelazwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro kwa matibabu baada ya kudaiwa kuchomwa sehemu za siri na bibi mzaa baba.

Mtoto huyo (jina linahifadhiwa) anadaiwa kufanyiwa unyama huo na bibi yake, Asia Ahmed (52), mkazi wa Kihonda Tushikamane, kwa madai ya kukerwa na tabia yake ya mara kwa mara ya kukojoa kitandani.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo, Dk. Francis Semwene, alikiri jana kupokewa kwa mtoto huyo tangu Juni 15, mwaka huu akiwa na majeraha sehemu za siri na kwenye mapaja na kwamba aliyemfikisha hospitalini alidai aliunguzwa na bibi yake.

Hata hivyo, alisema mtoto huyo kwa sasa anaendelea vizuri na matibabu, chini ya uangalizi wa madaktari na wauguzi.

Kuhusu madhara yanayoweza kusababishwa na moto, Dk. Semwene alisema iwapo mtu ataungua na moto anaweza kuwa na madhara au yasijitokeze, lakini kikubwa ni kuwa na makovu yanayoweza kutengeneza usugu kwa nyama kukakamaa.

Mwandishi wa habari hii alimshuhudia mtoto huyo akiendelea na matibabu chini ya uangalizi wa bibi yake mwingine na shangazi yake, Zainab Abdalah, aliyesema walipata taarifa za tukio hilo na kuamua kumuuguza.

Mtuhumiwa anayedaiwa kufanya ukatili huo, ambaye tayari amekamatwa na polisi, amebainisha amekuwa akimlea mjukuu wake huyo ambaye ni mtoto wa mwanawe wa kiume tangu akiwa na mwaka mmoja baada ya kutelekezwa na mama yake mzazi.

Bibi huyo alisema aliamua kumchoma sehemu za siri akiamini hiyo ilikuwa adhabu ya kawaida ili kumrekebisha tabia.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Wilbroad Mutafungwa, alisema wanaendelea kumhoji bibi huyo na taratibu zaidi za kumfikisha mahakamani zinaendelea.

Kamanda Mutafungwa pia alilaani vikali matukio ya ukatili wa kijinsia na ukatili kwa watoto yanayoendelea na kutaka wananchi wasiyafumbie macho kwa kuwa si masuala ya kifamilia bali ni jinai.

# Rugemalira aomba uamuzi Mahakama Kuu utenguliwe

**Na Hellen Mwango**

MFANYABIASHARA James Rugemalira, ameiomba Mahakama ya Rufani kutengua uamuzi wa Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam uliomnyima dhamana kwa sababu haikuwa sahihi katika uamuzi huo.

Madai hayo aliyatoa jana katika mahakama hiyo iliyoketi chini ya jopo la majaji watatu likiongozwa na Mwenyekiti, Jaji Richard Mziray, akisaidiana na Jaji Ignas Kitusi na Winfridah Korosso.

Awali, aliomba mahakama hiyo impe kibali cha kujitetea mwenyewe huku akisaidiana na mawakili wake pale panapohitajika hoja za kisheria zaidi.

Mahakama ilikubali ombi la mlalamikaji.

Rugemalira akisaidiana na wakili wake Pasco Kamala, alidai mashtaka yanayomkabili yana dhamana kisheria na kwamba kama hayadhaminiki hayakutajwa kisheria.

Mbali na dhamana, mshtakiwa anadai kwamba hati ya mashtaka ina upungufu wa kisheria, mahakama impe dhamana.

Akijibu hoja hizo, Wakili wa Serikali Mkuu, Dk. Zainabu Mango, akisaidiana na Mawakili wa Serikali Wakuu, Faraja Nchimbi na Tumaini Kweka, kwa nyakati tofauti alidai uamuzi wa Mahakama Kuu wa kumnyima dhamana ulikuwa sahihi.

Aidha, Dk. Mango alidai kuwa kwa sababu uamuzi wa Mahakama Kuu ulikuwa sahihi, Jamhuri wanaiomba Mahakama ya Rufani kuitupilia mbali rufani hiyo.

"Waheshimiwa majaji miongoni mwa mashtaka yanayomkabili mlalamikaji ni pamoja na kutakatisha fedha, mashtaka ambayo hayana dhamana kisheria..." alidai Dk. Mango.

Naye Kweka alidai kuwa, katika hati ya mashtaka kwenye kesi inayomkabili Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, shtaka la saba hadi la 12 ni la kutakatisha fedha kwa mujibu wa sheria hayana dhamana.

Ilidaiwa kwamba, mashtaka hayo yaliyofunguliwa chini ya kifungu cha 148, kifungu kidogo cha (5) (a) (v) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai (CPA), yanaonyesha kutendeka kati ya mwaka 2012 hadi 2014, kipindi ambacho sheria ya uhujumu uchumi bado haijafanyiwa marekebisho.

"Watukufu majaji, hati ya mashtaka, ina makosa ya kutakatisha fedha ambayo hayana dhamana na hayajafunguliwa chini ya Sheria ya Uhujumu Uchumi," alidai Kweka.

"Hata tukisema makosa hayo ya utakatishaji yaangukie katika sheria ya uhujumu uchumi, suala la kujiuliza ni kwamba Bunge ilipotunga sheria lilidhamiria kosa hilo liwe na dhamana? Bunge ilifanyia marekebisho Sheria ya Uhujumu Uchumi na kuweka shtaka hilo katika sheria ya uhujumu uchumi kwa kuwa iliona hilo ni 'serious offence'," alidai Nchimbi.

Baada ya kusikilizwa kwa hoja hizo, majaji hao waliahirisha shauri hilo hadi siku nyingine ya uamuzi watakayoalifiwa pande zote mbili.

Katika kesi ya msingi, Rugemalira, anashtakiwa pamoja na mfanyabiashara mwenzake Harbinder Sethi, wote kwa pamoja wanakabiliwa na mashtaka 12, ikiwamo ya kutakatisha fedha na kuisababishia serikali hasara ya Dola za Kimarekani 22,198,544.60 na Sh. bilioni 309.

Kesi ya msingi itatajwa leo katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam.

# Masele afichua utetezi dhidi ya wanyonge umempatia umaarufu

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MBUNGE wa Jimbo la Shinyanga Mjini, Stephen Masele, ambaye pia ni Makamu wa Rais wa Bunge la Afrika (PAP), amesema tuhuma alizozitoa kuhusu Rais wa Bunge hilo, Rodger Mkodo, za kuwadhalilisha kingono watumishi wa bunge hilo, zimempatia umaarufu duniani kwa kupigania haki za wanyonge.

Masele alisema hayo jana wakati akitoa salamu kwenye uzinduzi wa kampeni ya Shinyanga ya Kijani, iliyoandaliwa na Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM), Mkoa wa Shinyanga, ambayo imelenga kupata ushindi wa kishindo kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu mwakani (2020) kwa ushindi wa wagombea wa CCM.

Alisema Mwenyezi Mungu huwa ana makusudi yake ya kutaka kumuinua mtu kupata umaarufu na kwamba alimpatia ujasiri wa kuibua tuhuma hiyo dhidi ya Rais wa Bunge hilo la Afrika, aliyedai kutuhumiwa kufanya mapenzi kwa nguvu na watumishi wa bunge hilo, lakini kutokana na kusimamia ukweli kitendo hicho kimemfanya ajulikane dunia nzima.

"Napenda kutoa wito kwa UVCCM sababu mimi ni zao la UVCCM, mkitaka kufanikiwa kisiasa msikubali kutetereka wala kuyumbishwa bali simamieni ukweli kama nilivyofanya mimi, mpaka sasa mimi ni Kaimu Rais wa Bunge la Afrika na nina fahamika dunia nzima wananijua Masele ni nani," alisema.

"Nilipigwa vita sana nilipoibua sakata hilo hadi na wanaCCM wenzangu, lakini nimejifunza kitu kumbe Mwenyezi Mungu anaweza kutumia maadui zako kukuinua juu, na nina jilinganisha na Rais wa nchini Urusi Putin, ukinigusa tu umegusa chuma," aliongeza.

Aidha, aliwataka vijana hao wanapomuona mwenzao anakosea wamuite na kumrekebisha, na siyo kumshambulia kitendo ambacho hakileti afya ndani ya chama zaidi ya kuanza kufarakana na kutengeneza makundi.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa UVCCM Taifa, Kheri James, aliwataka vijana hao kujiandikisha kupiga kura pamoja na kufanya kampeni kwa nguvu zote ili wagombea wote wa CCM washinde.

Mwenyekiti wa UVCCM Mkoa wa Shinyanga, Barack Shemahonge, alisema wamezindua kampeni hiyo ili kuuganisha nguvu ya vijana kuwa pamoja, hasa katika kuelekea kwenye kipindi cha uchaguzi wa serikali za mitaa, kwa kupanga mbinu za kupata ushindi wa kishindo.



Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko (kulia), akikagua ujenzi wa madarasa katika Shule ya Msingi Masunula, Shinyanga Vijijini juzi na kukuta yakiwa yamejengwa chini ya kiwango kwa kuanza kutoa nyufa na kupakwa rangi vibaya. **PICHA: MARCO MADUHU**

# TPA yapanua bandari za Kiwira, Ndumbi

**Na Mary Geofrey,** NYASA

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), inafanya upanuzi wa bandari za Kiwira mkoani Mbeya na Ndumbi, wilayani Nyasa mkoani Ruvuma, ili kurahisisha usafirishaji wa shehena ya makaa ya mawe kwenda Mbeya na nchi za jirani.

Ujenzi wa miradi hiyo, utakapokamilika utawezesha meli mbili za mizigo MV Njombe na MV Ruvuma kusafirisha zaidi ya tani 16,000 za makaa ya mawe.

Meneja wa Bandari za Ziwa Nyasa, Abeid Gallus, akizungumza na waandishi wa habari jana alisema lengo la mradi huo utahusisha ujenzi wa magati na uwekaji wa sakafu ngumu katika Bandari ya Kiwira pamoja na ujenzi wa gati la kisasa katika Bandari ya Ndumbi.

"Shehena kuu katika Bandari za Ziwa Nyasa ni makaa ya mawe ambayo hupitia katika Bandari ya Ndumbi iliyoko wilayani Nyasa hadi Kiwira na baadaye kusafirishwa na malori katika viwanda vilivyopo Mbeya na nyingine kwenda nchi jirani ya Malawi, hivyo kukamilika kwa upanuzi huu kutasaidia kurahisisha biashara ya makaa ya mawe," alisema Gallus.

Alisema gharama za kusafirisha tani moja ya mzigo kwa njia ya barabara ni zaidi ya 100,000, lakini kwa njia ya maji ni Sh. 85,000 na inatumia saa 12 kutoka Ruvuma hadi Mbeya.

"Meli moja ya mzigo inabeba tani 1,000 ya makaa ya mawe kila moja tofauti na sasa lori moja linabeba tani 30 sawa na malori 33, hivyo mpango huu utasaidia kupunguza uharibifu wa barabara na mizigo mingi kusafirishwa kwa wakati mmoja," alisema Gallus.

Alisema mbali na shehena ya makaa ya mawe yanayopita katika Bandari za Ziwa Nyasa pia wanasafirisha mabati, dagaa na mizigo mchanganyiko kwenda maeneo mbalimbali nchini.

Kwa upande wake Mhandisi wa Bandari za Ziwa Nyasa, Khamisi Nyembo, alisema upanuzi ukikamilika utawezesha meli hizo kufanya safari nne kwa mwezi na kurahisisha biashara ya makaa ya mawe nchini na kuondoka na adha ya usafiri, gharama za safari na muda wa kupokea mzigo.

Kwa upande wake mmiliki wa Mgodi wa Makaa ya Mawe wa Liweta, uliopo Kijiji cha Liweta, Wilaya ya Nyasa, mkoani Ruvuma, Richard Mahundi, alisema changamoto iliyopo katika usafirishaji wa makaa hayo ni miundombinu ya barabara.

"Kwa sasa tunasafirisha tani 5,000 kwa mwezi, lakini usafiri wa meli utaturahisishia kubeba walau tani 2,000 kwa wiki na hivyo kutuongezea wigo wa biashara ndani na nje ya nchi. Kwa hili tunaipongeza serikali," alisema.

Alieleza kuwa wateja wao wakubwa ni Kiwanda cha Saruji Mbeya (Mbeya Cement).

Alimwomba Waziri wa Madini, Ditto Biteko, kuwasaidia wachimbaji wadogo kupata mikopo katika benki ili kukuza biashara zao na kusaidia kukuza uchumi wa taifa.

# Mkuchika aagiza utafiti wa rushwa, utawala bora

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora, Kapteni mstaafu George Mkuchika, amewahimiza wanataaluma nchini kufanya utafiti kuhusu rushwa na utawala bora.

Pia amezishauri klabu za wapinga rushwa katika vyuo vya elimu ya juu na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) kutoa mapendekezo mbalimbali ya kukabiliana na tatizo la rushwa.

Mkuchika alitoa ushauri huo jana jijini hapa alipokuwa akizungumza kwenye siku maalum ya mapambano dhidi ya rushwa kwa nchi za Umoja wa Afrika yaliyofanyika katika Chuo Kikuu Dodoma (UDOM).

Alisema rushwa ni changamoto inayogusa kila sekta na kwamba hakuna nchi isiyokabiliwa na tatizo hilo ndiyo maana Umoja wa Mataifa uliweka makubaliano kupitia mkataba wake dhidi ya rushwa uliotiwa saini mwaka 2003 na nchi wanachama Merida nchini Mexico.

Alisema Tanzania kwa kutambua umuhimu wa ushirikiano katika kupambana na rushwa, imetia saini na kuridhia mikataba na itifaki za kupambana na rushwa kimataifa na kikanda.

"Serikali inachukulia tatizo la rushwa kwa uzito ndiyo maana viongozi mbalimbali wa serikali wamefika katika kongamano hilo ambalo ni utekelezaji wa makubaliano yaliyowekwa na wakuu wa nchi za Umoja wa Afrika wa kuweka siku maalumu ya mapambano," alisema.

Alifafanua kuwa jitihada za serikali ya awamu ya tano inayoongozwa na Rais John Magufuli imejiwekea vipaumbele vingi vikiwamo kutokomeza rushwa jambo ambalo ni moja ya ajenda katika awamu hii, hivyo kila mdau ikiwamo vyuo vya elimu ya juu vinapaswa kuunga mkono.

Alisema dhamira ya dhati ya Rais inaonekana ndani na nje ya mipaka ya nchi kwa kuwa hata utafiti unaohusu rushwa na utawala bora unaonyesha Tanzania inaendelea kupiga hatua. "Tanzania imeonekana kuongeza kiwango cha utawala bora kwa kupata alama 58.5/100 na kuwa nchi ya 14 kati ya 54 kwa mwaka 2018 ikilinganishwa na mwaka 2017 tulipopata alama 57.5/100 na kuwa nchi ya 17 katika Bara la Afrika," alisema.

Hii ni kwa mujibu wa ripoti ya taasisi ya Mo Ibrahim Index of African Governs (IIAG) ambayo hutoa ripoti yake kuhusu utawala bora kwa nchi za Afrika.

Alibainisha kuwa kiashiria cha Transparency International (CPI) kimeonyesha kuwa ndani ya miaka mitatu tangu 2015 hadi 2018, Tanzania imepanda hatua 18. Mwaka 2015 ilishika nafasi ya 117 kwa kupata asilimia 30 wakati mwaka 2018 imeshika nafasi ya 99 kati ya nchi 180 duniani kwa kupata alama 36.

Mkuchika aliongeza kuwa utafiti mwingine wa Taasisi ya Repoa mwaka 2017 umeonyesha wananchi saba kati ya 10 (asilimia 71) ya waliohojiwa walisema ushiriki wa serikali katika mapambano dhidi ya rushwa ni mzuri.

"Imani hiyo ikiongezeka kutoka asilimia 37 ya kwenye matokeo yaliyotolewa mwaka 2014. Aidha, matokeo ya utafiti uliofanywa na Twaweza mwaka 2017 nao umebainisha kuwa asilimia 85 ya wananchi waliohojiwa walieleza kuwa rushwa imepungua ukilinganisha na asilimia 11 waliohojiwa mwaka 2014," alisema.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Prof. Elisante Ole Gabriel (wa pili kulia), akizungumza wakati wa maonyesho ya ng'ombe bora wa maziwa, katika viwanja vya Nanenane, jijini Dodoma juzi. Wengine kutoka kulia ni, Mkurugenzi wa Taasisi ya Kimataifa ya Utafiti wa Mifugo (ILRI), Dk. Jimmy Smith; Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI), Dk. Eligy Shirima na Msimamizi wa Mradi wa Utafiti wa Vinasaba vya Ng`ombe wa Maziwa kutoka Taasisi ya Kimataifa ya Utafiti wa Mifugo (ILRI), Dk. Okeyo Mwai. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watuhumiwa 3 mauaji askari JWTZ mbaroni

**Na Christina Haule,** MOROGORO

WATU watatu wamekamatwa na Jeshi la Polisi mkoani Morogoro, kwa tuhuma za mauaji ya askari wa Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ) Sajenti Liumba (52).

Akithibitisha kutokea kwa tukio hilo, Kamanda wa Polisi mkoani Morogoro, Wilbroad Mutafungwa, alisema askari huyo mkazi wa Nanenane, alikutwa amefariki Mei 30, majira ya saa nne asubuhi katika mashamba ya mkonge Tungi, baada ya kutoweka nyumbani kwake tangu Mei 25, mwaka huu.

Kamanda Mutafungwa alisema mwili wa askari huyo ulikutwa umetupwa katika mashamba hayo, huku ukiwa umefungwa kamba mikononi na miguuni pamoja na jeraha kichogoni na ukiwa umeharibika.

Alisema baada ya kupata ripoti kuhusu tukio hilo Jeshi la Polisi mkoani hapa, liliamua kufanya msako mkali ambao ulifanya kukamatwa kwa watuhumiwa watatu waliohusika na mauaji hayo pamoja na pikipiki ya marehemu iliyowekwa namba ya bandia MC.766 BHA SANLG rangi nyeusi yenye namba LBRSPJB59E9010592 na simu ya mkononi aina ya Hope.

Aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Charles Luhunga (36), mfanyabiashara ya bodaboda, Juma Ramadhani (25), mfanyabiashara wa Mkundi na Yusuph Makusi (24), dereva bodaboda.

Mutafungwa alisema, Charlse Luhungwa, ndiye kiongozi wa kundi hilo na amekuwa akitekeleza matukio ya mauaji ndani ya Manispaa ya Morogoro ikiwamo uporaji wa pikipiki na kuwajeruhi waendesha pikipiki na baada ya kuzipora huzipeleka maeneo ya Gairo na Kibaigwa.

Alieleza kuwa pikipiki hizo huwa anazifikisha kwa mpokeaji, Mabaya Edward (30), akishirikiana na wenzake Mnabo Michael (24) na Emmanuel Nelson (24), wote wakazi wa Pandambili Kibaigwa, ambao wamekutwa na pikipiki ya marehemu na nyingine ambayo imetambuliwa na mwenyewe.

# Naibu Spika amtetea mbunge aliyechana hotuba upinzani

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

NAIBU Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, amesema Mbunge wa Kasulu Vijijini, Augustine Vuma (CCM), aliyechana kitabu cha hotuba mbadala ya bajeti ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ya mwaka 2019/20, hakupelekwa na wala hatopelekwa kuhojiwa katika Kamati ya Bunge ya Kinga, Haki, Maadili na Madaraka.

"Maamuzi (uamuzi) yanapotoka (unapotoka) hapa mbele, yanatoka kwa kuangalia pande zote mbili kama ambavyo hakuna mbunge ambaye ameshapelekwa Kamati ya Maadili kwa kuchana kitabu humu ndani ya Bunge. Nimeshamtaja Mheshimiwa Esther Bulaya (Bunda Mjini-Chadema) alishafanya hivyo na Mheshimiwa Vuma, hivyo hivyo hakupelekwa na hatopelekwa. Hakuna Mbunge yeyote anayependelewa humu ndani, maamuzi (uamuzi) yanayotoka (unaotoka) yako (uko) kikanuni," alisema.

Dk. Tulia alitoa ufafanuzi huo jana kuhusu mwongozo ulioombwa na Mnadhimu wa Kambi Rasmi Bungeni, Joseph Selasini, ambaye ni Mbunge wa Rombo (Chadema).

Kabla ya Naibu Spika kutoa msimamo huo wa kiti, juzi jioni wakati wa kipindi cha pili, Dk.Tulia aliagiza kutolewa ndani ya ukumbi wa Bunge, wabunge watatu wa Chadema

INAENDELEA UK.8

# Mpina awapa mtihani mgumu watafiti kilimo

**Na Mwandishi Maalum,** DODOMA

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, amewapa kibarua kizito watafiti wa mifugo kuhakikisha wanafanya kazi usiku na mchana, ili kutoa matokeo bora na ya haraka yatakayoakisi jitihada kubwa zinazofanywa na serikali ya awamu ya tano katika kuinua sekta ya mifugo nchini.

Hivyo ameagiza utafiti wa ng'ombe bora wa maziwa uwe endelevu na uwafikie wafugaji wengi zaidi na usifanyike kwa sababu ya paredi tu kwani kufanya hivyo hakutaleta matokeo ya haraka ya kuongeza kiwango cha uzalishaji maziwa nchini.

Akizungumza baada ya kushuhudia gwaride la kwanza la ng'ombe bora wa maziwa waliochaguliwa baada ya tathmini ya vinasaba kupitia Mradi wa Kuboresha Mbavu za Ng'ombe wa Maziwa Afrika (ADGG) unaotekelezwa na Taasisi ya Mifugo Tanzania (TALIRI) jijini Dodoma, Waziri Mpina alisema hatua hizo zinapaswa kuwagusa wafugaji wa chini.

Shindano hilo lilishirikisha wafugaji wa ng'ombe wa maziwa 30,900, ng'ombe waliosajiliwa 108,000, ng'ombe waliyoshinda na kufanyiwa uchunguzi wa kina ni 6,000 ambapo kati hiyo ndipo wakapatikana ng'ombe bora 40 kati ya hao majike 20 na madume 20 waliofanyiwa tathmini ya vinasaba na kupigwa mnada katika gwaride hilo na ambapo ngombe jike aliuzwa kwa Sh. milioni 6.1

Aliagiza baada ya kumaliza gwaride hilo utafiti huo uendelee, na kwamba taarifa zote ziwe zinamfikia zikiwa zinaonyesha jina la mfugaji na idadi ya mifugo iliyotambuliwa ili kuiwezesha serikali kutekeleza kikamilifu mipango yake ya kuinua sekta hiyo.

INAENDELEA UK.8



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tunamngoja nani kuinusuru Kariakoo?

**BUNGE** limeambiwa kwa kina jinsi ambavyo Soko la Kariakoo jijini Dar es Salaam lilivyo taabani, likihesabu siku za kuishi kutokana na kukimbiwa na wateja. Chanzo cha kuachwa na wanunuzi hasa kutoka nchi jirani za Uganda, Zambia, Kongo na Malawi ni ugumu wa biashara unaochangiwa na kodi.

Historia ya Soko la Kariakoo inaelezwa kuwa ilianzia wakati wa ukoloni wa Mjerumani na kwamba kiwanja lilipo soko hilo leo, ndiyo yaliyokuwa yawe makao makuu ya ofisi ya Utawala wa Serikali ya Ujerumani.

Lakini, mpango huo ulitibuliwa na Waingereza baada ya kuwashinda kwenye Vita Kuu vya Kwanza vya Dunia.

Ni baada ya Wajerumani kushindwa na Waingereza kulichukua koloni lao la Tanganyika, hatua iliyoibadilisha Kariakoo kutoka kuwa makao makuu ya Mjerumani kuwa kambi ya wanajeshi wa kubeba mizigo kwa ajili ya askari wa Kiingereza, iliyokuwa ikijulikana kama Carrier Corps.

Hiyo ndiyo asili ya Soko la Kariakoo linaloonekana leo. Kwa ujumla ni kitega uchumi ambacho serikali ilikianzisha miaka ya 1970, kazi iliyofanywa na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ambayo iliagizwa kujenga soko la kisasa na kuwapatia Watanzania mahitaji ya chakula, mavazi na bidhaa nyingine za aina zote tena likitakiwa kuwahudumia wananchi kwa miaka zaidi ya 50.

Soko hili ni mojawapo ya vivutio, alama ya utambulisho na pambo la Jiji la Dar es Salaam pengine na Afrika.

Soko la Kariakoo na jingine liitwalo Markatu lilipo Addis Ababa Ethiopia, ni miongoni mwa masoko makubwa na ya kipekee barani Afrika.

Hivyo, Kariakoo si kitega uchumi cha kuupuzwa. Ni jambo la kuhuzunisha pale Bunge linavyoelezwa kuwa soko hilo lipo kwenye hati hati, kutokana na ugumu wa biashara.

Kitovu hicho cha biashara ambacho zamani kilikuwa kimbilio la wafanyabiashara wa Zambia, Malawi, Uganda na Congo siku hizi kinaporomoka.

Sababu zimetajwa bungeni kuwa ni pamoja na utitiri wa kodi unaotozwa kwenye bidhaa unaozifanya kuwa ghali zaidi na kuwakimbiza wateja hasa kutoka mataifa ya jirani.

Huu si wakati wa kulaumiana bali ni muda wa kutafuta ufumbuzi ili kuifanya Kariakoo izidi kung'ara na kuongeza mapato ya Jiji la Dar es Salaam pamoja na serikali kuu.

Serikali ina wataalamu na wabobezi wa masuala ya biashara na namna ya kuweka mikakati ya kuvutia wateja hasa kwenye maeneo hayo.

Tunawashauri kufanya mbinu na kubuni mikakati mbalimbali itakayoliwezesha soko hilo kuwa na viwango vya juu na bora hata kuliko ilivyokuwa hapo zamani.

Pengine ni wakati wa kuweka eneo ama ukanda maalumu kwa ajili ya wafanyabiashara kutoka nchi jirani. Eneo litakalokuwa na upendeleo maalumu.

Ikumbukwe hizi ni zama za ushindani, ukienda Kenya lipo soko la Eastleigh husoma 'Islii' ambalo ni maarufu kwa bidhaa za aina mbalimbali zinazopatikana Kariakoo na linalovutia wateja kutoka sehemu nyingi za kusini na mashariki mwa Afrika.

Hivyo ni wakati wa kujua kuwa kuna ushindani, lakini Tanzania tofauti na mataifa mengine ya ukanda huu ni eneo lenye usalama mkubwa na amani.

Hizo ni baadhi ya sifa zinazoifanya Bandari ya Dar na Soko la Kariakoo kuwa kwenye chati kila wakati.

Hima serikali, mamlaka za kodi, viongozi na wadau kwenye biashara chondechonde imarisheni Kariakoo na kuirudishia hadhi iliyokuwa nayo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Polisi, TPSIS jipangeni kuwaunganisha walinzi binafsi

Na Mashaka Mgeta

**HIVI** karibuni, kumezinduliwa mpango wa kuwasajili walinzi binafsi wanaofanya kazi kwenye makazi na taasisi za kijamii.

Mpango huo uliotangazwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Huduma za Kuunganisha Walinzi Binafsi (TPSIS), Dk. David Rwegoshora, unalishirikisha Jeshi la Polisi katika utoaji mafunzo na utunzaji wa taarifa za walinzi binafsi, hasa walio nje ya mfumo wa kampuni binafsi za ulinzi nchini. Dk. Rwegoshora anasema, mpango huo hauiingizi TPSIS katika kuwaajiri walinzi, bali kuchukua na kutunza kumbukumbu zao kwa mukhtadha wa kuwawezesha kujulikana rasmi polisi, kunufaika na mafunzo na kuunganishwa na masoko ya ndani na nje ya nchi.

Hiyo ni moja ya mambo mapya ya kibunifu na yanayojenga dhana ya kuisaidia jamii, ili iendelee kuishi katika mazingira ya amani na utulivu. Hivyo, kushiriki kikamilifu katika shughuli za uzalishaji.

Dk. Rwegoshora alinukuliwa akisema TPSIS haihusiki katika kuwaajiri walinzi binafsi, isipokuwa kuwaunganisha kwenye mfumo wa utunzaji wa kanzidata (database) ambao polisi itakuwa na uwezo wa 'kuupitia' katika ngazi ya Taifa na mkoa. Pia, Dk. Rwegoshora anasema walinzi watakaojisajili kupitia mpango huo, watapewa mafunzo yenye lengo la kutambua na kudhibiti uhalifu kabla haujatokea.

Anasema mbinu na stadi hizo zinatolewa na Jeshi la Polisi, huku TPSIS ikiwa ni mratibu wa mafunzo hayo.

Kwa muda mrefu, jamii imeshuhudia makubwa ya polisi, katika kukabiliana na wahalifu. Hiyo, haishii kuhatarishi maisha ya askari vijana raia wa taifa pekee, bali kunatumia fedha nyingi ambazo kama (uhalifu) ungedhibitiwa mapema, zingeelekezwa kwenye matumizi mengine.

Pia mpango huo unajijibu kadhia mbalimbali ambazo raia wamekuwa wakizipata pindi wanapohitaji walinzi binafsi kwenye makazi yao, taasisi kama shule ama maeneo ya kufanyia biashara.

Utaratibu uliozoeleka na unaoendelea kutumiwa na jamii ni wa kuagizia mlinzi binafsi kutoka maeneo yenye jamii, zenye historia ya uthubutu katika kuifanya kazi hiyo.

Awali, raia kutoka kabila la Wamakonde waliheshimika sana kwenye maeneo ya mijini hasa Dar es Salaam, kwamba walifaa kwa huduma ya ulinzi binafsi. Baadaye, hali ilibadilika taratibu na sasa sehemu kubwa ya Wamasai wanaaminika kufaa katika utoaji huduma hiyo, ingawa wapo watu kutoka jamii nyinginezo wanaojishughulisha na kazi hiyo.

Lakini, katika hali ya kustaajabisha, si walinzi binafsi au waajiri wenye taarifa sahihi zitakazowasaidia hasa yanapotokea matatizo. Kwa maana upatikanaji wake na namna wanavyoingia makubaliano ni miongoni mwa mambo yanayofanyika 'kienyeji'.

Ndio maana niliposoma kuhusu kuzinduliwa kwa mpango huo na kwamba unapatikana kwa njia ya kujisajili kupitia mtandao unaoweza kupatikana hata kupitia simu ya kiganjani, nikaona ni fursa zinazoweka mazingira bora kwa amani, usalama na utulivu.

Pengine sasa ni jukumu la waratibu wa mpango huo, TPSIS na Jeshi la Polisi kwa ujumla, kuhakikisha kwamba maeneo kadhaa yanapewa kipaumbele na kuingizwa kwenye mafunzo ama utendaji wa aina yoyote katika utekelezaji wa mradi huo.

Maeneo hayo ni pamoja na 'kuwaivisha' wanufaika wa huduma hiyo katika uzalendo kwa nchi na watu wake. Walinzi binafsi ni nyanja inayoajiri watu wengi wanaotekeleza wajibu unaopaswa kutekelezwa na Jeshi la Polisi, kwa mujibu wa katiba ya nchi. Hivyo, watakapowekwa kwenye kanzi data na kutambulika rasmi kwa majina, sura, alama za mwili na mienendo yao, hawana budi kutambua umuhimu wao kwa jamii. Umuhimu huo unajikita katika uzalendo kwa nchi.

Pengine, ndio maana mpango huo ukaweka bayana kwamba msisitizo mkubwa wa mafunzo kwa walinzi binafsi utawekwa katika kutambua na kudhibiti uhalifu kabla ya kutokea. Ni wakati kwa walinzi binafsi na wengine watakaotambua umuhimu wa mpango huo, kujitokeza na kuunga mkono kwa vile hatua ya kuwekwa pamoja, inatoa nafasi ya kufahamiana, kubadilishana mawazo na pengine kufatuta namna nzuri ya kukabiliana ama kuzitatua changamoto zinazowakabili.

Lakini, kwa upande wa waratibu na Jeshi Polisi, hawapaswi kulidhika tu, kwamba wamefanikiwa kuwaunganisha walinzi binafsi kwa kuwaandalia kanzi data, la hasha!

Katika ulimwengu wa sasa ambapo uhalifu wa kwenye mtandao umeshamiri, lolote linaweza kutumika hata ikibidi kwa nia ovu.

Inabidi wakati wote wahusika wa mpango huo waendelee kuwa makini, ili hatimaye kufikia malengo wanayoyakusudia.

**Mwandishi anapatikana kwa simu: (+255) 0754 691540 au baruapepe: geta2000@yahoo.com.**

**MJADALA/BARUA**

## Tamisemi hiki nini shuleni?

**Mhariri,**

*NAOMBA nitoe maoni yangu kuhusiana na ufaulu wa wanafunzi wanaojiunga na shule zenye vipaji maalum.*

*Sisi wananchi maskini tunaelewa kwamba kuna Baraza la Mitihani la Taifa (Necta), kwamba ndicho chombo rasmi cha kuandaa, kutunga, kusimamia na hatimaye kutoa matokeo ya mitihani husika. Pia, iko wazi wanafunzi wanaopangwa kwenda shule za vipaji maalum kidato cha tano, ni wanaopata daraja la kwanza kwenye mtihani wa kidato cha nne.*

*Mwaka jana walijiunga vijana ambao Julai ijayo, wanajiunga kidato cha sita. Tamisemi ikawaandalia mitihani kidato cha tano kwa kile kinachosemwa 'kuwachuja' ili wabaki na 'cream' inayolenga kuzipiku shule binafsi nafasi 10 bora kitaifa, shule zinazofanya vizuri. Niseme, ni mchakato ambao haukutushirikisha wazazi na ulikuwa na maamuzi watakaopata chini ya daraja C watapelekwa katika shule nyingine. Katika kidato cha tano na sita kuna masomo ya aina mbili, 'Subsidiary' na 'Principal.' Katika 'Subsidiary' hata mwanafunzi akipata alama, 100 daraja lake linabaki 'S.*

*Masomo ya 'Principal' yana madaraja; A, B, C, C, D, E, S, F kulingana na ufaulu wa mtahiniwa.*

*Sasa katika mtihani huo, Tamisemi iliyapa masomo ya 'Subsidiary' alama sawa na 'Principal.' Matokeo yake, mwanafunzi anayefanya vizuri katika masomo ya 'Subsidiary' kuliko 'Principal' yanampandisha daraja.*

*Matokeo yake baadhi ambao hawakufanya kwenye 'Subsidiary' na wako vizuri masomo ya 'Principal' wanabaki daraja inayotabuliwa kuwa mbaya, anahamishwa shule. Kumhamisha mwanafunzi baada ya kukaa mwaka mzima shuleni, naona ni kunamchanganya na kumuongezea gharama mzazi. Anatakiwa tena kukidhi mahitaji mapya ya shule anayojiunga. Pia, wazazi tumepewa taarifa Juni 8, mwaka huu, wakati wanafunzi waliporudi nyumbani kujiandaa kuingia kidato cha sita.*

*Kwa heshima, tunaomba hili kuingiliwa kati ili kusitishwa mchakato huu, kwani unatuumiza wazazi wanyonge, huku tukiamini kwamba ni maamuzi yasiyofuata misingi ya uamuzi, sheria za mitihani na utawala*

**Mzazi R.R.K. Lulea, Simu 0755-526089/ 0755-190947**


**WASILIANA NASI:**

**TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz**


# Inapendeza wananchi wetu wanavyojisogezea zahanati




**Na Zakaria Mateko**

KATIKA juhudi za kuboresha huduma ya afya, serikali imekuwa ikijenga zahanati kila kijiji, vituo vya afya vya kata na hospitali yenye hadhi ya wilaya kila halmashauri, wananchi wapatehuduma za afya mahali walipo.

Hatua hiyo imewezesha baadhi ya wananchi katika maeneo mbalimbali hapa nchini, ambao tayari ujenzi wa zahanati, vituo vya afya na hospitali kukamilika, kuanza kupata huduma hiyo.

Yapo baadhi ya maeneo kama vile Musoma Vijijini yenye vijiji ambavyo sasa vina zahanati 28 zinazofanya kazi huku nyingine zikiendelea kujengwa, ili kuhakikisha kila kijiji kinakuwa na zahanati.

Mbali na ujenzi wa zahanati, wakazi wa vijijini pia wamekuwa mstari wa mbele kuunga mkono juhudi za serikali katika ujenzi wa vituo vya afya na sasa kipo kinachofanya kazi, huku vingine vitatu vikiendelea kujengwa.

Mkuu wa Wilaya ya Musoma, Dk. Vincent Anney, anakitaja kituo cha afya kinachofanya kazi kuwa ni cha Murangi wakati cha Kata ya Mugango, kikiwa katika hatua ya mwisho kukamilika.

Anavitaja vingine ambavyo viko katika hatua mbalimbali kuwa ni cha Kata ya Nyambono na Bukima na kwamba wananchi wamehamasika kuchangia kwa hali na mali, kusogeza huduma afya katika maeneo yao.

"Musoma Vijijini ina kata 21 na vijiji 68, wananchi wake wamekuwa wakijitolea kwa hali na mali kuchangia ujenzi wa zahanati. Vituo vya afya vya kata na hata hospitali ya wilaya inayoendelea kujengwa," anasema Dk. Anney.

Mkuu huyo wa Wilaya, anasema kila kata imekubali kuchanga Sh.milioni 7.5 kuunga mkono juhudi za serikali kwa ajili ya kufanikisha ujenzi wa hospitali ya wilaya inayojengwa katika kijiji cha Suguti.

Iwapo kila kata itafanikiwa kuchangia kiasi ambacho wamekubaliana, basi zitapatikana jumla ya Sh. 157,500,000 kutoka kwa wananchi hao, wameamua kuungana na serikali kusogeza huduma za afya.

Kwa upande wa serikali kuu, ni kwamba imetoa Sh. bilioni 1.5 katika ujenzi huo, ambao tayari majengo manane yako katika hatua mbalimbali za kukamilika na inalezwa yanatarajiwa kuezekwa mwishoni mwa mwezi huu.

Majengo hayo ni ya utawala, mapokezi (OPD), maabara, mionzi, mama na mtoto, ufuaji, dawa na la kuchomea taka, ambayo mkuu wa wilaya anasema kufikia mwishoni mwa mwezi huu yatakuwa yameezekwa.

Iwapo ujenzi wa hospitali hiyo utakamilika, baadhi ya wakazi wa jimbo hilo watakuwa wameondokana na kusafiri umbali mrefu wa zaidi ya kilomita 90 kufuata huduma za afya katika hospitali ya mkoa iliyopo mjini Musoma.

Moyo wa aina hiyo wa wananchi kuunga mkono juhudi za serikali za kusogeza huduma za afya ni za kuunga mkono na unaonyesha ni jinsi gani wanatambua afya zao.

Hilo likifanyika kote nchini, litasaidia kuwaondolea wananchi wa maeneo mbalimbali usumbufu wa kufuata huduma za afya umbali mrefu kwasababu ya ukosefu wa zahanati, kituo cha afya au hospitali.

Hatua ya wakazi wa Musoma Vijijini kujitolea kuchangia kiasi hicho cha fedha kwa ajili ya kuunga mkono juhudi za serikali za kujenga hospitali ya wilaya ni za kuigwa, inaonyesha jinsi gani wanatambua umuhimu wa huduma ya afya.

Uchangiaji huo haukuibuka tu bali wapo watu, ambao wamefanya kazi ya kuwahamasisha kuchangia juhudi za maendeleo, akiwamo Mkuu wa Wilaya, Mkurugenzi wa Mbunge wa Musoma Vijijini, Profesa Sospeter Muhongo.

Kutokana na uhamasishaji wa watu hao na wengine wengi walioshirikiana nao, wananchi wamekuwa wakijitolea kuteka maji, mchanga, mawe na kokoto kwa ajili ya ujenzi wa zahanati, vituo vya afya na hospitali.

Mkuu wa Wilaya anasema, kwa sasa imekuwa jambo la kawaida wananchi kushiriki shughuli za maendeleo bila kusukumana, kwa vile wanaelewa mchango wao ni muhimu katika kufanikisha kazi ya kusogeza huduma za afya kwenye maeneo yao.

Kwa mtindo huo wa kujitolea kwa hali na mali, wanaweza kufanikisha mpango wa Serikali wa kuwa na zahanati kila kijiji iwapo wataendelea nao, na hivyo kuifanya Musoma Vijijini kuwa na jumla ya zanahati 68.

**KABWELA** **NA FADHIL MOHAMMED**



## HABARI KITAIFA



Mlezi wa watoto wanaosumbuliwa na saratani wa Tumaini la Maisha Muhimbili, Isidora Cosmas, akitoa shukrani kwa wanafunzi wanaosomea uandishi wa habari kutoka vyuo mbalimbali, walipowatembelea watoto hao, jijini Dar es Salaam, hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wahoji maofisa NEC kuwa makada CCM

**INATOKA UK. 2**

yake kwa mujibu wa katiba, sheria na kanuni ziliopo," Jaji Kaijage alisema na kuongeza:

"Katika tume ninayoiongoza, hakuna shabiki wala mwanachama wa chama cha siasa, kama walikuwapo ni historia siyo sasa."

Jaji Kaijage alisema uchaguzi unaendeshwa kwa mujibu wa sheria na tume haiwezi kuruhusu kada wa chama kuwa sehemu ya watendaji wake na endapo wakipata taarifa za kuwapo mtu wa aina hiyo, hawatamruhusu kusimamia uchaguzi wowote.

"Pale mazingira yatalazimisha kuchukua mtu mwingine, atachukuliwa na mfano mzuri katika uchaguzi mdogo uliofanyika hivi karibuni, tulipata malalamiko kwa wakati kuwapo kwa mazingira ya aina hiyo, msimamizi aliyekuwa asimamie uchaguzi aliondolewa na kuteuliwa mwingine," alisema.

Jaji Kaijage aliongeza kuwa ni vigumu kwa tume kutambua ni lini mtu amekuwa mwanachama na lini amekoma kuwa mwanachama wa chama fulani, hivyo ni muhimu kuongozwa kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa.

Alisisitiza NEC iko wazi na kwamba makamishna wake hawapaswi kuwa makada wa vyama vya siasa, viongozi wa siasa na kama walikuwapo, kwa mujibu wa kanuni wanatakiwa kuapa na kujiondoa huko waliko kabla ya kutumikia majukumu ya tume hiyo.

**WAKURUGENZI KUTOTUMIKA**

Katika semina hiyo, Jaji Kaijage pia alieleza msimamo wa tume kuhusu kutotumia au kutumia wakurugenzi katika kusimamia uchaguzi.

Alisema NEC inaheshimu uamuzi wa mahakama uliotolewa hivi karibuni kuhusu suala hilo kwa kuwa katika utekelezaji wa majukumu yake, inaongozwa na kuzingatia katiba na sheria. "Mahakama ilitimiza wajibu wake, ikavitengua baadhi ya vifungu vya sheria vilivyokuwa vimelalamikiwa, kulikuwa na vifungu maalum vilivyolalamikiwa na mahakama ikavitengua, vile vifungu vilivyolalamikiwa na vilivyotenguliwa havitatumika katika utekelezaji wa majukumu yetu," alisema.

## Mpina awapa mtihani mgumu watafiti kilimo

**INATOKA UK. 5**

Waziri Mpina alisema serikali imejipanga vizuri kuhakikisha kwamba inashughulika na magonjwa yote yanayoathiri mifugo na kuhakikisha kwamba chanjo zote muhimu zinapatikana tena kwa bei nafuu, ili kupata ng'ombe bora wenye afya na wanaotoa maziwa mengi.

Alisema mambo ya kuuzia wafugaji chanjo zilizokwisha muda wa matumizi hayawezi kupata nafasi tena, mambo ya kuwauzia wafugaji bei za chanjo feki na kuuza bei kubwa kuliko kawaida matokeo yake wafugaji wanaingia gharama kubwa na wengine kukata tamaa na kusababisha mifugo yao kufa.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Kimataifa ya Utafiti wa Mifugo, Gimmy Symith, alisema kila nchi ambayo inafanya mchakato wa mabadiliko kuwekeza katika viwanda vya kuzalisha maziwa imeweza kubadilisha uchumi pia kwa kupitia uboreshaji wa koosafu za mifugo.

Programu ya Kuboresha Mbari za Ng'ombe Bora wa Maziwa (ADGG) inafadhiliwa na Wakfu wa Bill & Melinda Gates, na ina nia ya kukuza ushirikiano kati ya wafugaji wa ng'ombe wa maziwa nchini pamoja wadau ili kupambana na changamoto za ufugaji na kuongeza uzalishaji wa tija.

Maonyesho ya ng'ombe bora wa maziwa yalianza Jumatatu hadi juzi, ambapo ng'ombe 40 bora nchini wamebainika kuwa za uwezo wa kuzalisha zaidi ya lita 30 kila mmoja kwa siku.

## Naibu Spika amtetea mbunge aliyechana hotuba upinzani

**INATOKA UK. 5**

walioibua zogo bungeni kuhusu uamuzi uliochukuliwa dhidi ya Vuma.

Wabunge waliotolewa nje kutokana na zogo hilo ni Esther Matiko (Tarime Mjini), John Heche (Tarime Vijijini) na Dk. Emmaculate Sware (Viti Maalum) baada ya Vuma kuchana hotuba hiyo wakati akichangia mjadala wa bajeti ya serikali mwaka 2019/20.

Wabunge hao walikuwa wakipinga uamuzi wa Dk. Tulia kumtaka Vuma kuomba radhi kwa alichokuwa akizungumza wakati akichana kitabu hicho kwamba si kitendo cha kiungwana.

Dk. Tulia alichukua uamuzi huo kwa maelezo kuwa taarifa iliyoombwa na Mbunge wa Tunduma (Chadema), Frank Mwakajoka, baada ya Vuma kuchana kitabu hicho, inazungumzia Mbunge kutamka maneno yasiyoruhusiwa bungeni.

Vuma wakati akizungumzia utekelezaji mzuri wa miradi ya serikali ikiwa ni pamoja na ujenzi wa reli ya kisasa (SGR), alishika kitabu hicho cha upinzani na kusema kina maneno yasiyofaa na kinafaa kuchanwa kisha kuchana.

Jana asubuhi, Selasini baada ya kumalizika kipindi cha 'Maswali na Majibu', alisimama na kuomba mwongozo wa kiti cha Spika akisema juzi walishuhudia Mbunge Vuma akichana kitabu cha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni na maoni hayo yalipelekwa katika Bunge hilo kwa mujibu wa Kanuni namba 99 (9) na kufanya kuwa kumbukumbu rasmi za Bunge.

Akijenga hoja yake ya kutaka Vuma kupelekwa Kamati ya Maadili kuhojiwa, Selasini alisema wabunge wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni wana hasira sana na yeye ameamua kusimama kwa sababu anapenda mjadaa uliopo uendelee kwa amani.

"Jana (juzi) wakati unatoa uamuzi hapa ulimtaka aombe radhi na ukasema hakuna kanuni yoyote ambayo inaongoza anayechana kitabu kama vile hakuna kanuni rasmi ambayo inaelekeza kumbe kuna mambo yanayotakiwa tu kuamuliwa na kiti chako kwa busara."

Zaidi alifafanua: "Kwa interest (maslahi) ya kuwa na mjadala wa amani katika Bunge hili, naomba mwongozo wako kwa nini kiti chako kisimtake Vuma kuomba radhi na kiagize apelekwe kwenye kamati ya maadili ili jambo hili lisijirudie tena kwa sababu leo imechwana hotuba ya kambi rasmi ya upinzani, lakini inaweza ikatokea mtu akachana hotuba ya waziri katika Bunge ambalo linatizamwa na watu, linatazamwa na dunia na kadhalika."


ewura
Energy and Water Utilities Regulatory Authority
ISO 9001:2015 Certified

Ghorofa ya 4, Jengo la PSSSF, Barabara ya Makole
S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania
Simu: +255-26 2329002-3; Nukushi: +255-26 2329005
Barua pepe: info@ewura.go.tz Tovuti: http://www.ewura.go.tz

20 JUNI 2019

TAARIFA KWA UMMA

MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA),

INAUARIFU UMMA KUWA MIKUTANO YA KUKUSANYA MAONI YA WADAU KUHUSU MAOMBI YA **DAWASA** YA KUREKEBISHA BEI ZA MAJI KWA MWAKA 2019/20 – 2021/22, ILIYOKUWA IMEPANGWA KUFANYIKA KATIKA JIJI LA DAR ES SALAAM, MJI WA KIBAHA NA BAGAMOYO IMEAHIRISHWA HADI HAPO ITAKAPOTANGAZWA TENA.

LIMETOLEWA NA
MKURUGENZI MKUU
EWURA

215286002

# Masauni ataka ripoti nyumba za polisi

**Na Romana Mallya**

NAIBU wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni, ametoa mwezi mmoja kwa Shirika la Rasilimali la Jeshi la Polisi kutoa vielelezo kwa kamati ya tathmini iliyoundwa kwa ajili ya mradi wa ofisi ya polisi Oysterbay na nyumba za makazi ya maofisa wa polisi na askari wa kawaida.

Lengo ni majengo hayo ambayo yamekamilika tangu mwaka jana yakabidhiwe rasmi serikalini.

Masauni alitoa agizo hilo jana baada ya kufanya ziara kwenye mradi huo uliotekelezwa maeneo matatu ambayo ni Polisi Oysterbay, Mikocheni na Kunduchi.

Alisema miradi hiyo ipo chini ya shirika hilo na kwamba iliundwa kamati ya tathmini iliyokuwa chini ya Wizara ya Fedha na kuhusisha wadau mbalimbali.

"Naliagiza Shirika hili la Polisi litoe vielelezo vinavyohitajika kwenye kamati hii ambayo nayo imechukua muda, ili miradi hii ikabidhiwe na wahusika waliokusudiwa waanze kuyatumia, mradi huu ulianza mwaka 2014 na hadi sasa haujakabidhiwa licha ya kukamilika," alisema.

Masauni alisema mradi huo umehusisha ujenzi wa kituo kipya cha Polisi Oysterbay na nyumba za makazi za maofisa wa polisi pamoja na za askari kwa kutumia eneo la jeshi hilo.

"Maelekezo ya serikali yapo wazi hatutaki maeneo ya jeshi yatumike kwa ajili ya miradi binafsi hayo ni maelekezo ya Rais John Magufuli, leo (jana) nimeamua kutembea mradi huu baada ya kuona unasuasua, mradi umekamilika lakini majengo hayajakabidhiwa, huku askari wakiendelea kuishi katika majengo mabovu," alisema.

Masauni alisema kuna tatizo la kasi ambayo haiendani sambamba na ya awamu hii ya Rais Magufuli ili kumaliza mradi huo kwa misingi ya maelekezo. "Nimekuja kuona hatua iliyofikiwa na nitapata fursa kukutana na wadau mbalimbali ili kupata taarifa ya moja kwa moja ili mchakato umalizike, mradi ukiendelea bila kutumika ni kutokwenda sambamba na maslahi ya serikali," alisema.



Mkuu wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Kamishna Jenerali Thobias Andengenya, akitoa elimu ya kujikinga na majanga ya moto kwa wanafunzi wa Simiyu Sekondari. Kushoto ni Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Anthony Mtaka. **PICHA: HAPPY SEVERINE**

# Simanjiro wanufaika kilimo cha umwagiliaji

**Na Mwandishi Wetu,** SIMANJIRO

UBORESHAJI wa miundombinu ya umwagiliaji katika Halmashauri ya Simanjiro mkoani Manyara umeongeza uzalishaji wa mpunga, hivyo kuwanufaisha wakulima na kuongeza mapato ya wilaya hiyo.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake juzi, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Yefred Myenzi, alisema serikali imewekeza Sh. bilioni 2.2 katika kilimo cha umwagiliaji kwa kuboresha miundombinu ya umwagiliaji na kutoa mafunzo ya uendeshaji na utunzaji wa miundombinu hiyo.

Myenzi alisema kutokana na serikali kuchukua hatua hizo, uzalishaji wa mpunga umeongezeka kutoka tani mbili 2.5 hadi tani tisa kwa hekta kwa msimu.

Alisema kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao yanayolimwa kwa njia ya umwagiliaji, kumeinua vipato vya wananchi na wengi wao kwa sasa wanaishi maisha bora kwa kuwa wamejenga makazi bora na kusomesha watoto wao.

"Katika halmashauri yetu kilimo cha umwagiliaji kinachangia mapato kiasi cha Sh. milioni 100 hadi milioni 200 kwa mwaka," Myenzi alisema.

Mkurugenzi huyo aliongeza kuwa kilimo cha umwagiliaji kwa mazao ya mpunga, mboga na mahindi kimeleta usalama wa chakula si tu kwa wakazi wa halmashauri hiyo, bali kwa mikoa jirani kwa kuwa kilimo hicho hufanywa kwa misimu miwili kwa mwaka.

Akizungumzia changamoto zinazokabili kilimo hicho, Myenzi alisema ni pamoja na kutokuwapo kwa soko la uhakika la mazao, bei isiyokuwa na tija kwa wakulima na gharama kubwa za kusafirisha mazao kwa kuwa skimu za umwagiliaji nyingi ziko mbali na miji.

"Changamoto nyingine kwa kulima ni ukosefu wa mashine za usindikaji na kuchakata mazao mbalimbali ili kuleta mnyororo wa thamani," Myenzi alisema.

Mkurugenzi huyo alitoa wito kwa sekta binafsi na wadau mbalimbali kwenda Simanjiro kuwekeza katika kilimo cha umwagiliaji kwa kuwa wilaya hiyo ina eneo linalofaa kwa kilimo hicho lenye ukubwa wa takriban hekta 10,000.

Alisema kati ya hekta hizo, zilizoendelezwa ni 3,000 na zinazotumika kwa sasa ni hekta 1,000.

# Wanawake washirikishwe kupambana mabadiliko tabianchi

**Na Jenifer Julius,** BONN

MABADILIKO ya tabianchi yanayotokana na kuongezeka kwa kiwango cha joto la dunia, yanaendelea kuleta athari kubwa duniani.

Kunapotokea majanga yanayotokana na athari za kama vile kimbunga, mafuriko, joto na ukame waathirika wakuu ni watoto na wanawake.

Ripoti ya mwaka 2018 iliyotolewa na Shirika linalohudumia wanawake UN Women inaonyesha kuwa athari za mabadiliko ya tabianchi zinawaumiza kwa kiasi kikubwa wanawake na watoto kwa kuwa uwezekano wa kundi hilo kufa kutokana na athari hizo ni mara 14 ikilinganishwa na wanaume.

Mfano mzuri kwa Tanzania hasa sehemu za vijijini, wanawake wanatumia muda mwingi na kutembea umbali mrefu kutafuta maji kwa ajili ya matumizi ya nyumbani. Katika kijiji cha Kilole kata ya Kwamngumi baadhi ya wanawake hutumia saa tatu kuteka maji kutokana na umbali wakutoka nyumbani hadi kwenye mabomba ya maji.

Katika mkutano wa mabadiliko ya tabia nchi unaoendelea jijini Bonn, nchini German, unaojadili mikakati ya kufikia Makubaliano ya Paris ya kupunguza kiwango cha joto kufikia nyuzi 2, moja ya mijadala inayoendelea ni umuhimu wa kuwajumuisha wanawake katika mkakati huo.

Mashirika kutoka sehemu mbalimbali likiwamo Action Aid, UN Women, walifanya kongamano lililolenga umuhimu wa kuhusisha wanawake katika vita dhidi ya mabadiliko ya tabianchi na kwa vipi itawezekana kuwajumuisha wanawake katika madawati yanayohusisha na vita dhidi ya mabadiliko ya tabianchi ni moja ya mambo yanayojadiliwa kwa dhana ya kwamba wanawake wana mawazo yanayopelekwa kutoa suluhisho juu ya athari hizo kama wakipewa nafasi.

Hoja hiyo imejengwa na dhana kuwa athari za mabadiliko ya tabia nchi zinawakumba wanawake moja kwa moja, hivyo wao ndio wana majibu sahihi ya nini kifanyike ili kukabiliana na hali hiyo.

Kuwaingiza wanawake katika miradi yenye lengo la kupunguza ongezeko la joto kama vile kuwaonyesha fursa za kibiashara, ikiaminika kuwa wanawake wana mzigo kubwa wa kubeba familia na hivyo wakipewa fursa hizo watazitekeleza ipasavyo ili kusaidia familia zao.

Lengo la kufikia Makubaliano ya Paris litafikiwa kwa urahisi kama wanawake wakipewa nafasi ya kuchangia. Kiongozi wa harakati za mabadiliko ya tabianchi kutoka Shirika la Kimataifa Christian Aid, Mohamed Adoe, alisema njia nyingine ni kufanya uhamasishaji wa vijana wa kike na kuwapa fursa za kujifuza na kufahamu zaidi mabadiliko ya tabia nchi kupitia makongamano, kutengeneza wanaharakati wa mapambano dhidi ya ongezeko la joto ili wakue na uelewa huo.

Nchi kama Ujerumani, vijana wanapewa msaada kutoka mashirika mbalimbali wanapotaka kuishinikiza serikali kuchukua hatua dhidi ya athari ya mabadiliko ya tabia nchi. Serikali na mashirika yasiyo ya kiserikali yanatakiwa kutoa msaada kusaidia vikundi vya kinamama vinavyojishughulisha na teknolojia yenye lengo la kudhibiti ongezeko la joto kama vile miradi ya umeme jua, majiko ya gesi, na kaboni.

Aidha, kutambulisha teknolojia inayolenga kuwa mbadala wa visababishi vya ongezeko la joto duniani pamoja na kuwaonyesha wanawake fursa zinazopatikana kutokana na teknolojia hizo.

Kuweka usawa wa kimajukumu linapokuja kati ya mwanamke na mwanamume, kwamba wanawake na wanaume wakae kiti kimoja na kufanya maamuzi ya pamoja ni nini kifanyike ili kupambana na mabadiliko ya tabia nchi. Mei, mwaka huu serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Nje nchini Australia imepeleka wanawake 13 kutoka bara la Asia kuhudhuria kongamano la siku tatu la mabadiliko ya tabia nchi ili kujifunza mambo yatakayojadiliwa katika mkutano wa mabadiliko ya tabia nchi unaoendelea jiji Bonn, Ujerumani.

# Serikali yakiri upungufu malighafi

SERIKALI imekiri kuwa Tanzania inakabiliwa na upungufu mkubwa wa malighafi zinazotokana na mazao ya kilimo kama alizeti na ngano ambayo hutosheleza nchini kwa asilimia 40, hivyo kuilazimisha kuagiza nje ya nchi.

Akijibu swali la Mbunge wa Nsimbo (CCM), Richard Mbogho, aliyehoji serikali imetekeleza kwa kiasi gani sera ya kilimo katika eneo hilo, Waziri wa Viwanda na Biashara, Inocent Bashungwa, alisema ni kweli kuna upungufu wa malighafi jambo ambalo limewalazimisha kuchukua uamuzi huo.

Majibu hayo ya serikali yalitolewa jana bungeni Dodoma na Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Ajira na Vijana), Anthony Mavunde, kwa niaba ya Waziri Bashungwa.

Alisema mkakati wa serikali ni kuongeza upatikanaji wa mbegu bora zitakazoongeza upatikanaji wa alizeti kutoka tani 768,188 kwa mwaka 2017/18 hadi tani milioni 1.5 mwaka 2020/21.

Aidha, alisema matarajio ya mwaka 2019/20 ni kuzalisha tani 820,905 za ngano kutoka tani 56,651 mwaka 2017/18 hadi kufikia tani 100,000 ifikapo 2021/22 na matarajio ifikapo mwaka 2019/20 uzalishaji utakuwa tani 85,000 na matunda kutoka tani 2,847,094 hadi tani 5,965,027 mwaka 2021/22.

Kuhusu ni kiwango gani ambacho serikali imefanikiwa kuwashawishi wawekezaji wa ndani na nje ili kuinua ajira nchini kupitia kilimo cha malighafi hizo, Mavunde alisema kwa mazao ya kimkakati kama alizeti, ufuta, michikichi na pamba, serikali inaendelea kuhimiza wawekezaji kuzalisha mafuta ya kula.

Alisema katika kilimo cha ngano na shayiri kwa ajili ya viwanda vya ndani vinavyohitaji malighafi hiyo na usindikaji wa matunda ili kupunguza uingizaji wa bidhaa hizo kutoka nje ya nchi, serikali pia imeendelea kuwaita wawekezaji kuwekeza katika eneo hilo.

"Uhamasishaji huo umewezesha Kiwanda cha Serengeti Breweries Ltd kuongeza ununuzi wa malighafi nchini kutoka tani 4,500 mwaka 2016 hadi tani 14,292 mwaka 2018," alisisitiza.

Kuhusu ni kwa kiasi gani uingizwaji wa malighafi kutoka nje ambao serikali haipati kodi unachangia kufifisha 'balance of payment' na serikali ina mpango gani wa unatekelezwa kuinusuru, Waziri alisema nakisi kwenye urari wa malipo inaweza kuwa na athari mbaya kwa uchumi au nzuri kutegemeana na chanzo cha nakisi hiyo.

"Nakisi inayotokana na uingizwaji mkubwa wa malighafi kwa ajili ya uzalishaji viwandani inaongeza tija kwenye uchumi wa viwanda vya ndani kwa kuchochea uzalishaji wa bidhaa viwandani, kuongeza ajira, husaidia kutunisha akiba ya fedha za kigeni," alisema.



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akizungumza na Mbunge wa Kijitoupele, Shamsi Vuai Nahodha, bungeni jijini Dodoma. **PICHA: PMO**

# Miundombinu rafiki kwa wenye ulemavu sasa kujengwa shuleni

KUANZIA sasa shule zote za msingi na sekondari nchini, zitalazimika kujengewa upya miundombinu ya vyoo na madarasa yanayozingatia mahitaji ya watu wenye ulemavu.

Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Mwita Waitara, alisema uamuzi huo umefikiwa baada ya serikali kubaini changamoto hiyo ya uhitaji wa wanafunzi na walimu wenye mahitaji maalum.

Kutokana na uhitaji huo, alisema serikali imeandaa mpango mkakati wa elimu jumuishi ambao pamoja na mambo mengine, unaelekeza ujenzi wa shule hizo kuzingatia mahitaji ya makundi ya watu wenye ulemavu.

Waitara alikuwa akijibu swali la msingi la Mbunge wa Viti Maalum (CUF), Nuru Bafadhili, aliyetaka kujua serikali ina mpango gani wa kuhamasisha ujenzi wa vyoo vinavyokidhi matakwa ya walemavu katika shule za sekondari na msingi.

"Ili kuhakikisha kuwa azma ya serikali kuwa miundombinu inakuwa rafiki kwa makundi yote, serikali imetoa maelekezo kwa Makatibu Tawala wa Mikoa (RAS) na wakurugenzi wa mamlaka ya serikali za mitaa wote nchini kuhakikisha ujenzi wa shule zote unazingatia mahitaji ya watu wenye ulemavu," alisema Naibu Waziri huyo.

Kwa mujibu wa Waitara, ramani za sasa za ujenzi wa miundombinu ya matundu ya vyoo na vyumba vya madarasa zinazingatia mahitaji ya watu wenye ulemavu.

Alisema ramani hizo zinazingatia pia makubaliano ya serikali yaliyofikiwa wakati wa utekelezaji wa programu ya School Water and Sanitation Hygiene (SWASH) ambapo vyoo bora hujengwa ikiwa ni pamoja na chumba maalum cha watoto wa kike.




**Habari zote na Godfrey Mushi,** DODOMA

## India yatoa mabilioni kuboresha huduma maji

NAIBU Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, amesema serikali imepata Dola milioni 500 za Marekani kutoka serikali ya India kwa ajili ya uboreshaji wa huduma ya maji.

Aweso aliyasema hayo jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Kilombero (Chadema), Peter Lijualikali.

Katika swali lake la msingi, Lijualikali alitaka kujua serikali ina mpango gani wa kuongeza mtandao wa maji katika Mji wa Ifakara ambao kwa sasa ni asilimia 40 tu.

Naibu Waziri alisema fedha hizo zitatumika kwa ajili ya kuboresha huduma za maji katika miji 28 ya Tanzania Bara na Zanzibar, ikiwamo Ifakara.

Alisema kwa sasa taratibu za kuwapata wataalamu washauri watakaofanya usanifu wakina na uandaaji wa makabrasha ya zabuni zinaendelea.

"Ni matarajio kuwa ujenzi wa miradi hiyo utaanza katika mwaka wa fedha wa 2019/20," alisema.

Alisema kukamilika kwa mipango hiyo kutaboresha hali ya upatikanaji wa maji katika Mji wa Ifakara kufikia asilimia 90 ifikapo mwaka 2020.

Awali Naibu Waziri huyo alisema katika mpango wa muda mfupi serikali kupitia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro imekamilisha mradi wa uboreshaji wa huduma ya maji.

## Serikali yatekeleza Mpango wa Elimu 2020/21

BUNGE limeelezwa kuwa kwa sasa serikali inatekeleza Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Elimu wa miaka mitano kuanzia 2016/2017-2020/21.

Kauli hiyo ilitolewa jana bungeni na Naibu Waziri Ofisi ya Rais Tamisemi, Mwaita Waitara, alipokuwa akijibu swali la Dk. Mary Nagu (Hanang-CCM).

Katika swali lake Nagu alitaka kujua serikali ina mpango gani mbadala wa mradi wa MMEM ili kusaidiana na wananchi katika ujenzi wa miundombinu ya shule za msingi.

Alisema katika mpango huo ambao unajumuisha elimu ya msingi serikali imekuwa ikijenga miundombinu mipya pamoja na ukarabati na umaliziaji wa miundombinu ya shule zilizojengwa kwa nguvu za wananchi.

Naibu huyo alisema baadhi ya programu zinazosaidia kutekeleza mpango huo ni pamoja na programu ya Lipa kulingana na matokeo EP4R.

Alisema programu nyingine ni kukuza stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu na mradi wa kuinua ubora wa elimu ya msingi nchini. Naibu huyo alisema katika mwaka wa fedha 2018/19 serikali kupitia mradi wa EP4R imeweza kujenga na kukarabati miundombinu ya shule yenye thamani ya Sh. bilioni 13.2.

Alisema fedha hizo zilitumika kwenye shule za msingi 214 na Sh. bilioni 35.4 kwa shule za sekondari 285.

Aidha, alisema shule tano za mfano za msingi zilijengwa kwa gharama ya Sh. bilioni 3.5 kupitia programu hiyo na umaliziaji wa maboma 2,761 ya vyumba vya madarasa na matundu ya vyoo 669 kwa gharama ya Sh. bilioni 35.25.

"Kwa sasa jumla ya Sh. bilioni 15.2 zimetumwa moja kwa moja shuleni kwa ajili ya ukarabati wa shule kongwe 17 za sekondari na ukarabati huo unafanyika kwa njia ya "Force Account" kwa kutumia mafundi wa maeneo yaliyopo shule katika hizo," alisema.

# CCM yawataka vijana wanaohitimu vyuo vikuu kuibadilisha jamii

**Na Allan Isack,** ARUSHA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimewataka vijana wa chama hicho wanaohitimu elimu katika vyuo mbalimbali kutumia mafunzo hayo kuleta mabadiliko chanya katika jamii badala ya kutengeneza migogoro na makundi.

Akizungumza jana wakati wa hafla fupi kwenye mahafali ya wahitimu wa vyuo vikuu katika Mkoa wa Arusha, Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM anayewakilisha vijana, Mussa Mwakitinya, alisema kumekuwa na changamoto kubwa kwa vijana kutokushirikiana na jamii baada ya kuhitimu mafunzo yao.

Mwakitinya alisema vijana wengi wamekuwa hawashirikiani na jamii kwa dhana walizojijengea kuwa wao ni wasomi na hawawezi kufanya kazi na watu ambao hawajasoma.

"Vijana tuache urasimu kuwa sisi tumesoma, lakini hatuwezi kushirikiana na watu ambao hawajasoma katika jamii. Tumieni maarifa na ujuzi mlioupata vyuo kuleta mabadiliko ya kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni katika maeneo mliyotokea," alisema.

"Mnapokwenda mtaani nendeni mkaishi ndani ya imani za chama chetu kama miongozo inavyotuelekeza na mkatumie elimu zenu kuielimisha jamii kwa hoja mahsusi, kwa mifano halisi ya mambo yaliyofanywa na serikali," alisema.

Pia aliwataka vijana kutumia mafunzo hayo kujiajiri na kujitoa kwa moyo mmoja katika hatua ya kukijenga chama kwa maslahi ya taifa na vizazi vijavyo. Katibu wa CCM Wilaya ya Arusha Mjini, Denis Mwita, aliwataka vijana hao wanapokwenda katika jamii wakafanye siasa za kistaarabu na wakashirikiane na kutoa ushauri kwa viongozi wa chama wakaowakuta huko.

Naye Katibu wa CCM Mkoa wa Arusha, Mussa Matoroka, aliwataka vijana wa CCM kujitokeza kugombea nafasi mbalimbali za uongozi katika uchaguzi wa serikali za mitaa, utakaofanyika Oktoba mwaka huu na uchaguzi mkuu wa mwakani.

Alisema chama kinatambua mchango wao kwa kuwa kwa miaka mitatu waliokaa katika mkoa huo wamerudisha uhai wa chama ndani ya vyuo na nje. Mjumbe wa NEC, Anna Msuya, alisema chama chochote duniani ili kishike dola kinayahitaji makundi mawili, vijana na wanawake, kwa hiyo huo ndio mtaji mkubwa wa chama.

Msuya alisema awali uongozi wa vyuo mkoani hapa ulikuwa ukishikiliwa na wanafunzi kutoka vyama vya upinzani, lakini baada ya mabadiliko makubwa ndani ya chama nafasi hizo zilirudi ndani ya CCM. Akisoma risala mbele ya mgeni rasmi, Katibu wa Seneti ya Vyuo Vikuu Mkoa wa Arusha, Wema Somba, alisema awali idara ya vyuo na vyuo vikuu kabla ya mabadiliko ya kanuni za Umoja wa Vijana CCM (UVCCM) ya mwaka 2014, ilikuwa ikitambulika kama shirikisho la vyuo na vyuo vikuu.

Alisema shirikisho hilo, lilianza likiwa na vyuo vitatu vikiwamo Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira, Chuo cha Uhasibu Arusha na Chuo Kikuu cha Arusha wakiwa na jumla ya wanachama 149.

Alisema Idara ya Vyuo Vikuu imeundwa kwa mujibu wa kanuni za Umoja wa Vijana toleo namba 2017 kwa lengo la kuwaandaa vijana wasomi kuwa wanachama bora katika jumuiya zake. Aidha, alisema hadi mwaka huu, chama hicho kimeongeza vyuo kufikia 13 na ongezeko la wanachama 7,408, sawa na asilimia 60.



Mbunge wa Jimbo la Simanjiro mkoani Manyara, James Ole Millya (kushoto), akisikiliza maelezo ya miradi mbalimbali ya maendeleo kwa Ofisa Mtendaji wa Kata ya Orkesumet, Edmund Tibiita, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

## Shirika lakabidhi tochi kufukuza wanyama wakali

**Na Zanura Mollel,** ARUSHA

SHIRIKA la Maendeleo ya Jamii la Oikos (EA), linalofanya kazi katika Wilaya ya Longido chini ya ufadhili wa Umoja wa Ulaya (EU), limekabidhi tochi maalumu kwa jumuiya ya hifadhi ya wanyamapori Enduiment (Ewma) kwa ajili ya kufukuzia wanyama wakali maeneo ya kilimo na ufugaji.

Mratibu wa mradi wa kudhibiti migongano baina ya wanyama na binadamu kutoka Oikos, Paschal Simon, alisema lengo la kutoa tochi hizo ni kuondoa migogoro baina ya wanyama, mifugo na binadamu ndani ya hifadhi ya Ewma.

Alisema tochi hizo ni michango ya wananchi 18 ambao walichanga fedha nusu na shirika nalo likawaongezea na kwamba zina uwezo wa kukaa na moto hadi saa 48, kutokana na matumizi ya mtu binafsi.

"Tulikubaliana wananchi wachangie asilimia 50 na shirika nalo asilimia 50. Kati ya wananchi 18 waliochanga fedha hizo, kila mmoja alitoa Sh. 168,750," alisema Simon.

Kwa mujibu wa Simon, tochi hizo zilichelewa kuwafikia walengwa kwa wakati kutokana na shirika kuagiza nchini China, huku kukiwa na ongezeko la thamani kwa kodi na gharama za usafirishaji.

"Tulivyoagiza kiwandani huko China walituambia hawawezi kutuma mzigo wa tochi 18 labda muagize kuanzia 500. Wananchi watusamehe kwa kuwachelewesha, si makosa yetu na hatukukusudia kuchelewesha," alisema.

Alisema tochi za awali walizokuwa wanategemea kuzipata zimekosekana na kupata za aina nyingine ambazo moja ina thamani ya Sh. 413,000, huku zote 18 zikiwa na thamani ya Sh. milioni 7.4.

# Camartec kutengeneza mashine za korosho

**Novatus Makunga,** ARUSHA

KITUO cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini (Camartec), kimeanza rasmi mchakato wa kutengeneza mashine za kubangulia korosho, kwa ajili ya viwanda vidogo vyenye uwezo wa kubangua kati ya kilo 500 hadi 1,500 kwa siku.

Mchakato huo pia unazihusisha taasisi zingine zilizoko chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara ambazo ni pamoja na Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda (Tirdo), Taasisi ya Uhandisi na Usanifu Mitambo Tanzania (Temdo) na Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (Sido). Mkuu wa Masuala ya teknolojia wa Camartec, Godfrey Mwinama, aliiambia Nipashe mjini hapa juzi kwamba mkakati huo umelenga kuwa na ubanguaji endelevu wa korosho utakaohusisha wazalishaji wa ngazi ya chini, wakiwamo wajasiriamali wa vijijini, vikundi vya wakulima na vyama vya ushirika vya masoko ya kilimo (Amcos).

Alisema viwanda hivyo vidogo vitajikita zaidi katika ubanguaji wa korosho wa awali ambao unahusisha kuondoa ganda gumu na kuziuza kwa kundi lingine la wawekezaji, ambao watajihusisha na kumenya ganda la ndani, kuzikausha na kisha kuzifungasha tayari kwa kuziuza.

Mwinama alisema mfumo huo unafanana na ule unaotumika katika kahawa ambapo wakulima huchakata mpaka hatua ya kupata kahawa iliyokaushwa yenye ganda laini kisha kuuzwa na kupelekwa viwandani.

"Tunajenga kiwanda darasa wilayani Ruangwa mkoani Lindi kabla ya kufikia mwishoni mwa mwaka huu kwa lengo la kuwa na eneo maalumu la kufundishia wakulima, wajasiriamali na mafundi wa mashine jinsi ya ubanguaji wa korosho na teknolojia yake," alisema.

Mwinama alisema Camartec itakuwa na jukumu la kutengeneza mashine ya kupanga madaraja na mtambo wa kuchemshia korosho ghafi, mashine ya kubangulia kwa kutumia mikono na miguu, mashine za kubangulia zinazotumia umeme na mafuta pamoja na mashine ya kupanga korosho kwa ajili ya ubanguaji.

Alisema sehemu kubwa ya mashine zitatengenezwa nchini, isipokuwa chache zitakazoagizwa nje ya nchi ambazo alizitaja kuwa ni pamoja na mtambo wa kunyevushia korosho, mashine ya kumenyea na mashine ya kufungasha. "Wenzetu wa Sido watakuwa na jukumu la kufundisha na kusambaza teknolojia kwa watumiaji na watengenezaji wa mashine kwa kushirikiana nasi yaani Tirdo, Temdo na Camartec," alisema. Mwinama alisema kuanzishwa kwa viwanda vidogo vya kubangulia kutawezesha kuongeza thamani kwa zao la korosho, kuongeza ajira kwa Watanzania na kujenga uwezo wa ndani katika ujenzi wa viwanda vya kuchakata korosho.







Charles Renatus akionyesha moja ya bustani anayolima mboga aina ya mchicha katika bonde la kilimo Buswelu Wilaya ya Ilemela juzi, eneo ambalo Manispaa ya Wilaya hiyo imeanza kupima na kuweka bikoni. **PICHA: ELIZABETH FAUSTINE**

# Tasaf kutumia Tehama kuondoa kaya feki

**Na Mary Mosha,** SIHA

WILAYA ya Siha, mkoani Kilimanjaro ni miongoni mwa wilaya tatu ambazo zitaanza kipindi cha pili cha mpango wa uhaulishaji wa fedha kwa kaya maskini ambao unatekelezwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf III).

Mpango huo utatekelezwa kwa majaribio katika kata 17 za wilaya hiyo, kwa kuainisha wanufaika walioachwa kipindi cha kwanza cha awamu ya tatu utakaofanyika kwa mfumo wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Tehama).

Taarifa ya Mkurugenzi Mtendaji wa Tasaf, Amedeus Kamagenga, ilieleza kuwa mpango huo wa majaribio wa utambuzi wa kaya za walengwa wa mpango wa kunusuru familia masikini, utafanywa kwa Tehama kuepuka changamoto za awamu zilizopita.

Alisema kutumia mfumo huu kutarahisisha mawasiliano na kupunguza muda wa ufanyaji kazi hiyo, ikiwa ni pamoja na kuhakikisha hakuna kaya yenye mahitaji itakayoachwa katika utambuzi.

"Zoezi hili linahitaji uwajibikaji wa hali ya juu na katika kuhakikisha hilo, watendaji wote wamerudia viapo vyao na watapewa simu za vitonge (tablate) vya kuweka picha za kaya, lakini ni lazima zianze na taarifa sahihi ili iwe rahisi kubaini iwapo kumefanyika makosa," alisema Mkurugenzi Tasaf.

Akifungua mafunzo ya kuanza awamu hiyo wilayani Siha, Mkuu wa Wilaya ya Hai, Onesmo Buswelu, aliahidi kuwashughulikia watendaji watakaoshindwa kuwajibika kwa uaminifu katika mradi huu.

Aliwataka watendaji kuwa wazalendo katika kuisaidia kuondokana na umaskini ambao unarudisha nyuma maendeleo, huku akitoa rai kwa wananchi kutoa taarifa sahihi za maisha kwa kaya zenye uhitaji ili kupunguza malalamiko ya kuachwa kwa walengwa.

Zuhura Mdungi ni mtaalamu wa mawasiliano kutoka Tasaf, akitoa maelezo yake, alisema kazi hiyo ni kwa majaribio na inafanyika katika wilaya za Siha na Mtwara.

Alisema ndizo ambazo wamelenga kufanya majaribio ya mfumo wa Tehama na si uhakiki wa uandikishwaji kaya maskini bali kuondoa kaya hewa.

"Mfumo huu wa Tehama unakuja na majibu ya changamoto zilizosababisha kuwapo kwa kaya hewa kwani baadhi ya watendaji hawakuwa waaminifu katika kujaza madodoso yaliyokuwa yakitumika pamoja njia za kusafirisha karatasi hizo bado hazikuwa rafiki, hivyo kusababisha baadhi ya taarifa kutofika kwa wakati," alisema Mdungi.

Diwani Juma Jani wa Sanya Juu, ni miongoni mwa walipokea mafunzo hayo, aliwataka wataalamu hao kufika wenyewe katika vijiji hivyo na kupokea taarifa za kaya maskini.

Alihidi kuwapa ushirikiano wa hali na mali ili kutokomeza kaya hewa kutokea katika wilaya hiyo.

"Tumepata mafunzo tumeelewa, tutakwenda kwenye kata zetu na kuhamasisha wananchi kujitokeza kwa wingi kwa ajili ya zoezi hili la utambuzi wa kaya za walengwa wa mpango wa kunusuru kaya maskini kwa mfumo wa Tehama, " alisema Dankan Urassa Diwani wa Kata ya Karansi.

## Wazawa walalamikia kuumizwa na kodi

**Na Mary Mosha**, MOSHI

WAWEKEZAJI wazawa mkoani Kilimanjaro wameiomba serikali kuwaangalia na kuwapunguzia utitiri wa kodi unaowakwamisha.

Walisema lengo la kufanya hivyo ni kuimarisha uwekezaji pamoja na kutoa ajira kwa vijana ili kupunguza umaskini.

Akizungunza na Nipashe Meneja Msaidizi wa Marenga Milis, Priva John, aliyejikita kwenye kuzalisha unga na vyakula vya nafaka, aliomba serikali iangalie namna ya kupunguza mrundikano wa kodi unaowakabili wawekezaji wa ndani.

Mrundikano huo alisema unawakwamisha hasa wawekezaji wazawa wenye mitaji midogo.

Alisema ikiwa serikali itapunguza kodi wazawa wataimarisha thamani za bidhaa wanazozalisha kwa kuwa na bei nafuu kwa wateja wao.

"Tunaiomba serikali pamoja na halmashauri kuangalia namna bora ya kumvutia mwekezaji mzawa, ili aweze kumudu gharama za uzalishaji ili azalishe bidhaa zenye ubora kwa bei nafuu," alisema mwekezaji huyo.

Baadhi ya wafanyabiashara katika Manispaa ya Moshi, Elia Mallya, alisema ikiwa serikali ina nia ya dhati ya kwenda kwenye taifa la viwanda ni lazima kuwatizama wawekezaji wazawa na kuwapunguzia mzigo wa kodi.

Alisema ikiwa watapunguziwa mzigo wa kodi watazalisha kwa wakati na bidhaa zenye ubora ambazo bei zake zitakuwa nafuu kwa walaji.

Mwekezaji mwingine Mwanaisha Mzava, alisema mbali na bidhaa hizo kuzalishwa kwa gharama kubwa na kushindwa kuuza bei ambayo ni ya kawaida, lakini pia wanashindwa kuwalipa wafanyakazi mishahara bora kutokana na faida ndogo,

Akijibu malalamiko ya mishahara midogo inayotelewa na baadhi ya wawekezaji kwenye viwanda vyao, Ofisa Kazi Mfawidhi Mkoa wa Kilimanjaro, Mwinyimkuu Mturuya, alisema idara inaendele kutoa elimu juu ya haki na wajibu wa wafanyakazi pamoja na waajiri.

# Wakulima waomba serikali iongeza bei

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WANACHAMA wa vyama vya ushiriki vya wakulima wanaozalisha kahawa wa Uru mkoani Kilimanjaro, wameiomba serikali kusaidia kuongeza bei ya kahawa ili ifikie angalau Sh. 5,000 kwa kilo.

Wazalishaji hao walisema bei ya sasa ni Sh. 3,000 ambayo ni ndogo ikilinganishwa na thamani ya kahawa duniani, na kwamba ongezeko la bei litawawezesha wakulima wa kahawa kuzalisha kwa wingi, kuzingatia ubora na kukuza pato lao na la taifa.

Aidha, wameomba kurudishiwa mfumo wa kuwakopesha pembejeo za kilimo ili waweze kuzalisha kahawa nyingi zaidi na yenye tija sokoni.

Mwenyekiti wa Muungano wa Vyama vya Ushirika Uru Njari, Felix Masao , alitoa ombi hilo kwenye mahojiano maalumu na gazeti hili kuzungumzia hali ya uzalishaji kahawa.

Alisema ikiwa wakuliwa watatazamwa kwa jicho la pekee wataleta mabadiliko ikiwa ni pamoja na kuondoa umaskini kwa jamii.

Masao alisema licha ya kahawa kwa sasa kushuka bei, mwamko wa wakulima ni mkubwa ukilinganisha na kipindi cha nyuma.

Alisema endapo serikali ingeongeza bei ya zao hilo ingesaidia kwa kiasi kikubwa kukuza ari ya mkulima aliyekata tama, huku akiwaomba kuendelea kuwapa miche ya kisasa itakayosaidia kuleta mabadiliko katika kilimo.

"Kwa kweli mwamko wa ulimaji wa kahawa ulivyo sasa ni mkubwa, ni rai yangu kwa serikali imwangalie mkulima huyu ambaye alikuwa amekata tama, lakini ameamua kurudi tena ila bei iko chini ukilinganisha na mazao mengine hasa korosho," alisema.

Prof. Mauki mkulima wa kahawa, aliliambia gazeti hili kuwa, kutokana na mkulima kutambua umuhimu wa zao hilo, ni vyema serikali ikaweka utaratibu wa kuvikopesha vyama vya msingi pembejeo ili wakawasaidie wakulima waliopo vijijini.

"Ombi langu kubwa kwa serikali ivikopeshe vyama vya ushirika pembejeo za kilimo ili waweze kuwakopesha wakulima na kuwakata kidogokidogo wanapoleta kahawa yao," alisema.

Aidha, Ofisa Kilimo wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, Chikira Mcharo, alikiri kuwapo kwa changamoto hizo, huku akiwataka wakulima kutokukata tama.

Mcharo pia aliwataka wakulima kutoka katika vyama vya ushirika kubadilisha miche ya zamani iliyopo mashambani na kuweka miche aina ya vikonyo kutoka taasisi ya utafiti wa kahawa ya TaCRI.

Alisema kahawa aina ya vikonyo haishambuliwi na wadudu na magonjwa kirahisi na kwamba huzaa sana na haihitaji dawa nyingi kama kahawa ya zamani.

# ama

ALHAMISI JUNI 20, 2019

AFYA NA MAZINGIRA



**Wenye wazazi waliotengana watoto wao wanenepa ovyo**

Ukurasa 17



Mabingwa CCBRT wawaponyesha bure watoto wagonjwa wa miguu kifundo

Ukurasa 20



Ukurasa 16

## Prof. Mkumbo: Dawasa wajibikeni kipindupindu kinachosambaa Dar




### BINGWA OCEAN ROAD:

# Wanandoa wawakimbia wenza wenye saratani

Ukurasa 14



Dawa mbalimbali. **PICHA: MTANDAO.**

## Waafrika wanunua dawa 85% kuliko wazungu

WATAALAMU wanasema kwamba, katika nchi za Afrika inaelezwa kuwa zinatumia gharama kubwa katika matumizi ya dawa mara 30 zaidi, kuliko nchi zilizoendelea kama Uingereza na Marekani.

Mkurugenzi wa Sera za Afya katika Kituo cha Maendeleo ya Afya Duniani, Kalipso Chalkidou, anasema hali ya ushindani wa soko la dawa haliko sawa duniani.

Anasema, uwiano ulioko ni kwamba katika nchi maskini wamekuwa wakinunua dawa nyingi za bei kubwa, kutokana na kukosekana vikwazo vikubwa katika hilo, wakati nchi tajiri ni wanunuzi wa dawa kidogo na za gharama kubwa.

Kalipso anasema, nchi maskini zimekuwa wateja wakuu wa asilimia 85 ya dawa zinazozalishwa na nchi tajiri, huku zikiwa na uwezo mdogo wa kupatana bei, hata michakato yao ya ndani inakabiliwa na ufisadi.

Anasema, ununuzi katika nchi tajiri unakabiliwa na vikwazo na masharti mengi ya kisheria na kanuni za kiafyza, zinazopunguza hata kiwango cha dawa zinazotumika.

Kwa mujibu wa Kalipso, kuna wakati zinapitia mikononi mwa wafadhili. Anaongeza: "Bila ya kuwapo kanuni na sheria, watu wanadhani dawa hazifanyi kazi kumbe kuna ukiukwaji wa kanuni."

Maoni ya kitaalamu yaliyopo sasa ni Shirika la Afya Duniani (WHO), linapaswa kuingilia kati kuweka sawa sera na miongozo mingine ya kiafya. BBC

AFYA

BINGWA OCEAN ROAD:

# Wanandoa wawakimbia wenza wenye saratani

- Awajuza haiambukizi, X- Ray nayo salama
- Asisitiza wagonjwa wasikose mboga majani
- Kila vifo sita duniani, mmoja wao saratani

**NA VERONICA MREMA**

SARATANI kwa asili yake inaangukia kundi la magonjwa yasiyo ya kuambukiza au kitaalamu inatamkwa 'non - communicable disease' (NCDs).

Licha ya ukweli huo kitaalamu, lakini uzoefu wa maisha ya kawaida yana yake tofauti. Imebainika kwamba, katika hilo baadhi ya wenza huwakimbia wenzao katika ndoa, wakihofu kuambukizwa saratani.

Hali hiyo ni matokeo ya uelewa duni uliopo kwenye jamii juu ya ugonjwa huo. Kimsingi, mtu hawezi kupata saratani kwa njia ya kuambukizwa.

**KWANINI SARATANI?**

Wataalamu wanataja vyanzo vingi, ikiwamo mtindo wa maisha, ulaji usioendana na kanuni bora za lishe, utumiaji vyakula vyenye mafuta mengi, chumvi iliyozidi, uvutaji sigara, unywaji pombe na kutokufanya mazoezi. Vyote vinaangukia katika vihatarishi.

Kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), magonjwa yasiyoambukiza yanajumuishwa na maradhi kama saratani, moyo na kisukari. Hivi sasa, ni tishio na yanatajwa kusababisha vifo vya watu wengi duniani.

Takwimu za WHO zinaonyesha, wakati saratani inashika nafasi ya pili kusababisha idadi kubwa ya vifo vya takriban watu milioni tisa kila mwaka duniani, nafasi ya kwanza inashikwa na maradhi ya moyo, yanayosababisha vifo vya watu milioni 18, kila mwaka.

Pia, WHO inawasilisha sura nyingine ya takwimu za saratani, kwamba ni chanzo cha wastani wa kifo cha mtu mmoja kati ya sita duniani. Hapo matumizi ya tumbaku yanachangia asilimia 22 ya vifo hivyo.

Katika kiwango hicho cha vifo, WHO inatoa elimu zaidi kwamba nusu ya vifo hivyo, vinaweza kuzuilika.



Tabibu Bingwa wa Taasisi ya Saratani ya Ocean Road, Dk. Nuru Mlagalila. **PICHA: VERONICA MREMA.**

> **"Ila wapo baadhi ambao huja kwa kificho wenyewe kuuliza jinsi gani anaweza kuishi na mwenza wake asiambukizwe saratani..."**

**TAASISI SARATANI**

Ilivyo nchini, takwimu za Taasisi ya Saratani Ocean Road (ORCI), zinaonyesha saratani ya mlango wa kizazi iko juu kwa kuchangia asilimia 31 ya wagonjwa; matiti asilimia 13; njia ya chakula asilimia 10; na saratani ya ngozi inachukua asilimia tisa.

Akizungumza na Nipashe ofsini kwake, Bingwa wa Magonjwa ya Saratani ORCI, Dk. Nuru Mlagalila, anasema changamoto kubwa wanayoona ni wagonjwa kuchelewa matibabu.

"Wagonjwa wengi tunaowapokea hapa huwa wameanzia kwenye tiba asili na tiba mbadala. Kutokana na hali hiyo hufika wakiwa wamechelewa, ugonjwa ukiwa hatua ya tatu na nne, hizi ni hatua za juu mno za ugonjwa," anasema.

Dk. Nuru anasema, hivi sasa jamii haina uelewa wa kutosha kuhusu magonjwa ya saratani na kuwapotaarifa potofu kunachangia wengi wao kuchelewa matibabu.

"Unakuta mtu anakosa choo kwa mfano siku moja, mbili, mwezi mmoja, miezi kadhaa au anatoa choo chenye damu, anashauriwa ale mapapai, parachichi au mboga za majani," analalamika na kuongeza:

"Au anashindwa kupumua vizuri na hata kumeza chakula anaambiwa amerogwa, anashauriwa kwenda kwenye tiba asili, hadi anakuja kufika hospitalini kwa uchunguzi na kugundulika anaugua saratani anakuwa amechelewa."

**WANANDOA**

Anasema, kutokana na uelewa mdogo uliopo kwenye jamii juu ya magonjwa ya saratani wapo baadhi ya wanandoa ambao wenza wao wanapogundulika kuwa wanaugua saratani hujawa na hofu kwamba watawaambukiza.

"Huwa tunapata hizo kesi, yaani mwenza mmoja anagundulika kuugua saratani, mwenzake anapata hofu kwamba ikiwa ataendelea kuishi naye anaweza kuambukizwa.

"Hapo sasa inatulazimu kumpatia elimu mwenza huyo kwamba saratani si ugonjwa wa kuambukiza, haiambukizi lakini mtu anaweza kurithi kwenye vinasaba.

"Lakini, ikiwa mgonjwa ana maambukizi ya magonjwa mengine kwa mfano Ukimwi ikiwa unamuhudumia basi unapaswa kuwa makini, ili kuepuka maambukizi.

"Kusema kweli, wapo baadhi ya wagonjwa wetu ambao wanakimbiwa na wenza wao wakiwa kwenye matibabu, wakirejea nyumbani wanakuta wameoa au kuolewa na wenza wengine.

"Ila wapo baadhi ambao huja kwa kificho wenyewe kuuliza jinsi gani anaweza kuishi na mwenza wake asiambukizwe saratani, tunawaelimisha haiambukizi, basi wanarejea nyumbani maisha yanaendelea," anasema.

**RIPOTI YA IARC**

Ripoti iliyotolewa ya Taasisi ya Kimataifa ya Utafiti wa Saratani (IARC) inaonyesha mwaka 2018, zaidi ya wagonjwa wapya milioni 18 wa saratani wameripotiwa duniani.

Aidha, kuna vifo vya zaidi ya milioni 9.5 duniani kutokana na

Inaendelea Uk. 15

AFYA

# Wanandoa wawakimbia wenza wenye saratani



Mgonjwa aliyepona saratani ya matiti, akitoa ushuhuda. **PICHA: MTANDAO.**

**Inatoka Uk. 14**

ugonjwa huo katika kipindi hicho.

Ripoti hiyo ya IARC iliyopatiwa jina 'Mzigo wa Saratani Duniani kwa mwaka 2018' ilihusisha takwimu zilizokusanywa kutoka nchi 185 na kugusa aina 36 za saratani.

IARC linasisitiza vifo vitokanavyo na magonjwa ya saratani, vinategemewa kuongezeka kufikia milioni 24 ifikapo 2035, iwapo juhudi za kinga na tiba hazitaimarishwa duniani kote.

Wanawake wanaougua saratani ya matiti duniani, wako juu kwa kiwango cha asilimia 25.2 au robo ya wagonjwa wote, ikifuatiwa na saratani ya utumbo mpana, asilimia 9.6; mapafu asilimia 8.4; na saratani ya mlango wa kizazi, asilimia 6.6.

Aidha, katika kundi la wanaume, saratani ya mapafu inaongoza kwa asilimia 14.5; ikifuatiwa na saratani ya tezidume asilimia 13.5; utumbo mpana asilimia 10.9; na saratani ya tumbo asilimia 7.2.


**TIBA MIONZI**

Dk. Nuru anabainisha, njia ya matibabu kupitia tiba mionzi imekuwa shida nyingine kwa wagonjwa, akifafanua: "Kuna changamoto ya uelewa. Baadhi ya wagonjwa tunapowaeleza kwamba sasa wanapaswa kutibiwa kwa mionzi, wapo ambao hukimbia matibabu.

"Hofu yao kubwa ni kwamba, mionzi inaua, ndiyo uelewa uliopo kwenye jamii. Ieleweke kwamba, mionzi tunayotoa hapa ORCI katika kutibu saratani, ni mionzi salama. Tunatoa tiba kulingana na vipimo vya kitaalamu katika kiwango cha hali ya juu," anasema.

Daktari huyo anaongeza: "Hatuwezi kusema moja kwa moja kwamba mionzi haina athari. Zipo, lakini ni ndogo ndogo kwa mfano kuharisha, kutapika, au kupata mabaka mabaka kwenye ngozi.

"Kiukweli, hakuna tiba isiyo na athari ndogo ndogo. Athari zile huwa ni za muda tu na baadaye hupotea, lakini tunatamani angalau wagonjwa wawahi katika hatua ya kwanza na ya pili ya ugonjwa.




**"Huwa tunashauri kama mwanamke ni mjamzito ajieleze, mjamzito hawezi kupatiwa matibabu ya aina hii, kwa sababu inaweza kumuathiri mtoto aliye tumboni," anaeleza.**

"Ni nzuri zaidi kuanza tiba na mgonjwa hupona kabisa, lakini ikiwa mgonjwa anachelewa, anakuja hatua ya tatu na nne, ni za juu mno. Tukimuanzishia tiba, tunamsaidia tu kukabili au kupunguza yale maumivu anayokuwa anayapata kwa wakati huo."

**SIRI YA MATUNDA**

Kwanini mgonjwa anashauriwa kutumia matunda? Dk. Nuru anaendelea: "Tiba zetu nyingi zinahitaji damu ya mgonjwa iwe vizuri, iwe ya kutosha, hivyo tunawashauri wale mbogamboga na matunda ya kutosha."

"Huwa tunashauri kama mwanamke ni mjamzito ajieleze, mjamzito hawezi kupatiwa matibabu ya aina hii, kwa sababu inaweza kumuathiri mtoto aliye tumboni," anaeleza.

Mtaalamu huyo wa tiba saratani ana maoni kwamba, ili kuisaidia jamii, ORCI imeamua kujikita katika utoaji elimu sahihi kwa jamii kupitia njia mbalimbali, ikiwamo kwenye vyombo vya habari, mitandao ya kijamii na televisheni zilizoko hospitalini hapo.

"Kwa njia hiyo tunaweza kufikia watu wengi zaidi, kila aina ya ugonjwa wa saratani tunaeleza na tunaeleza mpaka athari za tiba mionzi tunazotoa. Tunawaeleza ukweli hata athari ndogo ndogo zinazojitokeza wakati wa matibabu.

"Tunajikita zaidi katika elimu ya kinga, tunaelimisha jamii jinsi ya kuepukana na magonjwa haya, kinga ni bora kuliko tiba. Tunahimiza wafanye uchunguzi wa afya zao mara kwa mara, hatua hiyo itasaidia kugundulika mapema na kupata tiba mapema," anasisitiza.

AFYA

# Prof. Mkumbo: Dawasa wajibikeni kipindupindu kinachosambaa Dar

## Ofisi yake, Tamisemi, Jiji ziko nyuma



Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Dar es Salaam, Kate Kamba, akinywa maji katika kisima cha Kimbiji na Mpera, alipotembelea miradi ya maji inayoendeshwa na Dawasa. **PICHA ZOTE: FRANK MONYO.**




Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Profesa Kitila Mkumbo, akizungumza na wafanyakazi wa Dawasa (hawapo pichani).

**Na Frank Monyo**

NI siku chache tu, Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Profesa Kitila Mkumbo, aliiagiza Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Dar es Salaam (DAWASA), kuhakikisha inaingia vitani dhidi ya ugonjwa wa kipindupindu unatoweka, kwani ni aibu kwa wakazi wa jiji hilo.

"Jiji ambalo lina maskini wachache, chini ya asilimia tano. Jiji ambalo kipato chake ni kikubwa, ambalo serikali imewekeza sana katika miundombinu, lazima jambo hili dogo na la aibu la kipindupindu liishe," anasema Profesa Mkumbo.

Ni kauli yake alipozungumza na wafanyakazi wa Dawasa na Kamati ya Maendeleo ya Chama cha Mapinduzi (CCM), mkoa wa Dar es Salaam, walioongozwa na Mwenyekiti wa Mkoa, Kate Kamba.

Hiyo ilikuwa katika ziara ya kamati hiyo kutembelea miradi ya maji inayoendeshwa na Dawasa na kukagua maendeleo yake.

Profesa Mkumbo anasema, jijini Dar es Salaam kuna wadau watatu wakubwa kwenye suala la kushughulikia ugonjwa wa kipindupindu.

Anawataja kuwa ni Ofisi ya Rais (Tamisemi) kupitia Halmashauri ya Jiji na Manispaa zake, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, inayohusika na kuzuia, kudhibiti, pia kupambana na magonjwa.

**"Jiji ambalo lina maskini wachache, chini ya asilimia tano. Jiji ambalo kipato chake ni kikubwa, ambalo serikali imewekeza sana katika miundombinu, lazima jambo hili dogo na la aibu la kipindupindu liishe," anasema Profesa Mkumbo.**

Pia katika orodha hiyo anaitaja ofisi yake, Wizara ya Maji, anayoiita mdau muhimu, inaingia moja kwa moja kuwajibika, kwani kipindupindu kinasababishwa na ulaji na unywaji wa vitu vilivyoambukizwa vimelea vinavyosababisha ugonjwa.

### KULIKONI KIPINDUPINDU?

Profesa Mkumbo anasema, hivi karibuni Wizara ya Maji ilituma wataalamu wake kwenda kupima ubora wa maji katika maeneo nane jijini Dar es Salaam na majibu yakaja asilimia 99 ya maji wanayotumia, hayatoki kwenye mtandao wa Dawasa.

Anafafanua maana yake ni kwamba, wananchi wakiunganishiwa katika mtandao wa maji ya Dawasa, inatoa fursa ya kukidhibiti kipindupindu.

"Katika sampuli nane zilizopimwa, asilimia 99 katika maji hayo sio mtandao wa Dawasa. Watu wamejiunganishia wenyewe kwa hiyo watu hao wakiunganishwa na Dawasa itakuwa njia ya kudhitibi ugonjwa wa kipindupindu kwa asilimia 90," anasema Profesa Mkumbo.

Kutoka na hali hiyo, anatoa maagizo matatu kwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa Dawasa, Mhandisi Cyprian Luhemaje kujenga vituo vya kuchota maji ya Dawasa (vioski) katika maeneo ambayo yameathirika, hasa Vingunguti, lengo ni wananchi wapate mfumo rasmi wa serikali kupata huduma ya majisafi.



Ofisa Mtendaji Mkuu wa Dawasa, Mhandisi Cyprian Luhemeja.

Pili, anasema kuna haja ya Bodi ya Maji Bonde la Wami/Ruvu kwa kushirikiana na Dawasa zifanye ukaguzi na kusajili visima vyote jijini Dar es Salaam vinavyomilikiwa na watu binafsi.

"Bodi wameshaanza hii kazi... maana katika 'sampo' ya visima nane, visima saba vyote vya watu binafsi. Kwa maana hiyo, visima hivi lazima vikaguliwe na lazima visajiliwe, ili tuvijue na kufahamu hawa wananchi wanatumia maji ya aina gani," anasema Profesa Mkumbo.

Anaongeza kuwa, katika visima hivyo vinane vilivyofanyiwa uchunguzi, Dawasa inapaswa kwenda kuweka dawa ya kutibu maji, kwa kuwa jukumu la serikali ni kulinda uhai wa watu wake.

Pia, anasema ni lazima Dawasa iwe na utaratibu wa kujenga uhusiano mzuri na wananchi wote wanaotumia maji yasiyotoka katika vyanzo vya mamlaka hiyo kutoa elimu, vivyo hivyo watu wafahamu kumiliki kisima kwa kufuata kanuni na taratibu.

### KAULI YA DAWASA

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Dawasa, Mhandisi Cyprian Luhemeja, anasema wamepokea maelekezo ya Katibu Mkuu na kwamba jitihada za kuhakikisha wengi wanapata huduma ya majisafi kutoka Dawasa, zinaendelezwa.

Anafafanua kuwa, hivi sasa mikakati ya Dawasa ni kuhakikisha upatikanaji maji jijini Dar es Salaam unafikia asilimia 90 ifikapo Desemba mwaka huu, katika maeneo ambayo yana changamoto ya upatikanaji huduma ya maji safi na salama.

Anasema, katika mchakato huo wamedhamiria kuyafikia maeneo yasiyo na mtandao wa Dawasa, pia maeneo yaliyofikiwa na miundombinu, yakamilishiwe kazi ya kufikisha maji.

"Katika maeneo ambayo yana changamoto tumeandaa mpango maalumu wa kuwafikia wananchi kwa kutumia visima vinavyomilikiwa na halmashauri (visima vya vijiji), upo mpango wa kuhakikisha wananchi wanaunganishwa na mtandao huo kwa mkopo ili kuondokana na adha ya upatikanaji wa maji," anasema Mhandisi Luhemeja.

Anafafanua kuwa, sehemu kubwa ya Jiji la Dar es Salaam, makazi yake hayajapangika vizuri, hali inayofanya kazi ya kufikisha huduma hiyo ya maji kwa wakazi wa maeneo hayo kuwa na gharama kubwa zaidi.

### WAPEWA USHAURI

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi(CCM) Mkoa wa Dar es Salaam, Kate Kamba, anawataka wataalamu kutoka Dawasa, kutafuta mbinu mbadala za kuvuna maji ya mvua, ili kukabiliana na changamoto ya upatikanaji vyanzo vya maji.

"Tuna wahandisi wengi Dawasa, tujiandae kuja na mawazo ya jinsi ya kuokoa maji ya mvua yanayopotea baharini na kutuacha na shida ya maji," anasema Mama Kate.

Hata hivyo, anawapongeza Dawasa kwa kubana matumizi kutoka vyanzo vya fedha vya ndani na kuwekeza katika miradi ya maji mbalimbali, inayofanikisha kwa sehemu kubwa kuondokana na shida ya maji jijini.

"Niwashukuru kwa kujibana asilimia 35 ya mapato yenu na kutekeleza miradi, huku kutumia 'false account' kwa kujisimamia wenyewe na kutekeleza miradi kwa kiwango bora," anasema Mama Kate.

### BONDE LA WAMI/RUVU

Ofisa wa Maji Bonde la Wami/Ruvu, Simon Ngonyani, anaeleza kwamba, kutokana na agizo la serikali kufuta tozo ya visima vya maji kwa watumiaji binafsi na matumizi ya majumbani, wanawashauri watu wanaotaka kuchimba visima kufika katika ofisi zao, kwa ajili ya kupewa ushauri wa kitaalamu na waonyeshwe njia sahihi ya kuchimba.

**"Tuna wahandisi wengi Dawasa, tujiandae kuja na mawazo ya jinsi ya kuokoa maji ya mvua yanayopotea baharini na kutuacha na shida ya maji," anasema Mama Kate.**

"Sisi kama wataalamu, tunawashauri kwamba bado wafuate utaratibu, kwani kuchimba visima kiholela si jambo zuri kwa afya zao. Hata kama wakichimba hawalipi, lakini hii ya kutolipa haiwaondolei kwamba ni salama.

"Waje waombe vibali, ili tuweze kufahamu nani anachimba wapi, kwa sababu vinginevyo tutachimba hadi kwenye mashimo ya choo na matokeo yake ni hatari kwa afya zao na kusababisha magonjwa ya mlipuko kama kipindupindu," anasema Ngonyani.

Anasema, hadi sasa kuna watu wanaochimba visima kiholela, ambayo matokeo yake ni katika kipindi cha mvua, wanajikuta hatarini kupata magojwa ya mlipuko, kwani uchafu unaosombwa na maji ya mvua unaweza kupelekwa hadi kwenye visima vyao ambavyo huenda havijachimbwa kitaalamu.

# Wenye wazazi waliotengana watoto wao wanenepa ovyo

**Na Mwandishi Wetu**

DUNIANI kuna mambo. Watafiti wamejitosa kufanya kazi wakisema watoto ambao wazazi wao wametengana, kasi yao ni ya kunenepa zaidi, kuliko ambao wana wazazi wao wanaoishi pamoja, wasomi wamebaini kupitia utafiti.

Kulingana na matokeo ya utafiti yaliko katika Jarida la Idadi ya Watu, ni kwamba wamegundua ukuaji huo umejidhihirisha kwamba wanaoishi kwa mzazi mmoja wako vizuri zaidi.

Watafiti kutoka Shule ya Uchumi na Sayansi ya Siasa ya London, walifanya upekuzi huo wa kisomi kutoka kwa watoto 7,574, kati ya mwaka 2000 na 2002, kwamba watoto hao baada ya wazazi kutengana, wanakuwa na afya nzuri maradufu.

Kwanini hivyo? Watafti wamekuwa na ufafanuzi kadhaa wa kitaalamu wakiainisha katika vipengele vifuatavyo:

Watoto hao hawatengewi fedha nyingi kwa ajili ya lishe ya matunda na mboga; huku wazazi wenyewe wanakuwa na muda wa ziada katika shughuli za kikazi na wanabakiwa na muda mfupi kuandaa lishe bora kwa watoto wao.

Vivyo hivyo, inaelezwa kwamba wazi wanakuwa na muda mfupi kushughulikia mambo yanayohusika na mlo sahihi wa watoto waona wakati huo huo, hawana pesa na fursa za kuwawezesha watoto kujihusisha na mambo kama michezo ya ziada ambayo ni muhimu kiafya na kisaikolojia.

Mwisho, inaelezwa kwamba wazazi waliotengana, muda mwingi wana hasira za kutokana na kinachowakabili, inawafanya wote wakiwa na watoto wao wanaokula vitu vyenye sukari na mafuta mengi.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, ni utafiti uliowahusu watoto wenye umri kuanzia miezi tisa; miaka mitatu; miaka saba; na miaka 11 hadi 14.



Baadhi ya lishe zinazotumiwa kubadili afya ya watoto. **PICHA: MTANDAO.**

Mtazamo wa vigezo husika ulikuwa katika mitazamo ya uzito, urefu, umri, jinsia na vitambi.

Matokeo ya jumla, watoto hao waliofuatiliwa katika kipindi cha miezi 24 (miaka miwili) na wakabainika kwamba ambao wazazi wao walitengana walinenepa zaidi.

Walipofanyiwa tathmini ya mwaka mmoja (miezi 12) baadaye, walionekana kwa maana ya ilipotimu miezi 36, walikutwa na vitambi na uzito maradufu, kuwashinda wale wenye wazazi katika ndoa.

Sasa kuna maoni kwamba, kuna haja ya kuleta mabadiliko, kudhibiti kunenepa ovyo kwa watoto hao, hali ambayo ni hatari na afya zao.

"Kuingilia mapema (unenepaji wa watoto) kunaweza kusaidia kuzuia. Jambo jema ni kuzuia, au angalau kupunguza, mwelekeo unaochangia baadhi ya watoto kuwa na kitambi kisicho cha kiafya," unasema utafiti.

***Hii ni kwa mujibu wa jarida la Demografia.***

AFYA

BWANA CHANJO MANYARA...

# Daktari Bingwa wa Manyar mazito ya vichwa vikubwa

- Wanakijiji wakiri wanaishia kushangaa
- Jafo apagawa, aagiza mazito Tamisemi
- Mama alivyotelekezewa watoto wawili

**Na Jaliwason Jasson, BABATI**

WAZAZI wanaojiandaa kupata watoto, mara zote wanatakiwa kuwa makini kwa kuzingatia kanuni za afya katika kipindi hicho, lengo ni kijiwekea mazingira wezeshi yanayomjengea afya njema mtoto aliye tumboni, vivyo hivyo mama huyo mjamzito.

Ni tahadhari yenye maana kubwa kiafya, hapo yakitajwa maradhi mengi kwa mtoto ajaye, ikiwamo yanayoitwa 'mgongo wazi' na 'kichwa kikubwa,' lengo ni kudhibiti asije akaonekana 'hatakiwi.'

Pia, inafahamika kwamba katika saikolojia na mtazamo wa kijamii, kwamba kila mwanadamu anapenda afikie hatua ya kujitegemea, hata kuanzisha familia yenye wazazi wawili na watoto.

Katika mchakato wa kulifanikisha hilo, baadhi ya familia zikitawaliwa na mila na desturi, zinajikuta katika mtazamo wa kujihisi 'zimelaaniwa' kwa kupata watoto wenye magonjwa kama ya mgongo wazi na vichwa vikubwa.

Na maradhi ambayo ama wazazi au walezi wanajikuta katika mtihani mgumu wa kukabili. Wapo wazazi na walezi wanaovumilia changamoto hiyo na wengine wanakata tamaa. Hawaoni haja ya kuendelea kutetea vizazi vyao. Je, tatizo hilo ni nini?



Wananchi wenye ulemavu wa mgongo wazi na vichwa vikubwa, wakiandamana katika maadhimisho ya siku yao, mjini Dodoma, mwaka jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH.**

**Daktari bingwa**

Ezekiel Lukenza, ni daktari bingwa wa magonjwa ya mgongo wazi na vichwa vikubwa kutoka Hospitali ya Rufani Mkoa wa Manyara, anasema tatizo la mgongo wazi na vichwa vikubwa linaonekana mtoto anapozaliwa.

Analitaja kuwa tatizo la pili, likiongozwa na magonjwa yanayohusiana na moyo, kama vile matundu wazi ya moyo au mirija.

Dk. Lukenza anasema, sehemu inayokuwa wazi ni eneo karibu na kiuno panavimba na chini mawasiliano huwa yanakatika, hali inayomfanya mtoto ashindwe kutembea na hatimaye kichwa chake kinavimba.

Anataja sababu ya kichwa kuvimba, ni kwamba maji yanashindwa kutoka na kurudi kichwani, hali inayoathiri kichwa cha mtoto.

Dk. Lukenza anafafanua sababu nyingine ni pamoja na mtu anavyoumbwa au urithi wa asili, ingawaje katika hilo ana mtazamo wa 'kuchechemea' kupatia kauli: "siyo moja kwa moja, ila ninahusishwa kuwa ni miongoni mwa sababu za ugonjwa huo."

> **Anatumia fursa hiyo kuzitaja jitihada za serikali katika kupambana na ugonjwa huo, kwamba inasisitiza wajawazito kula madini ya 'folic acid' na imetunga sheria ya kuwabana wazalishaji bidhaa hizo, ili kukabili ongezeko la watoto wanaozaliwa na tatizo hilo.**

Kukosa madini ya 'folic acid' vinakuwa virutubisho, anavyosema wanawake wanapojiandaa kubeba mimba, wanatakiwa kutumia vyakula kama mayai, maini, maembe, parachichi na mboga za majani,

Hivyo ni muhimu ili viwasaidie ndani ya siku 30 za mwanzo wa mimba, virutubisho hivyo ndio vinahitajika mno, kwa maana uti wa mgongo ndio unatengenezwa.

Magonjwa ya kisukari yanaelezwa ni hatari kwa wajawazito, kwani inakaribisha uwezekano wa kupata mtoto mwenye mgongo wazi.

Hivyo, ushauri wake ni kwamba katika kipindi cha ujauzito, kinamama wanashauriwa kujitahidi kuidhibiti kiwango cha sukari mwilini kisiwe cha juu, kwani hata baadhi ya dawa ya kifafa, zinahusishwa na sukari.

Katika ufafanuzi wake, Dk. Lukenza anasema kadri uti wa mgongo unavyokuwa mkubwa, ndivyo kichwa cha mtoto kinakuwa kikubwa na kujaa maji.

**Uhalisi ulikosimama**

Mtaalamu huyo anasema, Mkoa wa Manyara una bahati kwamba wagonjwa namna hiyo ni wachache kulinganisha na kwingineko nchini na athari za mgongo wazi kwa asilimia kubwa, hurudi kwenye hali yao ya kawaida.

Pamoja na uhalisia huo, Dk. Lukenza anasema jamii hupata kero ya kukwama kuzalisha, kunyanyapaliwa na jamii, hata wengine kuwahusisha na uchawi.

Anasema, wagonjwa katika mkoa wa Manyara, athari zao si mbaya sana, tofauti na jamii nyingine, mtoto anakuwa tegemezi zaidi, kiasi cha kuwa rahisi kushambuliwa na magonjwa kama maambukizi ya mkojo (UTI) na homa za kila mara.

Daktari bingwa huyo anataja changamoto walio nayo ni uhaba wa wataalamu, hivyo anashauri serikali kuwaanda wataalamu wengi zaidi, ingawaje anakiri kuwapo gharama kubwa.

Kupitia taarifa aliyoitoa Novemba, 2016, Kaimu Mkurugenzi wa Taasisi ya Mifupa na Mishipa ya Fahamu Muhimbili (MOI), Dk. Othman Kiloloma, anahusisha mgongo wazi na mfumo mkuu wa mshipa wa fahamu uitwao "central never system."

Anasema, kati ya watoto 4,000 wanaozaliwa na tatizo hilo kila mwaka, ni 600 pekee wanaofikishwa hospitalini na waliobaki 3,400 wanapotelea njiani.

Dk. Kiloloma anasema, gharama ya kuweka kifaa cha kusaidia kunyonya maji kichwani ni kati ya Sh. 160,000 hadi shilingi milioni moja, kulingana na ubora wake, wakati mgonjwa anapohitaji.

Anatumia fursa hiyo kuzitaja jitihada za serikali katika kupambana na ugonjwa huo, kwamba inasisitiza wajawazito kula madini ya 'folic acid' na imetunga sheria ya kuwabana wazalishaji bidhaa hizo, ili kukabili ongezeko la watoto wanaozaliwa na tatizo hilo.

Mtaalamu huyo anasema, kila

AFYA

# ra asimulia
# , mgongo

wiki wanapokea watoto wenye ugonjwa huo 10 na kwa mwaka ni zaidi ya 500, wanaotibiwa.

Kwa mujibu wa Shirika la Utangazaji la Uingereza (BBC), nchini bado kuna vituo vichache vya kuhudumia maradhi hayo nje ya Dar es Salaam, vikiwamo Lindi, Mtwara na Mwanza.

Mwaka huu, Tanzania imo katika nchi zilizoadhimisha Siku ya Mgongo Wazi Duniani mwaka huu, huku na Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha Wazazi wenye ulemavu wa migongo wazi na vichwa vikubwa nchini, Abdlkarim Bayakub, alibainisha mjini Dodoma, kuwa watoto wenye tatizo hilo nchi nzima wako 10,000.

Akiwasilisha taarifa yake kwa aliyekuwa mgeni rasmi Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, mwenyekiti huyo alitaja changamoto kubwa kwao ni gharama za kupata matibabu, ikiwamo kuziwa mrija mmoja wa Sh. 200,000, ambayo ni mtihani kwa wenye kipato kidogo.



**Jafo apagawa**

Katika nasaha zake, Waziri Jafo, alishindwa kuvumilia kukaa kwenye jukwaa katika maadhimisho hayo, alipoziagiza halmashauri zote nchini kutenga shilingi milioni sita katika mipango yao ya bajeti ya mwaka wa fedha mpya unaoanza, kwa ajili ya kuhudumia matatizo hayo.

Pia, waziri alitumia fursa hiyo kuzitaka halmashauri nchini kutunga sheria ndogo za kuwabana wenye viwanda kwenye maeneo yao, kuweka virutubisho vya lishe vinavyozuia ugonjwa huo unaoshika kasi nchini.

> “Hata kama baba yao amenikimbia na kutuacha, tunahangaikia matibabu yao, labda naomba Mungu anisaidie nipate wasamaria wema, ili watoto hawa wapate matibabu,” anasema mama huyo.



Mkazi wa Manyara, akiwa na wanawe wanaosumbuliwa na tatizo la mgongo wazi. **PICHA: JALIWASSON JASSON.**

**Mkasa wa mzazi**

Mkazi wa Kijiji cha Hallaa, katika Halmashauri ya Mji wa Babati, Anastazia Abogasti (38), ni mama mwenye watoto wanane; mabinti watano na wavulana watatu.

Anasema, watoto hao walizaliwa wazima, ila walipofikisha umri wa miezi sita, walibainika kuwa na ugonjwa wa mgongo wazi na vichwa vikubwa.

Mama huyo anasema, licha ya kuendelea kuhangaika kusaka matibabu yao, hakujua chanzo cha ugonjwa wa wanawe, akabaki njia panda.

Wakati akiwa bado katika mshangao, mumewe alimkimbia na watoto wanne wa kike akienda kuoa mwanamke mwingine, baada ya kuhisi hatoweza kuwatunza watoto hao waliopatwa na ugonjwa huo.

Anastazia anaeleza msimamo wake na wanawe akitamka: “Mimi ninawapenda watoto wangu hawa sana na sijawahi kujuta kuwazaa hawa watoto.

“Hata kama baba yao amenikimbia na kutuacha, tunahangaikia matibabu yao, labda naomba Mungu anisaidie nipate wasamaria wema, ili watoto hawa wapate matibabu,” anasema mama huyo.

Anaiambia Nipashe kuwa, ameshawapeleka katika Hospitali ya Rufani ya Hydom, Manayara walikofanyiwa upasuaji ila wakapewa rufani ya kwenda Hospitali ya Rufani KCMC, mjini Moshi, lakini amekosa fedha za kwenda huko.

Mama huyo hivi sasa anaeleza ombi kwa wanajamii na taasisi mbalimbali na wadau wenye uwezo wamsaidie watoto wake.

Mama huyo anaeleza hali ya watoto hao inauma kuwa wanachoka wakitembea umbali kidogo na mara nyingine wanashindwa kukaa, kwani wana mifupa duni kwenye miili, pia wanachoka haraka au wakati mwingine tumbo zao zinajaa gesi.

“Watoto hawa waliposhindwa kukaa, nilikuwa nawaweka kwenye beseni na kuwazungushia nguo. Huyu wa kwanza aliposhindwa kabisa, nilienda kituo cha afya Gallapo, ili nipate ushauri, ndipo waliniambia niende Hospitali ya Mrara.

“Mrara nao wakanisukuma Hospitali ya Dareda na Dareda walipima kwenye ‘x-ray’ na kuwachunguza ndipo niliambiwa niende KCMC,”anasimulia mchakato ulivyo.

Pia, alieleza Nipashe alipotakiwa kufafanua kuwa, alianza kuhudhuria kliniki alipokuwa na ujauzito wa miezi sita kwa watoto wake wote.

**Mashuhuda**

Mkazi wa eneo la Halla, Simon Kimoro, anakiri kuwafahamu wa watoto hao muda mrefu na baadhi ya watu wamekuwa wakimkatisha tamaa kwamba ‘watoto hao hawatapona.’

Kimoro anasema, hata kijiji chao anachoishi kilimchangia mama wa watoto hao, kiasi cha shilingi 400,000 za kwenda kutibiwa hospitalini Hydom, ingawaje haikutosha kukidhi mahitaji hayo ya tiba.

Pia, Merania Jacob, ambaye ni mkazi wa Gallapo, anasema hajui chanzo cha ugonjwa huo, hivyo anashauri wataalamu wa afya watenge muda kuwafikia vijijini kuwapa elimu wazazi kuhusu namna ya kujikinga na ugonjwa huo, ambao ni mzigo mzito unaowahangaisha kwa kukosa fedha za kuwatibu watoto, jambo ambalo ni hatari kwa maisha ya wahusika.

Dativa Sulle, mkazi wa Babati, anaungana na mtangulizi wake kwamba hufahamu ugonjwa huo, ila zaidi anausikia kwenye vyombo vya habari, naye anadia haja ya jamii kupewa elimu mapema kuhusu namna ya kujikinga na maradhi hayo, ili watu wasiangukie fikra kuwa ni ‘laana’ au ‘wamerogwa’.

Thomas Daniel, katika maoni yake yaliyo katika kuali ya kubahatisha, anasema haelewi vyema chanzo chake, akidhani ni magonjwa ya kurithi kutoka kwa ndugu au huenda wanapungukiwa na aina za viini lishwe vya vitamini. Hivyo, Daniel anawaomba wataalamu wa afya wapewe nafasi ya kuifundisha jamii unatokeaje, siri ya athari hizo, kwani jamii isipoelimishwa, ugonjwa huu utazidi kukua na kuenea, kwani wapo wazazi watakaowaficha watoto wa namna hiyo kwa kuogopa jamii itawachukulia tafsiri mbaya au watalazimika kuwadhuru watoto hao.



Baadhi ya watoto wenye vichwa vikubwa na mgongo wazi .**PICHA: MTANDAO.**

AFYA



Picha mbili zinazoonyesha miguu ya mtoto kabla na baada ya kutibiwa, akapona. **PICHA ZOTE: MAKTABA.**

# Mabingwa CCBRT wawaponyesha bure watoto wagonjwa wa miguu kifundo

- Kila mwaka wanawafikia wahitaji 400
- Wanakumbushwa kliniki kupitia 'sms'
- Ugonjwa usiochagua, wamfikia yeyote

**Na Yasmine Protace**

NYAYO ya kifundo mguuni ni aina ya ulemavu unaotokana na matatizo ya mifupa. Ulemavu huo huwa ni wa kuzaliwa na unaweza kumpata mtoto yeyote duniani.

Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya CCBRT, Brenda Msangi, anasema takwimu zinaonyesha watoto zaidi ya 2000 nchini Tanzania huzaliwa na ugonjwa wa miguu kifundo au nyayo zilizopinda.

Brenda anayasema hayo na kuongeza kuwa, kila mwaka ifikapo Juni 3, ni Siku ya Miguu ya Kifundo Duniani na mwaka huu yamefanyika mkoani Dodoma.

"Miguu kifundo au nyayo zilizopinda ni aina ya ulemavu unaotokana na matatizo ya mifupa," anasema na kuongeza kuwa ulemavu wa aina hiyo huwa ni wa kuzaliwa nao na unaweza kumpata mtoto yeyote katika maisha yake duniani.

Brenda anasema, lengo la CCBRT ni kuhakikisha wanawafikia wagonjwa kwa wakati muafaka na ni muhimu wazazi wasipowawaisha watoto wao kupata matibabu mapema, wanawasababishia kupata ulemavu.

Mkurugezi huyo wa CCBRT, anasema wanatoa bure matibabu, ikiwamo urekebishaji miguu ya wahusika.



Mtoto akihudumiwa katika kambi za vijijini, iliyoko Shirati, Mara, Desemba mwaka jana.



Hivi ndivyo lilivyo tatizo hili la miguu ya mtoto mchanga.

Kwa mujibu wa mtendaji huyo mkuu wa hospitali, wazazi wengi walikuwa hawajui kama matibabu hayo yanatolewa bure CCBRT, ambako idadi ya watoto wanaofuata matibabu imekuwa ikiongezeka maradufu.

Anasema, wamekuwa wakiwatumia ujumbe wazazi kwa njia ya simu wakiwakumbusha kuwaleta watoto kliniki kuendelea na matibabu, ambayo wanakuwa wameandikiwa na kurudi kuendelea.

Brenda anasema, katika kuhakikisha ubora wa kile wanachokitoa, wamekuwa wakiwaongezea ujuzi wataalamu wao, kila mwaka CCBRT ikitoa mafunzo maalum kwa wataalamu wao.

> **"Mtoto hata akizaliwa leo akagundulika na tatizo, anatibiwa. Matibabu yake ni rahisi na akiwa ana miaka miwili anafanyiwa upasuaji," anasema.**

Kuhusu chanzo cha ugonjwa huo, Brenda anasema hakuna sababu sahihi inayohusishwa kitaalamu na watoto kuzaliwa na miguu ya aina hiyo.

Anasema, maoni ya wataalamu ni kwamba kuna uwezekano mkubwa wa mtoto kuzaliwa hivyo, iwapo kuna mmmoja akikuwa na ulemavu huo.

Pia, takwimu wanazirejesha katika ubashiri wa kitaalamu kuwa katika kila vizazi hai 1000, kuna uwezekano wa kuzaliwa mtoto mmoja au wawili kwenye nyayo zilizopinda.

Brenda anafafanua: "Takwimu za Tanzania zinaonyesha kuwa watoto 2,500 hadi 2,800 wanazaliwa na hali hiyo kila mwaka."

**Daktari bingwa**

Dk. Prosper Aute, ni bingwa wa masuala ya mifupa wa CCBRT, anasema kuwa wapo watoto ambao wanaopata ugonjwa huo kwa kurithi, lakini wanawatibu na kupona.

"Mtoto hata akizaliwa leo akagundulika na tatizo, anatibiwa. Matibabu yake ni rahisi na akiwa ana miaka miwili anafanyiwa upasuaji," anasema.

Anaongeza kuwa, matibabu hayo yanatolewa CCBRT jijini Dar es Salaam na kituo chake kilichoko mjini Moshi, eneo la Pasua.

Kwa mujibu wa Daktari Aute, iwapo matibabu hayo yangetolewa kwa gharama, ingekuwa katika tozo la wastani isiyopungua shilingi milioni moja.

Dk. Aute anasema, kutokana na matibabu kutolewa bure, jamii zenye watoto waliozaliwa na ugonjwa huo, inapaswa kuwapeleka CCBRT wakapatiwe matibabu ambayo ni ya muda mfupi na wanarudi katika maumbile ya kawaida ya mwanadamu.

Kwa mujibu wa Dk. Prosper, kila mwaka wanawatibu watoto 400 wenye ugonjwa huo.

**Mzazi aeleza**

Johari John, ni mkazi wa Kiwalani, jijini Dar es Salaam, anayesema alijifungua mtoto akiwa na miguu kifundo na mwanawe aligunduliwa kuwa na tatizo hilo, akiwa na umri wa siku 20.

Anasema baada ya kugundulika, alipelekwa CCBRT jijini Dar es Salaam na akapatiwa matibabu, sasa anaendelea vizuri.

Johari ana shauri kwamba, wazazi wenye watoto walio na miguu kifundo, wawapeleke CCBRT ili wakapatiwe matibabu ambayo yanatolewa bure.

Mbali na huduma hiyo, CCRT ni kituo kinachotoa tiba mahsusi katika maeneo ya kiafya yanayosumbua jamii, ikiwamo maradhi ya fistula kwa kinamama, ambayo nayo yanatolewa bure, kama ilivyo mguu kifundo.

Pia, hospitali hiyo ni kituo maarufu cha kupambana na ulemavu wa aina nyinginezo na maradhi ya kifua kikuu nchini.





## Wateja wanufaika Wiki ya Utumishi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MAMLAKA ya Mawasiliano nchini, (TCRA) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, imeadhimisha Wiki ya Utumishi wa Umma kwa kusajili kadi za simu kwa kutumia alama za vidole kwa wateja mbalimbali wakiwamo wanachuo.

TRCA ilishirikiana na kampuni mbalimbali ya simu pamoja na mamlaka zingine za kiserikali kukamilisha kazi hiyo, wakati wa maadhimisho hayo yalifanyika juzi katika Chuo cha Sayansi na Teknolojia cha Mbeya (Must).

Wanafunzi wa chuo hicho na majirani wa Must walisajiliwa kadi zao na kupatiwa elimu kuhusu faida za utaratibu huo mpya.

Akizungumza wakati wa usajili huo Mkuu wa TCRA Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Mhandisi Asajile John, alisema kazi hiyo pia iliwashirikisha Jeshi la Polisi, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (Nida) pamoja na Idara ya Uhamiaji.

Alisema mbali na kuwasajilia wanafunzi wa chuo hicho simu zao, pia jamii na wananchi wanaoishi maeneo ya kukizunguka chuo hicho walinufaika na elimu na kusajiliwa.

Mhandisi John alisema waliamua kuadhimisha Wiki ya Utumishi wa Umma kwa kuleta pamoja kampuni zote za simu, taasisi za umma zinazohusika katika mchakato wa usajili ili kuwarahisishia wateja badala ya kila mmoja kufuata huduma hiyo kwenye kampuni husika.

"Tumeona kuna usumbufu kwa wateja wanaotumia laini zaidi ya moja kwenda kujisajili kwa mtoa huduma mmoja hadi mwingine ni changamoto. Ndiyo maana sasa tumeamua kuzileta pamoja kampuni zote hapa, ili mteja asipate usumbufu, aweze kumaliza usajili hapa hapa kwa wakati mmoja," alisema.

Kwa upande wake Mkuu wa Kitengo cha Uhalifu wa Mtandaoni kutoka Jeshi la Polisi Mkoa wa Mbeya, Joram Magova, aliwatahadharisha watumiaji wa simu za mkononi kufuata sheria za mtandao ili wasikabiliwe na mkono wa sheria.

Alitolea mfano wa uhalifu wa mtandao ni pamoja na utapeli kwa njia ya mtandao, lugha ya matusi na udhalilishaji, uchochezi, kusambaza picha na video za ngono pamoja na picha zinazowadhalilisha watoto.

"Kwa upande wetu Jeshi la Polisi tunaendelea kutoa elimu ni kitu gani unatakiwa ukifanye na kipi ambacho hautakiwa ukifanye kwa sababu unaweza kujikuta umekiuka sheria ya mtandao. Lakini pia tunasisitiza kwa wananchi kuepuka kuokota na kununua mitaani vifaa vya kielektroniki ili wasiingie kwenye hatia," alionya Mgova.

Ofisa Usajili wa Mamlaka ya Vitambulisho (Nida) Mkoa wa Mbeya Lovia Ntalima, alisema kazi hiyo inawahusu wanafunzi wa chuo cha Must, na wananchi ambao hawakuanza mchakato wa usajili kwenye ofisi za serikali za mitaa na mamlaka ya Nida. Alisema Nida inaendelea kutoa vitambulisho vya taifa kwa awamu ili kuwawezesha wananchi kusajili kadi zao na kwamba kwa wale ambao bado hawajavipata waendelee kusubiri.

# Kigogo aliyekuwa na kesi adaiwa kujinyonga

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MHANDISI wa Majengo wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya, Aswile Msika (37), amekutwa amekufa, ikidaiwa kuwa amejinyonga kwa kutumia suruali yake.

Tukio hilo lililotokea katika eneo la Nyatura lililoko kata ya Mbugani wilayani humo, kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi Ulrich Matei. Alisema tukio hilo liltokea juzi wakati mtumishi huyo wa umma aliyekuwa anakabiliwa na mashtaka ya rushwa akiwa amejitundika.

Alisema chanzo cha tukio hilo hakijafahamika na kinaendelea kuchunguzwa na polisi, lakini awali marehemu alikuwa na kesi ya kuomba na kupokea rushwa shauri ambalo lilikuwa linaendelea katika Mahakama ya Wilaya ya Chunya.

"Alikuwa na kesi ya kuomba na kupokea rushwa ya Sh. 1,000,000 kutoka kwa mmoja wa makandarasi wanaofanya kazi wilayani humo na kesi hiyo ilikuwa inaendelea mahakamani," alisema Kamanda Matei.

Alitoa rai kwa wananchi kuepuka kufanya matukio kama hayo na kuwataka watu wanaosumbuliwa na msongo wa mawazo kuwashirikisha ndugu zao ili wasaidiwe badala ya kuchukua maamuzi magumu.

Alisema tukio kama hilo ni la pili kutokea katika mkoa huo ndani ya kipindi kifupi ambapo alisema mtu mwingine alijinyonga wilayani Mbarali, huku chanzo kikidaiwa kuwa ni wivu wa mapenzi. Alisema pamoja na kwamba inadaiwa kuwa chanzo ni migogoro ya mapenzi, lakini jeshi hilo linaendelea kuchunguza ili kubaini chanzo halisi cha kifo hicho.

Aliwaomba viongozi wa vijiji na mitaa kusaidia kutoa elimu kwa jamii ili iepuke kufanya matukio hayo ambayo alisema yanaumiza na kuchafua taswira ya mkoa huo.



Naibu Waziri wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhandisi Hamad Masauni (wa pili kushoto), akiwa na wataalamu kutoka Kikosi cha Uzalishaji cha Jeshi la Polisi na Wasimamizi wa Mradi, kutembelea eneo la Kunduchi, jijini Dar es Salaam, ambako Mradi wa Nyumba 330 za makazi ya polisi zinazoonekana pichani zikiwa zimeshakamilika. **PICHA: WMN**

# Uwanja wa Ndege Songwe kupanuliwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

NAIBU Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Atashasta Nditiye, amesema serikali inatarajia kupanua Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe (Sia), ili uhudumie ndege kubwa za mizigo na abiria wakati wote.

Uwanja huo utapanuliwa kutoka kilomita mbili zinazotumika sasa hadi kufikia kilomita 3.3, hatua itakayofanikisha ndege kubwa kutua katika uwanja huo.

Aliyasema hayo juzi jijini Mbeya wakati wa kongamano la kuhamasisha uwekezaji katika kilimo cha mboga na matunda lililoandaliwa na Kituo cha Uwekezaji (TIC), Taasisi ya Kuendeleza Kilimo Ukanda wa Kusini mwa Tanzania (Sagcot) na Shirikisho la Wakulima wa Mboga na Matunda (Taha).

Alisema lengo la serikali ni kuwezesha ndege za mizigo kutua na kupaa kwa urahisi na kuwarahisishia wananchi kusafirisha bidhaa zao kwenda kwenye masoko yakiwamo ya matunda na mboga.


Aidha, serikali inakusudia kuukarabati uwanja huo kwa kuweka taa ili kuwezesha ndege kutua na kupaa kwa wakati wote. "Muda si mrefu tutakuwa tumempata mkandarasi wa kuupanua na kuuongeza uwanja wetu, hii itasaidia ndege kubwa za mizigo kutua na kurahisisha usafirishaji wa mazao ya wawekezaji wetu, hivyo wakulima tunawashauri mwendelee kuzalisha," alisema Nditiye.

Kwa upande wake Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Stella Manyanya, aliwataka wawekezaji kuendelea kujitokeza kuwekeza katika viwanda vya kuzalisha bidhaa mbalimbali. Alisema itatafuta masoko kwenye maeneo mbalimbali ndani na nje ya Tanzania.

Alisema serikali imejipambanua kwa kuimarisha uchumi wa viwanda kwa kuhamasisha ujenzi wa viwanda vya kuchakata mazao mbalimbali ili kuepuka kuuza mazao ghafi ambayo tija yake mara nyingi inakuwa ni ndogo.

Alisema Wizara ya Viwanda kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Fedha imejipanga kuhakikisha wananchi wananufaika na kile wanachozalisha kwa kuuza bidhaa zao kwa bei nzuri.

"Wawekezaji tunawaomba tuwasiliane kwa lolote linalotokea, chukueni namba za mawaziri, ili kuwasiliana nao haraka kutatua changamoto zinazowakabili kwenye uwekezaji wenu naahidi kuzishughulikia kwa haraka," alisema Manyanya.





# Wasiosikia waomba vituo mawasiliano

Na Peter Mkwavila, KONDOA

WATU wenye ulemavu wasiosikia (viziwi) wilayani Kondoa, wameiomba serikali kuwawekea vituo vitakavyotoa elimu ya lugha ya mawasiliano kwa ajili ya vyombo vinavyohudumia jamii, vikiwamo mahakama, magereza, hospitali na polisi.

Ombi hilo lilitolewa na Mratibu wa Taasisi isiyo ya Kiserikali ya Mpango Elimu kwa Viziwi Dodoma (Mevido), Ally Mailache, alipokuwa akisoma risala kwa washiriki wa kongamano la lugha ya alama na kutoa uamuzi kuwapo kwa mfumo na uboreshaji wa mawasiliano lililofanyika Kondoa.

Katika kongamano hilo ambalo limepata ufadhili kutoka Taasisi ya The Foundation for Civil Society na kushirikisha wadau mbalimbali wakiwamo watoa uamuzi, mratibu huyo alisema kuwapo kwa vituo hivyo kutawawezesha watu wenye ulemavu wa kutosikia kupata huduma za kimsingi kutokana na elimu itakayotolewa kwa walengwa.

"Watu wenye ulemavu wa kutosikia wanakabiliana na changamoto kubwa hususani pale wanapohitaji kupatiwa huduma kwenye maeneo mbalimbali yakiwamo mahakama, polisi, magereza na hospitali hata kwenye upande wa elimu. Hii inatokana na kukosa wataalamu wa lugha ya mawasiliano," alisema.

Alisema taasisi hizo zenye kutoa uamuzi zimekuwa zikishindwa kuwasikiliza watu wenye ulemavu wa kutosikia kutokana na mawasiliano kuwa magumu, hatua ambayo imekuwa ikisababisha kukosekana kwa haki kama ilivyo kwa watu wengine wasiokuwa na ulemavu kama huo.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Kondoa, Robert Sungura, alisema kumekuwapo na changamoto kubwa ya kuwasaidia watu wenye ulemavu wa kutosikia kutokana na watoa huduma kwenye vyombo vya serikali kutoifahamu hiyo lugha ya mawasiliano.

Alisema kutokana na changamoto hiyo, watu wasiosikia wamejikuta wakitengwa na kubaguliwa na kukosa haki zao za msingi kwenye maeneo mbalimbali kama vile shuleni, hospitalini na kwenye vyombo vya sheria.

Mkurugenzi huyo alishauri vyombo vinavyotoa huduma mbalimbali kwa wanajamii, watendaji wake ni muhimu wakajifunza lugha ya alama ili kuwasiliana na watu wenye ulemavu wasiosikia katika utoaji wa huduma kwenye maeneo yao ya kazi.

# Jafo akwazwa mikoa kutopeleka watendaji

Na Augusta Njoji, DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, ameionya mikoa ya Dodoma, Lindi na Njombe kwa kushindwa kupeleka watendaji kuhudhuria semina ya kuandika miradi ya kimkakati.

Onyo hilo alilitoa juzi wakati akifungua semina ya siku mbili iliyoshirikisha Mamlaka za Serikali za Mitaa Tanzania Bara na Sekretarieti za Mikoa katika Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo.

Jafo alisema semina hiyo ni muhimu kwao kwa ajili ya kuwajengea uwezo utakaowawezesha kuibua miradi mbalimbali, lakini ameshangaa mikoa hiyo kutopeleka watendaji.

"Hapa hatuna wawakilishi wa Dodoma, Njombe na Lindi, wakati Dodoma mradi mkakati walioupata ni Kondoa peke yake. Hakuna Bahi, Chamwino wala Jiji. Njombe nao hakuna mradi mkakati walioupata cha kushangaza kwenye semina hii hawapo," alisema.

Alisema Lindi wana mradi mkakati katika halmashauri za Liwale na Ruangwa, lakini bado hawajahudhuria semina hiyo na Mtwara wana mradi katika halmashauri moja, lakini Nanyumbu, Masasi, Newala, Tandahimba na Nanyamba hakuna mradi wowote walioupata lakini pia hawajahudhuria.

"Hii Nanyamba ni halmashauri ya mwisho katika ukusanyaji wa mapato, nawaagiza wahakikishe awamu ya pili ya semina hiyo wanakuwapo," alisema.

Jafo alisema mpaka sasa Sh. bilioni 268.37 zimeshatolewa na serikali kwa ajili ya kugharamia miradi 38 na hapo kuna halmashauri hazijaguswa na miradi hiyo kutokana na maandiko yao kutokuwa na sifa za kupata fedha na hali yao ya uchumi bado iko mbaya.

"Leo hii unapoona halmashauri zimepewa nafasi hiyo, lakini bado zimelala kuanzia wilayani hadi mkoani, hapo kuna matatizo," alisema Waziri Jafo. Alibainisha kuwa ni lazima kubadili mbinu za ukusanyaji wa mapato kwa kuwa serikali lengo lake kubwa ni kuhakikisha inaondoa mzigo kwa watu wanyonge na ili hizo kodi na tozo zenye kero ziondoke ni lazima halmashauri ipate mapato kwa njia mbadala.

"Jiji la Dodoma hawapo hapa. Sijui ni kiburi cha kukusanya mapato mengi ndiyo maana hawataki kuja hapa na fedha hizo ujue ni fedha za kwetu tumeandikia miradi sisi ya TSP wala hawajaandika yao. Nilitamani waje hapa wajifunze. Leo hii Dodoma mpaka mwezi huu wameshakusanya Sh. bilioni 60 wangekuja hapa wangepata maarifa mengine zaidi," alisema.

Alizitaka halmashauri kutekeleza miradi inayopelekwa kwao bila kusuasua kwa kuingiza maslahi yao hasa katika ajenda ya ununuzi kwa kila mtu kwenda na makaratasi yake ikiwa na mkandarasi wake hali inayofanya miradi hiyo kutoendelea. Awali, Mkurugenzi Msaidizi Idara za Serikali za Mitaa, Angelista Kihaga, alisema miradi ya kimkakati ni utaratibu mpya wa serikali wa kutoa fedha za maendeleo kwa mamlaka za serikali za mitaa.

Naye Kaimu Mkuu wa Chuo cha Hombolo, Dk. Michael Msendekwa, alisema mafunzo hayo yametokana na utafiti uliofanywa na chuo hicho kuonyesha kuna changamoto katika uandishi wa miradi katika mamlaka za serikali za mitaa.



Baadhi ya wachoma nyama wa eneo la Mbande, Wilaya ya Kongwa, mkoani Dodoma, wakiandaa kitoweo hicho juzi, kwenye eneo la wazi bila kujali tahadhari za kiafya, kandokando ya barabara kuu ya Dodoma - Morogoro. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Ofisa elimu sekondari kikaangoni

Na Augusta Njoji, KONGWA

MKUU wa Idara ya Elimu Sekondari katika Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa, Nelson Milanzi, amepewa siku nne za kujieleza kwa maandishi kwa kushindwa kuwajibika katika utekelezaji wa miradi ya elimu kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi).

Agizo hilo lilitolewa juzi na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Tamisemi), Selemani Jafo, alipotembelea miradi kadhaa katika Wilaya ya Kongwa na kukuta shughuli za ujenzi kwa shule mbili za sekondari ukiwa kwenye hatua ya msingi miezi sita tangu kutolewa kwa fedha.

Kutokana na hali hiyo, Jafo alionyesha kuchukizwa na utendaji kazi wa watendaji wa wilaya hiyo kwa kutofanyia kazi maagizo wanayopewa.

Akiwa katika Shule ya Sekondari ya Kongwa ambako ujenzi wa mabweni uko katika hatua ya msingi, Jafo alimwagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Kongwa kumpigia simu Milanzi ambaye yuko Mtwara kwenye mashindano ya Umiseta kurejea kwenye kituo chake cha kazi.

"Na arejeshe fedha za safari alizopewa kwa siku ambazo alitakiwa kuwapo kwenye mashindano hayo ya michezo ya shule za sekondari," aliagiza na kumtaka kuandika barua ya kujieleza kwa nini asichukuliwe hatua kwa kutotimiza wajibu wake. "Akishajieleza Katibu Mkuu atapima maelezo yake na kuamua ama kumbakisha au akapangiwa kazi zingine maana anaweza kurudi kufundisha kuwa ofisa elimu kata," alisema.


Akiwa kwenye Shule ya Sejeli, Jafo alisema kilichofanyika ni uzembe kwa kuwa kazi inaonekana imeanza baada ya kuambiwa Waziri atafika kukagua.

Alisema fedha kwa ajili ya shule hizo zilitolewa na kupokelewa tangu Januari, mwaka huu, lakini hakuna kitu kilichofanyika wakati maeneo mengine waliyopelekewa fedha kama hizo wamemaliza mabweni na wamajiandaa kupokea wanafunzi wa kidato cha tano.

"Mnamwangusha Spika (Job Ndugai) ambaye ametafuta fedha kwa ajili ya wananchi wake, kwa kweli sijaona sababu ya msingi. Nendeni Bahi ina watumishi kama ninyi lakini wanajenga mabweni, madarasa, hospitali ya wilaya na mambo yanaenda vizuri ila hapa sijaridhika," alisema.

Awali, Mkuu wa Wilaya hiyo, Deogratius Ndejembi, na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri, Dk. Omary Nkulo, waliodai kuchelewa kujengwa kwa majengo katika Shule ya Sekondari Kongwa na Sejeli kutokana na kuwapo kwa mvutano wa ama watumei mfumo wa 'Force Account' au watumie mkandarasi.

Katika maelezo yake, Dk. Nkulo pia alisema utekelezaji wa miradi umekuwa ukichelewa kutokana na kuwapo kwa changamoto ya wahandisi wa ujenzi. Alisema kwa sasa kuna fundi mchundo mmoja ambaye ndiye anayesimamia miradi yote inayotekelezwa wilayani hapo.





Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Maendeleo ya Wazee, Wanawake na Watoto, Moudline Castico, akiangalia bidhaa za kazi ya mkono zilizotengenezwa na watoto katika maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika, yaliyofanyika hivi karibuni katika kijiji cha SOS.
**PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# SMZ kuanza mjadala nyongeza gawio BoT

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Fedha na Mipango Zanzibar, imesisitiza kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), inapata gawio la fedha linalotolewa na Benki Kuu ya Tanzania (BoT) la kila mwaka, licha ya kwamba ni kidogo.

Waziri wa wizara hiyo, Balozi Mohamed Ramia Abdiwawa, alisema mgao unaopatikana BoT kwa Zanzibar ni asilimia 4.5 kwa mujibu wa makubaliano yaliyofikiwa, wakati Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inapata mgao asilimia 94.5.

Alisema kiwango hicho ni kidogo na tayari mazungumzo yameanza kufanywa na pande mbili za Muungano kwa ajili ya kuzifanya marekebisha kasoro hizo.

Waziri huyo aliyasema hayo katika Kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akitoa ufafanuzi wa swali lililoulizwa na Mwakilishi wa Jimbo la Shauri Moyo, Hamza Hassan, aliyetaka kujua mwenendo wa gawio la BoT kwa upande wa Zanzibar. Balozi Ramia alisema gawio hilo linapatikana ingawa viwango vinatofautiana mwaka hadi mwaka kutokana na hali ya upatikanaji wa faida ulivyo.

Alieleza kawaida Benki Kuu ya Tanzania haifanyi biashara, isipokuwa kazi yake kubwa ni kuangalia mwenendo wa fedha na mzunguko wake na kuzisimamia benki zilizopo nchini.

Aidha, alisema taasisi hiyo pia hujishughulisha na kuangalia mwenendo wa mfumuko wa bei na hali ya uchumi kwa ujumla na kutoa taarifa serikalini, wafanyabiashara na wawekezaji mbali mbali pamoja na kutafuta ufumbuzi.

"Hizo ndizo kazi za Benki Kuu ya Tanzania, haifanyi biashara kazi yake kuangalia mwenendo wa uchumi na kuzisimamia taasisi nyingine za kifedha pamoja na benki nchini kuona zinafanya kazi zake kwa mujibu wa sheria, hivyo si taasisi ya kuzalisha," alisema Waziri wa Fedha.

# Wawakilishi wamsifu Rais kwa uchapakazi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

BAADHI ya wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wamempongeza Rais John Magufuli, kwa uchapakazi, utekelezaji majukumu na usimamizi wa masuala mbalimbali ya serikali.

Wamesema hayo yote yameleta nidhamu kazini na uwajibikaji serikalini pamoja kuongeza mapato ya taifa.

Mwakilishi wa Viti Maalumu wanawake, Panya Ali Abdallah, alimpongeza Rais Magufuli kwa kitendo chake cha kuwaita wafanyabiashara mbalimbali na kujadiliana nao changamoto zinazokwamisha kiutendaji likiwamo suala la kodi.

Alisema mkutano uliofanywa na Rais Magufuli uliibua mambo mengi ambayo yamesaidia kwa kiasi kikubwa kuzijua kasoro ambazo zinaikosesha serikali mapato yake.

Mwakilishi huyo aliwataka watendaji wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuiga mambo mazuri ya uwajibikaji yanayofanywa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano ili kuzipatia ufumbuzi kero ziliopo katika sekta ya biashara.

"Nachukua nafasi hii kumpongeza kwa dhati amekuwa mfano wa kuigwa kwa watendaji wengine katika uwajibikaji. Kiutendaji tumeona mengi na karibuni mkutano wake na wafanyabiashara ulivyoibua mambo mengi ambayo yalikuwa kero kwa wafanyabiashara wetu," alisema. Naye Mwakilishi wa Jimbo la Mpendae Mohamed Said Dimwa, alisema utendaji kazi wa Rais Magufuli wa kusimamia mashirika ya umma na kuongeza uwajibikaji katika uzalishaji na kutoa gawio Serikali Kuu ni wa kupongezwa.

Alisema katika kipindi cha uongozi wa Rais Magufuli mashirika ya umma yameongeza ufanisi wa kazi na kuwasilisha gawio serikali kuu tofauti na miaka ya nyuma.

"Viongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tuige utendaji kazi wa Rais Magufuli katika kuyabana na kuyasimamia mashirika ya umma, yasiyowasilisha gawio la serikali bora tuyafunge kwa sababu hayana ufanisi wa kazi," alisema Mwakilishi Dimwa.

Dimwa alisikitishwa na taarifa za Waziri wa Fedha na Mipango, Balozi Mohamed Ramia, kwamba mashirika matano ya serikali yametoa gawio la jumla ya Sh. bilioni 5.8 tu.

"Tunayo mashirika ya umma zaidi ya 12 kwa nini mashirika matano tu ndiyo yanayowasilisha gawio la fedha serikali kuu na haya mengine yanafanya nini? Aliuliza Dimwa.

Kwa mujibu wa taarifa za Balozi Ramia aliyataja mashirika yaliyowasilisha gawio kuwa ni Shirika la Bima la Zanzibar, Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ), Shirika la Taifa la Biashara (ZSTC) ,Shirika la Umeme (ZECO) pamoja na Shirika la Bandari la Zanzibar.

# Wanahabari wafundwa kuripoti vyema uchaguzi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Kituo cha Huduma na Sheria Zanzibar, Harusi Mpatani, amewataka waandishi wa habari kuandika habari za uchaguzi bila ya kuleta migogoro ndani ya jamii na taasisi nyingine.

Aliwaambia kuwa watafikia azma hiyo iwapo watafuata sheria zilizopo na kufanyakazi kwa uadilifu na uangalifu.

Akitoa mada inayohusu nafasi ya waandishi wa habari kuripoti uchaguzi mkuu, mkurugenzi huyo, alisema wakati umefika kwa wanahabari kufanya kazi zao kwa mujibu wa sheria ili zisiwe chanzo cha migogoro.

Alieleza kuwa kila miaka inavyosonga mbele sheria za uchaguzi zimekuwa zikibadilika kwa mujibu wa taratibu zilizopo hivyo waandishi wana wajibu kuzijua.

Alisema kuwa uchaguzi wa mwaka 2020 utakuwa tofauti na mwingine uliopita kutokana na hivi sasa kuwepo sheria mpya ya uchaguzi ya mwaka 2018 ambayo ina mabadiliko tofauti na iliyopia.

Mkurugenzi huyo alieleza kuwa katika kipindi cha uchaguzi mkuu wananchi wengi wanakuwa na hamu ya kujua kila kinachotokea na kuwaamini sana waandishi wa habari hivyo, wanataaluma hao wanapaswa kuandika habari zenye ukweli na usahihi.

Wakichangia mada baadhi ya waandishi wa habari walisema umefika wakati kwa vyombo husika vya kutunga sheria kuwa na wigo mpana wa kuwashirikisha makundi mbalimbali ili sheria zikishatungwa zisiwe na changamoto za kiutekelezaji.

Yahya Saleh ni miongoni mwa waandishi wa habari aliyeshiriki mafunzo hayo alieleza kuwa ni vyema waandishi wa habari kuzijua sheria ikiwamo sheria mpya ya uchaguzi ili wanaporipoti habari zao kusiwe na mgongano.

Mapema akifungua mafunzo hayo kwa waandishi wa habari Naibu Mkurugenzi wa Shirika la Marekani la USAID, katika ofisi ya demokrasia na haki za binadamu, Jennifer Horsfall, alisema waandishi wa habari wana dhamana kubwa ya kuwaunganisha jamii na si chanzo cha migogoro ndani ya jamii.

Alieleza kuwa inapotokezea migogoro katika jamii waandishi wa habari wanapaswa kutumia kalamu zao katika kutafutia ufumbuzi mgogoro huo na wasiwe kichocheo cha kuendeleza mgogoro.

Mafunzo hayo ya siku mbili kwa wahariri na waandishi mbalimbali wa Unguja yameandaliwa na Shirika la Kimataifa la Kusaidia Waandishi wa Habari la Internews kupitia mradi wake wa kuboresha habari kwa kushirikiana na USAID.

# Waajiri watakiwa kulipa madeni

**Na Boniface Gideon,** TANGA

KAIMU Mkuu wa Mkoa ambaye pia ni Mkuu wa Wilaya ya Tanga, Thobias Mwilapwa, amewataka waajiri wote wanaodaiwa kwenye vyama vya ushirika mkoani hapa, kulipa madeni ya wafanyakazi wao haraka iwezekanavyo kabla hawajachukuliwa hatua kali za kisheria.

Kauli hiyo aliitoa jana wakati akifungua mkutano wa mwaka wa vyama vya ushirika Mkoa wa Tanga.

Mwilapwa alisema wapo waajiri ambao wanakwamisha vyama vya ushirika visiendelee kwa kushindwa kulipa madeni yao kwa wakati na wengine wakiwa serikalini.

Alisema baadhi ya waajiri hao ni pamoja na Wakurugenzi wa Halmashauri. "Wapo waajiri kiukweli wamekuwa wakikwamisha vyama vya ushirika hapa mkoani kwetu kwa ujumla wamekuwa kizuizi cha vyama vya ushirika mpaka kufikia hatua ya kushindwa kujiendesha," alisema Mwilapwa.

Alisema wapo pia wana ushirika ambao ni kikwazo kikubwa kwenye vyama vyao kwa kuwa wanakopa na kushindwa kurejesha madeni.

Kwa upande wake Mrajisi Msaidizi wa vyama vya ushirika Mkoa wa Tanga, Jackline Senzighe, alisema vyama vya ushirika mkoani Tanga vinakabiliwa na changamoto kubwa ya ukata wa fedha unaosababishwa na wanachama kushindwa kurejesha mikopo kwa wakati.

Baadhi ya wanachama wa vyama vya ushirika mkoani Tanga, akiwamo David Mbogi, alisema vyama vya kuweka na kukopa (Saccos) vimekuwa muhimili mkuu kwa wafanyakazi kwa kuwa vinawakwamua kiuchumi.



Mwakilishi wa Mkuu wa Wilaya ya Tarime, Jonathan Machango, akikata utepe kuzindua mnara wa Tigo wa 4G, mjini Tarime, mkoani Mara jana. Kushoto ni Mwakilishi wa Mkurugenzi wa Wilaya ya Tarime, Emmanuel Sizo, Meneja wa Tigo Kanda ya Ziwa Kaskazini, Daniel Mainoya (wa pili kushoto), na Meneja Mauzo wa Tigo wa mkoa huo, Abdillahi Luhorela. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanaozunguka machimbo wapimwa vimelea vya TB

**Na Gideon Mwakanosya,** TUNDURU

WANANCHI wa vijiji vinavyozungukwa na machimbo ya madini katika Wilaya ya Tunduru, mkoani Ruvuma, wameanza kupimwa vimelea vya ugonjwa wa kifua kikuu kama hatua mojawapo ya kukabiliana kuenea na kupunguza ugonjwa huo hasa baada ya kubainika kuwa wilaya hiyo inaongoza kuwa na idadi kubwa ya watu wanaougua ugonjwa huo.

Kampeni ya uchunguzi wa vimelea vya TB inafanyika katika machimbo yote ya madini katika vijiji vya Majimaji, Muhuwesi na Magomeni, ambapo watu wanaojihusisha na uchimbaji wa madini wanatajwa kuwa kundi mojawapo ambalo limeathirika na ugonjwa wa kifua kikuu.

Kampeni hiyo inafanywa na Shirika Linalojihusisha na Uboreshaji wa Huduma za Afya (MDH) kwa kushirikiana na Hospitali ya Wilaya ya Tunduru chini ya kitengo cha kifua kikuu na ukoma na inalenga kuwafikia watu wote wanaoishi katika maeneo ya machimbo na vijiji vyote vinavyozungukwa na shughuli za uchimbaji.

Akizungumza na wananchi wa kijiji cha Majimaji na Magomeni kabla ya kuanza kwa zoezi la uchunguzi wa vimelea vya ugonjwa huo, Ofisa mradi wa uibuaji wa wagonjwa wa kifua kikuu katika jamii kutoka Shirika la MDH, Mkoa wa Ruvuma, Dk. Nixson John, alisema uchunguzi wa wagonjwa wachimbaji wa madini pamoja na vijiji vinavyozunguka maeneo hayo linafanyika katika wilaya zote za Mkoa wa Ruvuma. Kwa mujibu wa Dk. Nixson, zoezi hilo lilianza Mei 12 hadi 17 na katika Wilaya ya Tunduru, uchunguzi ulifanyika kwenye machimbo ya wachimbaji wadogo katika kata ya Muhuwesi na Majimaji na idadi ya wahisiwa wa ugonjwa wa kifua kikuu 202, na sampuli 200 za makohozi zilikusanywa. Alisema, mpaka sasa watu waliogundulika na maambukizi ya vimelea vya kifua kikuu ni tisa kati ya sampuli zilizokwishapimwa, kati yao mtoto mmoja alianzishiwa dawa kutokana na kukidhi vigezo na mtu mzima mmoja alianzishiwa kwa kuwa na dalili za kifua kikuu nje ya mapafu na zoezi la upimaji wa sampuli bado linaendelea.

Dk. Nixson alisema, wataalamu walioshiriki katika kazi hiyo ni kutoka Hospitali ya Wilaya ya Tunduru, wakiongozwa na Mratibu wa Kifua Kikuu na Ukoma, Dk. Mkasange Kihongole na Shirika la MDH ni watekelezaji wa mradi chini ya ufadhili wa mfuko wa Dunia wa Mapambano ya Ugonjwa wa Kifua Kikuu, Malaria na Ukimwi (Global Fund).

Mratibu wa kifua kikuu na ukoma wa Hospitali ya Wilaya ya Tunduru, Dk. Mkasange Kihongole, alisema watu wanaoishi katika vijiji vinavyozungukwa na machimbo na wanaoishi katika maeneo ya machimbo wako katika hatari zaidi kupata ugonjwa.

Alisema, hali hiyo inatokana na mwingiliano wa mara kwa mara na mkusanyiko mkubwa wa watu kutoka katika maeneo mbalimbali ambao baadhi tayari wamepata maradhi ya kifua kikuu.

Dk. Kihongole alisema, kampeni ya uchunguzi wa vimelea vya ugonjwa huo katika Wilaya ya Tunduru imefanyika katika vijiji vya Muhesa, Majimaji na Magomeni na jumla ya sampuli zilizochukuliwa kwa ajili ya kufanyiwa uchunguzi ni 200 na mpaka sasa zilizopimwa na kupata majibu ni wagonjwa tisa na upimaji unaendelea.

Alisema, ugonjwa wa kifua kikuu ni miongoni mwa magonjwa 10 duniani ambayo yanaongoza kwa kuua watu, ndiyo maana kwa kutambua ukubwa wa tatizo serikali kwa kushirikiana na mfadhili Shirika la MDH limeanza uchunguzi na upimaji kwa wananchi kwa kuwafuata vijijini kwa ajili ya kufanya uchunguzi wa vimelea vya TB badala ya kuwasubiri ofisini.

# Waiomba NEC kutoa usafiri wakati wa kampeni

**Na Christina Haule,** MOROGORO

WANANCHI wa kata tano za wilaya mbalimbali mkoani Morogoro wameiomba serikali kupitia Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kuona umuhimu wa kupunguza gharama za uchukuaji fomu na kuweka usafiri kwenye kampeni kwa wagombea wenye ulemavu na wanawake, ili kuwawezesha kufikia malengo yao ya ushindi.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti kwenye mafunzo ya kujenga uelewa kwa wadau mbalimbali juu ya uongozi kwa mrengo wa kijinsia yaliyoandaliwa na mtandao wa jinsia Tanzania (TGNP-Mtandao) kwa kushirikiana na wadau wao NORAD, washiriki hao akiwamo Abdalia Sultani, mkazi wa Kata ya Mikese alisema, wagombea wanawake na wenye ulemavu katika uchaguzi mbalimbali wamekuwa wakikumbwa na changamoto za gharama hizo na kubaki wakitegemea viti maalum kwa wanawake.

Sultani alisema, serikali ipunguze gharama hizo na kuondoa nafasi ya viti maalum ambayo imekuwa ikiwalemaza wanawake.

"Gharama za uchaguzi ambazo ni kuchukua fomu huwa ni Sh. 150,000 kwa serikali za vijiji, udiwani Sh. 50,000 na ubunge Sh. 100,000, na gharama za usafiri kwenye kampeni, vimekuwa mwiba kwa wagombea wanawake jambo linalofanya kutokuwa na uwiano au mrengo wa kijinsia katika matokeo ya uchaguzi," alisema.

Alisema kura za wagombea viti maalum ndizo zinapoteza nafasi za uongozi kwa kinamama na kwamba kungekuwa na mabadiliko ya kutokuwa na viti maalum mapema wanawake wangegombea nafasi kama wanaume.

"Ni lazima wanawake wakubali kushawishiwa kugombea na kuwa na idadi kubwa ya wanawake katika ngazi ya uchaguzi, huku mkiacha dhana ya 'tukiwezeshwa tunaweza" bali msimame kwa miguu yenu wenyewe," alisema.

Akizungumzia hilo mshiriki mwingine kutoka Kata ya Kisaki, Tatu Mleta aliiomba serikali kutenga bajeti za gharama za usafiri wa kuzunguka kujitangaza kwa wananchi ili kusaidia wanawake ambao wengi wao hushindwa kutokana na kukosa kipato.

"Wanawake mara nyingi hasa wa vijijini hatuna kazi, sasa gharama zinapozidi zinatuchanganya na kutufanya wakati mwingine kukata tamaa," alisema Maleta.

Naye Ofisa Prorgamu wa TGNP-Mtandao, Deoratius Temba, aliiomba serikali kuondoa gharama zozote zinazokuwa kikwazo kwa wanawake, vijana na wenye ulemavu kushiriki kikamilifu kwenye uongozi ikiwamo kuchukua fomu na usafiri kufuatia wengi wao kutokuwa kwenye mfumo wa ajira.

Alisema, marekebisho hayo yatasaidia si kwa uchaguzi wa 2019/20 pekee bali hata kuleta manufaa kwenye chaguzi zijazo.

Mafunzo hayo ya siku mbili yamehusisha viongozi wa dini, asasi za kiraia, mitandao ya kijamii, viongozi wa dini na mila kutoka katika kata za Turiani-Mvomero, Mkambarani-Mikese, Tomondo, Kisaki na Bwakila Chini.

HABARI KITAIFA

## UNHCR: Watu milioni 71 wanaishi kama wakimbizi duniani

**GENEVA, Switzerland**

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa linalohudumia Wakimbizi (UNHCR) limesema watu takriban milioni 71 wameyakimbia makazi yao duniani kote, kuepuka ghasia na unyanyasaji.

Miongoni mwao milioni 41 ni wakimbizi wa ndani ya nchi zao.

Ripoti hiyo ya UNHCR imetangazwa kwenye mkesha wa siku ya kimataifa kwa ajili ya wakimbizi ambayo inaadhimishwa leo.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, watu milioni 70.8 walilazimika kuyahama makazi yao mwaka jana, likiwa ni ongezeko la watu karibu milioni mbili ikilinganishwa na mwaka juzi.

Akizindua ripoti hiyo jana mjini Geneva, Kamishna wa UNHCR, Filippo Grandi alisema kwa bahati mbaya ongezeko hilo linachukua mwelekeo usio sahihi.

Grandi amepinga dhana kwamba wote wanaozihama nchi zao ni wakimbizi wa kimaslahi.

"Watu huyahama makazi yao kwa sababu mbalimbali, ambazo tunaweza kuziita za mseto. Bila shaka, wapo wanaoondoka kutafuta fursa bora za kiuchumi, lakini, na wapo wengine ambao wanakimbia ghasia na vitisho vikubwa wanavyofanyiwa," alisema Grandi.

Kiongozi huyo wa UNHCR alisema matatizo ya wakimbizi yanaongezeka kasi kwa muda wanaoishi uhamishoni, na kwamba asilimia 80 wamekuwa wakimbizi kwa zaidi ya miaka 5.

Wakimbizi waliokimbia vita vya Syria vilivyodumu kwa miaka minane, ndilo kundi kubwa, wakifika karibu milioni 13.

Kundi lingine la wakimbizi ambao ni wengi wametoka nchi ya Wavenezuela, idadi yao yafikia 340,000. Ripoti hiyo kuhusu wakimbizi inaonyesha kuwa watu milioni nne wamezihama nchi za Amerika Kusini mnamo miaka ya hivi karibuni, lakini ni mmoja tu kati ya wanane ambaye ameomba rasmi hifadhi ya ukimbizi.

Grandi alisema Marekani bado ndio mfadhili mkubwa wa shughuli za kuwasaidia wakimbizi ulimwenguni, lakini alikosoa kauli kali dhidi ya wakimbizi ambazo zimejitokeza hivi karibuni. Alisema si Marekani tu bali hata Ulaya wakimbizi na wahamiaji wanachukuliwa kama watu waliokuja kuwapokonya wenyeji fursa zao za ajira, na kutishia usalama na maadili yao ya kijamii.

UNHCR imesisitiza kwamba idadi kubwa ya wakimbizi na wahamiaji iko katika nchi zanazoendelea, sio katika mataifa tajiri. Imeonyesha pia kwa miaka saba mfululizo, idadi ya wakimbizi imekuwa ikipanda kila mwaka ikivunja rekodi ya iliyotangulia. *DW*

# Uganda kuanza kutumia chanjo kujikinga na ebola

**KAMPALA, Uganda**

MAOFISA wa afya nchini Uganda wamepewa idhini ya kutumia dawa za majaribio kutibu ugonjwa wa ebola, ikiwa imepita wiki moja baada ya watu wawili walioingia nchini humo wakitokea Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) kufariki dunia kwa ugonjwa huo.

Waziri wa Afya nchini Uganda, Jane Ruth, aliandika katika ukurasa wake wa mtandao wa kijamii wa Twitter kuwa: "Ni furaha kufahamisha umma kwamba, tumepata kibali kutoka Baraza la Sayansi na Teknolojia la Uganda na vile vile kutoka kwa Mamlaka ya Taifa inayoshughulikia dawa kwamba tunaweza kutumia dawa hizo kutibu ebola".

Hata hivyo, Waziri Jane hakuweka maelezo zaidi ya dawa zipi zilizoidhinishwa na kwa kiasi gani zitaagizwa.

Aina nne za dawa za kutibu ebola tayari zinatumika nchini Congo.

Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO), linaeleza kwamba watu wawili waliofariki kwa ugonjwa huo nchini Uganda walitokea Congo, mvulana wa miaka mitatu aliyerudishwa Congo baada ya kupatikana na maradhi hayo alifariki mwishoni mwa wiki.

Hadi sasa nchini Congo zaidi ya watu 2,000 wameshaambukizwa maradhi ya ugonjwa wa ebola, huku watu 1,411 wamefariki dunia tangu Agosti baada ya kuzuka kwa mara ya pili mlipuko wa maradhi hayo.

Ofisa mawasiliano wa WHO, Benjamine Sensasi, alisema wananchi nchini Uganda wameingia hofu na wako tayari kupokea chanjo hiyo.

"Hawaonekani kuogopa wako tayari kupokea chanjo, ni chanjo isiyodhuru. Chanjo hiyo inatolewa kama inavyotolewa chanjo zingine. Kwa hivyo hakuna kitu cha maajabu na wanaelewa ni kwa ajili ya manufaa yao wenyewe kuweza kuwa na afya bora na kuokoa maisha ya wengine," alisema Benjamine.

Baada ya kuzuka kwa maradhi hayo mwaka 2013 wanasayansi wa matibabu wamekuwa wakitafuta chanjo na dawa za kutibu ama kuzuia kuzuka tena kwa virusi vinavyosababisha ebola.

Lakini tangu kuzuka kwa ebola Agosti mwaka jana, maradhi hayo yamekuwa yakisambaa kwa kasi kaskazini mwa mkoa wa Kivu nchini Congo.

WHO inasema hadi sasa hakuna taarifa yoyote iliyotolewa ikieleza kusambaa kwa ebola nchini Uganda na matukio yaliyoripotiwa yote ni ya watu wanaotokea nchini Congo.

WHO imesema imeamua kutotangaza hali ya dharura nchini Congo licha ya kusambaa kwa maradhi hayo hadi Uganda kwa sababu kufanya hivyo kutasababisha madhara makubwa ya kiuchumi.

Mtaalamu wa maradhi yanayosababishwa na virusi ambaye pia ni msaidizi wa Profesa wa Chuo Kikuu cha Queensaland nchini Australia, Ian Mackay, alisema licha ya kuwapo kwa upimaji wa mara kwa mara wa kiafya, dawa na chanjo bado maradhi hayo yanaendelea kwa sababau za kiimani na tabia za watu wenyewe. *DW*



Waziri wa zamani wa Mambo ya Nje wa Uingereza, Boris Johnson kutoka chama cha Conservative, ambaye anapewa nafasi kubwa ya kumrithi Waziri Mkuu wa Uingereza, Theresa May. **PICHA: REUTERS**

## Mwanamfalme wa Saudi Arabia kuchunguzwa kwa mauaji

**RIYADH, Saudi Arabia**

UCHUNGUZI uliofanywa na wataalamu wa Umoja wa Mataifa (UN), umeonyesha kuwa mwanamfalme wa Saudi Arabia, Mohammed bin Salman na maofisa wengine wa serikali walihusika na mauaji ya mwanahabari Jamal Khashoggi.

Mtaalamu wa UN aliyeongoza uchunguzi huo, Agnes Callamard, katika ripoti yake, alieleza kuwa ushahidi walioupata unathibitisha kuwa Khashoggi aliuawa katika ubalozi mdogo wa Saudi Arabia mjini Istanbul nchini Uturuki na waliohusika ni maofisa wa usalama wa Saudi Arabia.

"Haiwezekani kuwa mwanamfalme Mohammed bin Salman hakufahamu kuhusu kilichotokea, mauaji hayo yanakwenda kinyume na sheria za kimataifa kwa hivyo ni vema uchunguzi zaidi ufanyike," alisema Callamard na kuongeza:

"Hakika kwa uchunguzi wetu, mauaji ya Khashoggi, yalipangwa na yalikuwa yanafahamika vema."

Aidha, ripoti hiyo, imemtaka Salman kuchunguzwa kutokana na mauaji hayo ya Khashoggi kwa sababu ushahidi unaonyesha kuwa alifahamu kila kitu.

Imebainika pia kuwa wauaji wa Khashoggi walikuwa washirika wa karibu wa mwanamfalme Salman, na walinaswa kupitia mkanda wa sauti, wakijadiliana kuhusu mauaji hayo.

Khashoggi raia wa SaudI Arabia aliuawa akiwa na umri wa miaka 58, wakati alipokwenda katika ubalozi wa nchi yake Oktoba 2018, alipokwenda kutafuta vibali ili kufunga ndoa na mpenzi wake Hatice Cengiz.

Wakati wa uhai wake, alikuwa mkosoaji mkubwa wa serikali ya Saudi Arabia kupitia makala alizokuwa anaandika kupitia Gazeti la Washington Post.

Saudi Arabia imeendelea kukanusha madai ya kuhusika na mauaji ya Khashoggi na tayari imewafungulia kesi washukiwa 11 kwa madai ya kutekeleza mauaji hayo.

Hata hivyo, ripoti ya UN inaeleza kuwa kesi dhidi ya washukiwa hao ambao hawajafahamika, haijafikia viwango vya kimataifa vya kisheria vinavyotakiwa. Mwili wa Khashoggi haujawahi kupatikana. *RFI*

# Wafanyabiashara ya damu Vingunguti walia kunyanyaswa

**Na Beatrice Shayo**

WAFANYABIASHARA wa damu katika machinjio ya Vingunguti wamelalamikia kufanyiwa unyanyasaji, huku wakidai kubambikiwa kesi na kulazwa mahabusu bila sababu za msingi.

Akizungumza kwa niaba ya wafanyabiashara hao, Joseph Abdallah, alimtuhumu mfanyabiashara Anna Peter, kuwafanyia unyanyasaji tangu afike eneo hilo.

"Tumekuwa tukikamatwa mara kwa mara hapa hatuna amani mara tunaambiwa tulitaka kumuua, kupitia fedha zake hatufanyi biashara kwa raha tunanyanyasika tunaomba viongozi wa juu waingilie kati suala hili," alisema.

Abdallah alisema kabla ya mama huyo kuanza kuchukua damu katika machinjio hayo, walikuwa wanafanya biashara zao kwa amani bila kufanyiwa unyanyasaji.

"Huyu mama anataka damu yote aichukue yeye anadai amepewa kibali na mahakama, je, sisi tutaenda wapi wengine hii biashara tuna zaidi ya miaka 15 tunaifanya yeye kaja majuzi hataki sisi tuifanye hili hatukubali," alisema.

Alisema wanachokitaka ni serikali ije na wanasheria wake kwa ajili ya kuangalia mikataba ya huyo mfanyabiashara ili kuondoa mgogoro uliopo.

Sabina Benedict alisema ameanza kuifanya biashara hiyo tangu mwaka 2009 walivyojitokeza waathirika wajane ambao wapo 20 wakajisajili na Manispaa ikawatengenezea hadi majiko ili yawasaidie.

Alidai mfanyabiashara huyo kutoa mamilioni ya fedha kwa chama kingine cha wachinjaji huku wao wakifukuzwa.

"Sisi ambao tumeathirika maisha yetu magumu huyu mama kaja mwaka 2014, hataki sisi tuifanye hii biashara anatuambia damu yote ya machinjio ni yake," alidai.

Kwa upande wake, Jasmine Yaki, alisema alishapelekwa Segerea na kuwaacha watoto wake nusu wabakwe anamshukuru mjumbe wake alimsaidia.

Alisema baada ya kutoka jela alikamatwa tena na kuwekwa kituo cha polisi kwa siku 16 jambo ambalo linamuumiza kuendelea kuteswa katika biashara hiyo.

"Fedha za Anna Peter ni fimbo ya kutuchapia sisi wanyonge ambao ni wajane wakati tuliruhusiwa kufanya biashara, tunamuomba Rais John Magufuli atusaidie," alisema huku machozi yakimtoka.

Kaimu Meya wa Manispaa ya Ilala, Omary Kumbilamoto, ambaye pia ni Diwani wa Kata ya Vingunguti, alipoulizwa kuhusu tuhuma hizo, alisema tayari mgogoro huo ulishamalizika tangu mwaka 2016 na kwamba atakayechinja ng'ombe damu hiyo ni mali yake na anauwezo wa kuiuza.

Alisema ameshangazwa na mgogoro huo kuibuka tena, hivyo atakwenda kuandaa kikao na kuwaita pande hizo na kuongea nao ili kufikia mwafaka.

Kuhusu mfanyabiashara wanayemtuhumu (Anna Peter) kutajwa kuwatesa wafanyabiashara hao, alisema hawakubaliani na jambo hilo na kwamba watamchukulia hatua.

"Huyu mfanyabiashara Anna Peter simfahamu nimemsikia hapa. Sisi kama viongozi tutaangalia pande zote mbili kama anafanya mateso tutatoa agizo usitishwaji huo usiwepo maana serikali ya Rais John Magufuli haipendi watu kunyanyaswa," alisema.

Naye Anna alipohojiwa kuhusu tuhuma zinazomkabili, alisema biashara yake ni ya kihalali na mahakama imempa uhalali wa kuchukua damu hiyo mpaka deni lake litakapomalizika.

"Hao waliobeba mabango ndio walionipiga panga wasubiri deni langu liishe ndio hao wajane watapata damu bure, wakitaka kununua kwangu ni Sh. 18,000," alisema.




Mkuu wa Kitengo cha Masoko ya Nje wa Benki ya Barclays Tanzania, Esther Maruma (wa pili kushoto), akizungumza na Mkurugenzi wa Uendeshaji wa Hoteli ya Hyatt Regency jijini Dar es Salaam, Timothy Mlay (wa pili kulia), wakati wa uzinduzi rasmi wa kituo cha kubadilishia fedha za kigeni cha benki hiyo, hotelini hapo, jana. Wengine (kushoto) ni Meneja wa Benki hiyo, Tawi la City Mall, Winford Mwang'onda na Mkuu wa Kitengo cha Wateja Binafsi, Oscar Mwamfwagasi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mataifa kupambana vita dhidi ya tabianchi 2020

**Na Jenifer Julius, BONN**

MATAIFA mbalimbali duniani yametakiwa kufanya kazi pamoja ili kufikia makubaliano ya Paris ya kupunguza ongezeko la joto kufikia nyuzi mbili katika mabadiliko ya tabianchi.

Aidha, mataifa hayo yametakiwa yaendane na uhamasishaji kwa nchi zilizoendelea ili ziongeze michango kufikia Dola za Kimarekani bilioni 100 zinazohitajika kusaidia majanga yanayotokana na athari za mabadiliko ya tabianchi kwa nchi zinazoendelea.

Akizungumza katika mkutano wa mabadiliko ya tabia nchi unaoendelea mjini Bonn, nchini Ujerumani, mwakilishi kutoka Shirika la Kimataifa la Action Aid, Harjeet Sighn, alisema nchi zinazoendelea zinashindwa kwenda na kasi inayotakiwa kufikia kupunguza nyuzi joto kwa sababu haziwezi kujiendesha zenyewe.

"Ni miaka sita sasa tangu kuingia makubaliano ya nchi kupunguza joto, lakini hakuna mfumo wowote ulioandaliwa kusaidia nchi maskini kupambana na athari za mabadiliko ya tabia nchi," alisema Sighn.

Alisema mataifa yanayoendelea yanapitia changamoto mbalimbali zinazotokana na athari za mabadiliko ya tabia nchi kama vile mafuriko, ukame, uhaba wa chakula, hivyo zinahitaji msaada hasa wa kifedha ili ziweze kuendana na kasi ya makubaliano ya Paris.

Alitoa mfano wa Zimbabwe ambayo bado inahitaji msaada wa Dola za Kimarekani milioni 612, kujikimu na athari za kimbunga cha Idai kilichosababisha maelfu ya watu kupoteza makazi.

Wakati nchi zinazoendelea zikipiga hatua katika kufikia malengo ya makubaliano ya Paris ya kupunguza joto kwa asilimia 1.5- 2, hali ni tofauti kwa nchi zinazoendelea kutokana na vikwazo vinavyopitia ikiwamo ukosefu wa fedha za kufanikisha utekelezaji huo.

Naye mchambuzi wa kimataifa wa masuala ya kisera kutoka kampuni ya Climate Action Network (CAN), Eddy Perez, alisema ikiwa umebaki mwaka mmoja kufikia 2020, mataifa yaliyoendelea yanatakiwa kutoa ripoti ya jinsi gani yamefanikisha kupatikana dola bilioni 100.

Anashauri nchi zinazoendelea kuhamasishwa ili ziweze kutoa msaada kama vile Norway na Ujerumani, ambao wameongeza msaada mara mbili katika Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi.

Aidha, alisisitiza kuwapo mifuko wa "loss and damage" ambao utasaidia nchi zinazoedelea zinapopata majanga yanayotokana na athari za mabadiliko ya tabia nchi.

Nchi za Afrika zimekadiria kuhitaji msaada wa Dola za Kimarekani bilioni 100 kukabiliana na athari hizo, lakini changamoto kubwa imekuwa ni jinsi gani pesa hizo zitapatikana hali inayoiweka nchi hizo njia panda.

Akifungua mkutano huo, Mwenyekiti wa Bodi ya Utekelezaji (Subsidiary body of Implementation), Emanuel Diamini, alisema wanahitaji nguvu ya ziada ili kufikia utekelezaji wake kabla ya muda uliopangwa.

Mkutano wa mabadiliko ya tabia nchi ulianza jana mjini hapa na mataifa 188 yanatarajiwa kukutana kujadili ajenda zilizoachwa katika mkutano wa Cop 24 uliofanyika mwaka jana, ambao makubaliano yatajadiliwa mwaka huu kwenye Cop 25.

# Tarime wapelekewa mtandao 4G wa Tigo

**Na Mwandishi Wetu**

WAKAZI wa Tarime mkoani Mara na maeneo ya jirani, sasa wanaweza kupata huduma za mtandao wenye kasi zaidi wa 4G baada ya kampuni ya Tigo kuzindua mnara wenye uwezo wa kutoa huduma hiyo wilayani humo.

Kufuatia uzinduzi huo, wateja wa Tigo wataweza kupata huduma bora na za uhakika zaidi watakapokuwa wanapiga simu, wanapotumia intaneti pamoja na huduma za kutuma na kupokea fedha (Tigo Pesa).

Mkuu wa Wilaya wa Tarime Mjini, Charles Francis Kabeho, aliikaribisha uwekezaji huo na kuushukuru uongozi wa Tigo kwa kuunganisha wakazi wa Tarime na teknolojia pamoja na mtandao wa 4G.

"Tunaishi katika nyakati za sayansi na teknolojia, shughuli nyingi hufanikishwa kupitia mawasiliano ya simu za mkononi au mtandao wa intaneti. Kama mnavyofahamu, Tarime ni mji wa uchimbaji madini," alisema na kuongeza:

"Tumepakana kusini na mbuga ya Serengeti, na upande wa kaskazini mpaka mashariki ni nchi ya Kenya, hii ina maanisha kwamba mtandao huu mpya wa 4G utawezesha shughuli zetu za kiuchumi kwenda kwa kasi zaidi."

Meneja wa Tigo Kanda ya Ziwa, Daniel Mainoya, alisema kampuni hiyo inawahakikishia wakazi wa Tarime kupata huduma bora na ya gharama nafuu kupitia ofa zake za kibunifu ikiwa ni pamoja na ofa ya 'Saizi Yako'.

"Kupitia ofa ya Saizi Yako, kama mteja anatumia muda wa maongezi zaidi kuliko intaneti na SMS, basi atapata kifurushi chenye muda wa maongezi zaidi. Na kama mteja anatumia zaidi intaneti kuliko muda wa maongezi na SMS, mteja huyo atapata kifurushi cha intaneti chenye GB zaidi. Utaratibu huo utafuatwa pia kwa ajili ya SMS," alisema Mainoya.

# TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MAGARI NA VIPURI

**CRANE FUSO FOR SALE,**

(1.) Fighter 2002, SAKAI_340,3 stages, New in TZ,
2. Magnum 1991, TADANO_290, 2 Stages, 3 years in TZ.

**"Dalali Hatakiwi" Simu 0692 469 669**

## NAFASI ZA KAZI

**TANGAZO LA KAZI ,** Mtu wa IT diploma anahitajika na Mesenger form six. Mawasiliano: 0715 885533


## ELIMU/ MASOMO

**NAFASI ZA MASOMO,** Chuo cha Uuguzi na Ukunga MASSANA kilichopo dar es Salaam, Mbezi Beach Goba Road. Kinatangaza nafasi za masomo kwa ngazi ya Diploma na cheti yatakayoanza mwezi wa September 2019. Njoo tukujazie Form Kupitia Mtandao wa Nacte: 0713 321260/0769 666880


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI



## KUPOTEA KWA CHETI



**Hussein Ahamad** anatangaz kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S. 0105/0030** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 1997 katika shule ya Sekondari Chidya Mtwara. Yeyote atakaeiona atoe Taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **IGU/RB/1104/2017**

115285202


## KUPOTEA KWA CHETI



**Ezekieli Salvatory Massawe** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S.4405/0515,** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2017 katika shule ya Sekondari St. Amedeus. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **DAR/MBA/RB/69231/2019**

115284502

## KUPOTEA KWA PASSPORT/ HATI YA KUSAFIRIA



**Collins Robert Mongi** anatangaza kupotelewa na Passport/Hati ya kusafiria yenye namba **TAE087154** iliyotolewa ofisi za Uhamiaji Dar es Salaam mwaka 2019. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **DAR/OST/RB/70462/2019**

115284302

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 232233
Barua Pepe ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,
19/06/2019

## TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya IJUMAA tarehe **21/06/2019** kampuni ya **MEERO CONTRACTORS** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka KIJENGE ARUSHA kuelekea **ARUSHA NATIONAL PARK (MOMELA)** gari hilo lina namba za usajili: **T.747 ASM/T.163 DLR.**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| **Urefu** | – | **mita 17** |
| **Upana** | – | **mita 3.0** |
| **Kimo** | – | **mita 4.9** |

3. Njia itakayotumika **KIJENGE ARUSHA** hadi **ARUSHA NATIONAL PARK (MOMELA) kupitia MANDELA ROAD** gari litasafiri muda wa mchana tu (Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.SC***

215285102

## GOROFA INAUZWA



BOKO KAMWANGA STR
LOW DENSITY AREA
BLOC "C",
PLOT NO. 65

**SIMU**: 0754 226 687 / 0756 410 345.

115258902

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**TUMPE ATUFIGWEGE ANGETILE** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T352 AGV** AINA YA SUZUKI STATION WAGON. CHASSIS NAMBA **TDOIW280518.** ENGINE NAMBA **G16A431475.** YEYOTE ATAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.TAARIFA YA POLISI **SM/TRB/6866/2019.**

115285702

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MOHAMED HIMID MBAYE** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 959 BDC** AINA YA TOYOTA CORONA. CHASSIS NAMBA **AT2110117223.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU. TAARIFA YA POLISI **SMT/RB/6866/2019.**

115285802

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo: MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;130/2019**

**Ombi la WILFRED D.MWORIA Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu ALPHONCE AUGUSTINO MWORIA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 19/07/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa Tarehe 18/06/2019.



115285502

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;131/2019**

**Ombi la APOLONIA MELIKIORI SWAI Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu ANDERSON ELIA SOKA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 05/07/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 18/06/2019.



215285002

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;133/2019**

**Ombi la STELA RAPHAEL MASAWE Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu GODSON ULIRK MKENDA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 19/07/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 19/06/2019.



215284902

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M. 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

**Katika Mahakama ya mwanzo MJINI -TANGA**

**Usimamizi wa Mirathi NAMBA 84/2019**

**Ombi la HASSANI MOHAMEDI kuteuliwa Msimamizi wa mirathi marehemu NGARE ISSA NGARE**

**Kwa YEYOTE ANAYEHUSIKA**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 05/07/2019 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe **07/06/2019**



215284002

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo: MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;134/2019**

**Ombi la BENNO TIMOTHY MSIMBE Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu ANNA PAULO FERDINAND**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 24/06/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa Tarehe 19/06/2019.



115285302

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KTK MAHAKAMA YA MWANZO MJINI**
**ILIYOPO MOROGORO**

**TANGAZO LA KUITWA SHAURINI**

**SHAURI LA MADAI NAMBA:26..2019**

**Mdai: ........................................JONESTA SALVATORY**

**DHIDI YA**

**Mdaiwa: ........................................ESDORY MASONDA**

**Kwa: ESDORY MASONDA**

**Ombi la Mdai: JONESTA SALVATORY**
**Madai ya: PESA SHILINGI LAKI TISA (900,000)**

Unatakiwa kuudhuria hapa mahakamani ktk shauri tajwa hapo juu bila kukosa.Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 12 mwezi 07 mwaka 2019 saa 08:30 Asubuhi.
Angalia kama hukuudhuria/hamkuudhuria siku iliyotajwa hapo juu.Mahakama ikidhibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini,hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa /mmeshindwa.
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 19 mwezi 06 mwaka 2019.



115285402

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM 11**
**(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

**Katika Mahakama ya Mwanzo DODOMA MJINI**

**Usimamizi wa mirathi 46/2019**

**Ombi la FATUMA JUMA HIDA kuteuliwa Msimamizi wa mirathi Marehemu JUMA HIDA NKUMBI.**

**KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA TANZANIA- BARA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnano tarehe 2/7//2019 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa Tarehe 19/6/2019



215284402

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M. 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

**Katika Mahakama ya mwanzo MJINI -TANGA**


**Usimamizi wa Mirathi NAMBA 78/2019**

**Ombi la MAIMUNA SALIM BUGU kuteuliwa Msimamizi wa mirathi marehemu MWANAM-WISHO ALLI MKANGA**

**Kwa YEYOTE ANAYEHUSIKA**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 24/6/2019 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa. **Tarehe 23/5/2019.**



215284102


*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Tupigie 0767 223 311*


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## ATLETICO MADRID YAMGEUKIA XHAKA

**LONDON, England**

KLABU ya Arsenal imejikuta kwenye wakati mgumu baada ya kuletewa ofa na Atletico Madrid wakimtaka, Granit Xhaka.

Atletico wanataka kumsajili kiungo huyo kwa ajili ya kuziba nafasi ya Rodri, ambaye anakaribia kutua pale Manchester City.

Kwa mujibu wa Gazeti la The Mirror, Atletico wamemuona Xhaka kama ndio chaguo lao la kwanza la kurithi nafasi ya kiungo ya Rodri.

Arsenal haitaki kumuuza Xhaka, lakini Atletico imepanga kutuma ofa kubwa zaidi kwa ajili ya kumsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa Uswisi ili aondoke pale kwenye dimba la Emirates.

Xhaka msimu uliopita alikuwa nguzo muhimu zaidi kwa kikosi hicho akicheza mechi 40 kwa 'Washika Bunduki' hao katika mashindano yote.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, kwa ujumla amekuwa kwenye kiwango cha kuvutia zaidi tangu atue hapo, na sasa Arsenal inajiuliza mara mbilimbili uwezekano wa kumuuza.

Mwaka jana Xhaka alisaini mkataba mpya ambao utamfanya kukaa hapo Arsenal hadi kipindi cha majira ya joto msimu wa 2023.

Huku Aaron Ramsey tayari akiwa ameshaondoka kwenda Juventus kwa uhamisho huru, uwezekano wa Arsenal kumuachia Xhaka ni mdogo zaidi hasa ikizingatiwa kwamba alikuwa nguzo muhimu zaidi kwenye nafasi ya kiungo ya timu hiyo.





# DE LIGT

## AKATAA KUJIUNGA NA BARCA

**AMSTERDAM, Uholanzi**

NYOTA wa Ajax, Matthijs de Ligt amekataa kujiunga na Barcelona, licha ya klabu hizo kufikia makubaliano ya ada yake ya uhamisho ya euro milioni 75.

Akiwa ndiye mchezaji anayewindwa zaidi kwa sasa barani Ulaya, De Ligt alikuwa kivutio kwa klabu kadhaa na licha ya Paris Saint-Germain kuonyesha nia kubwa ya kutaka kumsajili, wengi waliamini kwamba atatua pale Camp Nou. Hata hivyo, kwa mujibu wa televisheni ya Cadenar Ser, De Ligt amekataa kwenda Barcelona baada ya kushauriwa na wakala wake, Mino Raiola.

Kuna imani kwamba, De Ligt yupo tayari kufanya lolote analoshauriwa na Raiola na hajawahi kusita kufuata ushauri wa wakala wake huyo na ameamua sasa kuitosa Barcelona.

Bado sababu za Raiola kumshawishi nyota huyo kutojiunga na Barcelona hazijulikani.

Hata hivyo, De Ligt aliomba kiasi kikubwa zaidi cha fedha kuliko mchezaji mwenzake wa Ajax, Frenkie de Jong, ambaye tayari amejiunga na miamba hao wa Catalunya.

Sasa De Ligt ametajwa kwamba atachagua klabu moja ya kujiunga nayo kati ya PSG, Juventus na Bayern Munich, ambazo nazo zimetoa ofa kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19.

Na sasa inaonyesha wazi kwamba, PSG wana nafasi kubwa zaidi ya kumsajili De Ligt.

# Martinez: Lukaku sasa ondoka Man United

**MANCHESTER, England**

MSHAMBULIAJI wa Manchester United, Romelu Lukaku anapaswa kuondoka kwenye klabu hiyo, kwa mujibu wa kocha wa timu ya Taifa ya Ubelgiji, Roberto Martinez.

Lukaku mwenye umri wa miaka 26, alijiunga na United akitokea Everton kwa kitita cha pauni milioni 75 Julai mwaka 2017 na ameifungia mabao 42 katika michezo 96.

Mchezaji huyo alihusishwa na mipango ya kuondoka pale Old Trafford msimu huu wa joto baada ya kuwa na wakati mgumu chini ya kocha, Ole Gunnar Solskjaer.

"Ni muhimu sasa kwa Rumelu kutafuta klabu inayofaa," alisema Martinez akiliambia Gazeti la Ubelgiji, Het Laatste Nieuws.

"Itakuwa vizuri kwa pande zote mbili."

Martinez, ambaye alimfundisha Lukaku akiwa Everton na sasa katika timu ya taifa, aliongeza: "Ni wazi kuwa anapaswa kuondoka Manchester United."

Lukaku ambaye alikuwa akihusishwa na taarifa za kuhamia Inter Milan, mkataba wake na United utakapomalizika mwaka 2022.

Alipoulizwa kuhusu mipango yake ya baadaye baada ya ushindi wa 3-0 wa Ubelgiji dhidi ya Scotland na kufuzu michuano ya Euro ya 2020 juma lililopita, alisema: "Nitajua nitakachofanya, lakini sitasema. Tutaona."

Lukaku alifunga mabao 15 katika michezo 45 msimu uliopita, lakini Solskjaer amekuwa akipendelea zaidi kumtumia mshambuliaji, Marcus Rashford.

HABARI MICHEZO



# MOURINHO
## AFIKIRIA KUINOA TIMU YA TAIFA

**LONDON, England**

JOSE Mourinho amebainisha kwamba, anajiona atarudi kwenye kufundisha soka, lakini katika kazi ya kimataifa.

Mourinho bado hajachukua jukumu lolote la kuinoa timu tangu alipofukuzwa na Manchester United, Desemba mwaka jana.

Raia huyo wa Ureno amekuwa akihusishwa na klabu kadhaa, lakini Mourinho amesema anaweza kuchukua jukumu la kuifundisha timu ya taifa kwa mara ya kwanza.

"Nataka kushindana kwenye mashindano mapya. Nafikiri kuhusu Kombe la Dunia na Kombe la Ulaya," amesema wakati akizungumza na Kituo cha Televisheni cha Eleven Sports.

"Kwa muda mrefu nimekuwa na hamu ya kujaribu changamoto mpya. Kwa sasa najiona kwenye timu ya taifa kuliko kwenda kwenye klabu mpya.

"Timu ya Taifa ya Ureno kwa upande wangu? Sio muhimu zaidi kwangu."

Mourinho alikuwa kocha pale Old Trafford kwa kipindi cha miaka miwili na nusu, akishinda Kombe la Ligi ya Europa, EFL na Ngao ya Jamii.

Pia ameshinda mataji mawili ya Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na Klabu za Porto ya Ureno na Inter Milan ya Italia.

## MARTA AFUNIKA WANAUME MABAO KOMBE LA DUNIA

**PARIS, Ufaransa**

MCHEZAJI bora mara sita wa dunia kwa upande wa wanawake, Marta alifunga bao la 17 kwenye Kombe la Dunia na kuiwezesha Brazil kutinga hatua ya 16-bora baada ya kuifunga Italia bao 1-0, ambayo inaongoza Kundi C kwa tofauti ya mabao.

Michuano ya Kombe la Dunia kwa wanawake inaendelea nchini Ufaransa kwa sasa ikiwa imefikia hatua ya mtoano wa timu 16.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33, alifunga bao hilo kwa mkwaju wa penalti na kuwa mfungaji bora wa wakati wote wa Kombe la Dunia kwa upande wa wanawake na wanaume, akiipiku rekodi ya mshambuliaji wa Ujerumani, Miroslav Klose ya mabao 16.

Italia ambayo ilikwishafuzu, ilikaribia kufunga mara mbili kupitia kwa mshambuliaji wa Juventus, Barbara Bonansea, lakini mashuti yake yaliokolewa na golikipa wa Brazil.

Miamba hao wa Amerika Kusini sasa watawakabili Ufaransa kwenye hatua inayofuata mjini Le Havre Jumamosi katika michuano hiyo inayozidi kushika kasi nchini Ufaransa.

Italia ambao ndio vinara wa kundi watacheza hatua ya mtoano ya 16-bora dhidi ya timu iliyopo nafasi ya tatu na kuna uwezekano ikawavaa Nigeria au China.



# Neymar: Nataka kurudi nyumbani Barcelona

**PARIS, Ufaransa**

NEYMAR ameiambia Paris Saint-Germain anataka 'kurudi nyumbani' huku akibainisha kwamba hakupaswa kuondoka Barcelona.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil aliondoka Barcelona kwenda katika klabu hiyo ya jijini Paris mwaka 2017 kwa ada iliyoweka rekodi ya pauni milioni 198.

Lakini majaliwa ya mchezaji huyo na miamba hao wa Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, yamebakia na sitofahamu, huku taarifa zikisema kwamba anataka kurudi katika klabu yake ya zamani ya Barcelona.

Kocha wa PSG, Thomas Tuchel, ameripotiwa na Gazeti la Mundo Deportivo akisema kwamba kutokana na matatizo aliyosababisha Neymar kwenye vyumba vya kubadilishia nguo anaona kuna nafasi kubwa ya nyota huyo kuondoka.



Na sasa Neymar ameripotiwa kuwa amemuwambia Rais wa PSG, Nasser Al-Khelaifi kwamba: "Sitaki kuendelea kucheza zaidi PSG. Nataka kurudi kwenye nyumba yangu, sehemu ambayo sikutakiwa kuondoka."

Habari zaidi zinasema kwamba, kurudi kwa Neymar pale Nou Camp kipindi hiki cha majira ya joto kumechangiwa zaidi na Lionel Messi ambaye anamtaka mchezaji huyo, kwa mujibu wa Gazeti la El Mundo.

Taarifa zaidi zinaeleza kwamba, miamba hao wa Catalunya watakuwa tayari kumuacha mshambuliaji wa Atletico Madrid, Antoine Griezmann aende PSG, huku wao wakimchukua Neymar.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# TOFAUTI YA ARGENTINA YA MESSI NA YA MARADONA

●●●Watu wanazungumza kuhusu wote, lakini alikuwa na wachezaji wazuri mbele yake na...

**Belo Horizonte, Brazil**

Lionel Messi hapaswi kulinganishwa na Diego Maradona kwa kutofanya vizuri kwa sababu wachezaji wenzake wa Argentina hawapo kikazi zaidi ukilinganisha na waliocheza kikosi kimoja na nguli huyo.

Maoni hayo ni kwa mujibu wa kocha wa zamani wa AC Milan, Real Madrid na England, Fabio Capello kufuatia matarajio ya Messi kufanya vizuri kwenye michuano ya Copa America kuwa shakani.

Argentina jana ilitarajiwa kuivaa Paraguay huko Belo Horizonte nchini Brazil, ikitoka kupokea kipigo cha mabao 2-0 dhidi ya Colombia katika mechi yao ya kwanza ya Kundi B.

Nguli wa Barcelona, Messi hajawahi kushinda kombe kubwa akiwa na timu yake ya taifa - uvumilivu ambao unaonekana anajiandaa kuuona ukiendelea katika kiwango chake cha sasa.

Sababu hiyo inamfanya kuonekana havutii machoni mwa mashabiki wengi wakati anapolinganishwa na Maradona, ambaye kwa nguvu zake aliiongoza 'La Albiceleste' kutwaa Kombe la Dunia mwaka 1986.

"Watu wanazungumza kuhusu wote, lakini Argentina ya Maradona ilikuwa imara na ilikuwa na ubora kuliko ya Messi," Capello aliiambia Redio Marca.

"Alikuwa na wachezaji wazuri mbele yake, lakini katika kiungo na nyuma amekosa ulinzi. Hilo ndilo tatizo muhimu.

"Messi ni wa kipekee, anaishi akiwaza kuhusu kucheza na si kuhusu biashara, kama kwa mfano anavyofanya Neymar."

Raia mwenzake wa Messi na kocha wa Atletico Madrid, Diego Simeone anakubali kwamba matatizo ya nchi yake ni ya pamoja.

"Messi anaweza kutafuta suluhisho katika mechi, lakini anahitaji ushirikiano wa timu," Simeone aliiambia Fox Sports.

"Wachezaji ambao wanacheza na Messi wanapaswa kuelewa umuhimu walionao, ambao ni mkubwa na ni suala binafsi kwa kila mchezaji.

"[Messi] anahitaji kila mmoja wa wale wanaofanya timu kujisikia salama na kujiamini wakati wanapokuwa karibu naye.

"Sina hofu kuhusu daraja la Messi na ubora, na atakabiliana na hali yoyote kwa sababu anahitaji kushinda. "

## KWA UFUPI

**NEYMAR SOKONI RASMI PSG**
Paris St-German ipo tayari kumuuza mshambuliaji wao, Mbrazil Neymar, 27, majira haya ya joto. ***(ESPN)***

**WEST HAM YAGOMA MARTIAL KWA DIOP**
Manchester United itapaswa kulipa pauni milioni 75 kama itahitaji kumsajili beki Issa Diop, 22, kutoka West Ham, wakati huu 'The Hammers' wakiwa tayari wamekataa pendekezo la kujumuishwa kwa mshambuliaji Mfaransa mwenzake, Anthony Martial, 23, kama sehemu ya dili hilo. ***(Mirror)***

**ERIKSEN BADO LULU MADRID**
Real Madrid inaandaa ofa kwa kiungo wa Tottenham na Denmark, Christian Eriksen, 27. Miamba hiyo ya Hispania itakuwa tayari kutoa pauni milioni 45 pamoja na kiungo Mhispania Dani Ceballos, 22. ***(Sun)***

**ICARDI AWEKA USIKU KWA LUKAKU INTER**
MAJALIWA ya mshambuliaji wa Manchester United, Romelu Lukaku, 26, kujiunga na Inter Milan yanaweza kutegemea endapo dili la Mbelgiji huyo litamjumuisha nyota wa kimataifa wa Argentina, Mauro Icardi, 26, kukubali kwenda upande wa pili. Na kama sivyo, Inter itahitaji kumuuza kwanza Icardi kabla ya kusajili mshambuliaji mwingine. ***(Telegraph)***

**ARSENAL YAIACHIA SPURS ANDERSEN**
Spurs imepewa ofa ya kumsajili beki wa Sampdoria, Joachim Andersen, 23, kwa pauni milioni 31.2 baada ya Arsenal kuachana na mpango wa kuisaka saini ya Mdenmark huyo. ***(Star)***

**GERRARD AKATAA KUMRITHI LAMPARD**
KOCHA wa Rangers, Steven Gerrard ameukataa mpango wa kwenda kuinoa Derby County wakati huu miamba hiyo ya Championship ikitafuta mbadala wa Frank Lampard anayetarajiwa kwenda kuinoa Chelsea. ***(Times)***

**CASEMIRO AGEUZWA CHAMBO REAL**
Real Madrid inaweza kumjumuisha kiungo Mbrazil Casemiro, 27, katika ofa yoyote ya kumsajili Neymar kutoka PSG. ***(Marca)***

**POGBA KULAMBA BONASI UNITED**
KIUNGO wa Manchester United, Paul Pogba, 26, atapokea pauni milioni 3.78 kama bonasi ya uaminifu kutoka kwa klabu hiyo Julai Mosi, mwaka huu, licha ya kiungo huyo Mfaransa kusema "itakuwa ni vizuri kwenda kwingineko kutafuta changamoto mpya". ***(Mail)***

**MIGNOLET KUMPISHA MCCARTHY LIVER**
KIPA wa Southampton, Muingereza Alex McCarthy, 29, amefungua milango ya kujiunga na Liverpool, wakati huu 'Wekundu' hao wakijiandaa kumruhusu Mbelgiji Simon Mignolet, 31, kuondoka ili kumhakikishia nafasi katika kikosi cha kwanza. ***(Standard)***

**UNITED KUANZA NA WAN-BISSAKA**
KIPAUMBELE cha kwanza cha Manchester United ni kumsajili kwanza beki wa Crystal Palace na England U-21, Aaron Wan-Bissaka, 21, kabla ya kuhamishia mipango yake ya usajili kwingineko. ***(Manchester Evening News)***

**EVERTON, BARCA KUMALIZANA KWA GOMES**
Everton inakaribia kukamilisha dili la usajili wa kiungo Mreno Andre Gomes, 25, kutoka Barcelona kwa pauni milioni 22. ***(Mail)***

**GORETZKA AMSUBIRIA SANE BAYERN**
KIUNGO wa Bayern Munich, Leon Goretzka amesema atakuwa ni mwenye "furaha sana" kama klabu hiyo itamsajili winga wa Manchester City, Leroy Sane, 23, majira haya ya joto, lakini hatatia msukumo kwa mchezaji mwenza huyo wa Ujerumani kukamilisha uhamisho huo. ***(Manchester Evening News)***

**SPURS YATAJIWA DAU LA ZAINIOLO**
Roma inahitaji pauni milioni 62.4 kwa kiungo Mtaliano Nicolo Zainiolo, 19, ambaye amekuwa akihusishwa na kujiunga Tottenham. ***(Calciomercato, via Teamtalk)***

HABARI MICHEZO

# KMC FC, TP MAZEMBE KUKIPIGA MICHUANO KOMBE LA KAGAME

**Na Somoe Ng'itu**

BARAZA la Soka Afrika Mashariki na Kati (Cecafa), limesema jumla ya timu 13 zimethibitisha kushiriki mashindano ya Kombe la Kagame yanayotarajiwa kuanzia Julai 6 hadi 21, mwaka huu jijini Kigali, Rwanda zikiwamo KMC FC ya Dar es Salaam na TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Kushiriki kwa KMC kuna maana katika mashindano hayo ya mwaka huu, Tanzania Bara itawakilishwa na timu mbili, wengine wakiwa ni mabingwa watetezi wa michuano hiyo, Azam FC.

Hii ni baada ya mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba na watani zao, Yanga kutangaza kujitoa kushiriki mashindano hayo kwa sababu mbalimbali, mojawapo ikiwa ni kutokuwa na wachezaji wao wa vikosi vya kwanza, ambao wako katika fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) 2019 nchini Misri.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa Cecafa, Nicholas Musonye, alisema maandalizi ya mashindano hayo yako katika hatua za mwisho na yatatumika kama sehemu ya sherehe za miaka 25 tangu kurejea kwa amani katika nchi hiyo mwenyeji.

Musonye alizitaja timu nyingine ambazo zimethibitisha kushiriki mashindano hayo ni pamoja na wenyeji, Rayon Sports na APR, Gor Mahia, Bandari FC kutoka Kenya, KCCA, Proline za Uganda.

Alizitaja klabu nyingine zitakazowania kombe hilo ni Maafande wa KMKM ya Zanzibar, AS Ports (Djibouti), Heegan (Somalia) na Green Buffaloes ya Zambia.

"Bado tunasubiri barua ya uthibitisho kutoka kwa DC Motema Pembe ya DRC na Big Bullets ya Malawi, tunaamini yatakuwa ni mashindano makubwa na yenye ushindani, yatawasaidia sana wote watakaoshiriki kujiandaa na msimu mpya wa michuano ya kimataifa na ligi za ndani," alisema Musonye.

Aliongeza kuwa ratiba kwa ajili ya mashindano hayo itatoka kesho, na akaipongeza Chama cha Soka cha Rwanda (Ferwafa) kwa maandalizi waliyofanya na kuonyesha wanataka wageni watakaowasili wafanye kazi moja ya kuwania kikombe tu.

Bingwa wa mashindano hayo ataondoka na zawadi ya Dola za Marekani 30,000 (Sh. milioni 68.7) wakati mshindi wa pili atajinyakulia Dola za Marekani 20,000 (Sh. milioni 45.8) na timu itakayomaliza kwenye nafasi ya tatu itapewa Dola za Marekani 10,000 (Sh. milioni 22.9 za Tanzania).

MSHINDI...



Mkuu wa Idara ya Huduma za Kadi wa Benki ya Barclays Tanzania, Deogratias Moshy, akikabidhi zawadi za seti ya television, sofa na seti ya muziki kwa mkazi wa Mkoa wa Pwani, Majjid Omari (kushoto), mmoja wa washindi wa kampeni ya Ligi Kuu ya Uingereza ya benki hiyo. Mshindi katika droo kubwa atabahatika kupata safari ya Uingereza kushuhudia moja ya mechi ya Ligi Kuu ya nchi hiyo. Hafla hiyo ilifanyika jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Ofisa Masoko na Uhusiano wa benki hiyo, Esther Ndazi. MPIGAPICHA WETU

# Judo wapania All-Africa Games

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU ya mchezo wa Judo inaendelea kujifua katika viwanja vya Ukonga jijini Dar es Salaam kwa ajili ya kujiandaa na mashindano ya All-Africa Games yatakayofanyika kuanzia Agosti 19 hadi 31, mwaka huu nchini Morocco.

Akizungumza na Nipashe jana baada ya kumaliza mazoezi asubuhi katika viwanja hivyo, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Omar Mgowe alisema mashindano hayo yatashirikisha nchi zote za Afrika ambapo Tanzania itashirikiana na Zanzibar kuunda timu moja.

Kocha huyo alisema kwa upande wa Tanzania, itawakilishwa na wachezaji sita kati yao watatu wakitoka Zanzibar na wengine Tanzania Bara, ambao wataambatana na kiongozi mmoja.

Aliwataja wachezaji hao kuwa ni Musa Sheky, Jofrey Pawa na Anangise Pwele kutokana Tanzania Bara wakati kwa upande wa visiwani Zanzibar wakiwa ni Abdulrab Alawi, Mansab Alawi na Hamis Ally.

Aliongeza kuwa wachezaji wote wanafanya vizuri kwenye mazoezi pamoja na kuonyesha nidhamu ya hali ya juu.

"Vijana wanaendelea vizuri na mazoezi kwa ajili ya mashindano ya All-Africa Games ninajitahidi kuwapa mbinu ambazo zitawafanya waitangaze vizuri nchi yetu,"alisema Omar.

# Bushir aitaka ZFF kugeukia kufua vijana

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KOCHA wa timu ya Mbao FC, Ali Bushir, amesema bila ya kuwa na utaratibu mzuri wa kuziandaa timu za vijana itakuwa changamoto kubwa katika kuendeleza soka na hata kushindwa kufikia malengo ya kutoa wachezaji wazuri wenye viwango.

Bushir alitoa kauli hiyo wakati akifanya mahojiano na waandishi wa habari visiwani Zanzibar na kufafanua kuwa duniani kote katika suala la kukuza soka, tegemeo kubwa ni kwenye timu za vijana ndiko kunapatikana wachezaji wazuri ambao watazitumikia vema timu zao za taifa.

Alisema kuna kila sababu sasa kwa Shirikisho la Soka Zanzibar kuwekeza zaidi katika soka la vijana kuanzia umri wa miaka sita kama ilivyokuwa miaka ya nyuma ili kuweza kutoa vijana wenye uwezo na viwango.

**"Zanzibar kuna vipaji vya mpira tena vizuri na vijana wanacheza kwa ufundi kabisa licha ya kwamba bado baadhi ya vijana wao wenyewe kuona kama mpira ni kazi ambayo inaweza kuwaingizia kipato, lakini nafikiri kama kutakuwa na mfumo mzuri wa kuwekeza katika soka la vijana, basi watajitambua," alisema**

Aidha, alisema changamoto iliyopo kwa Zanzibar katika kukuza soka la vijana ni kutokuwapo kwa mfumo wa kukuza soka la vijana kuanzia miaka sita, nane, miaka 10 na kuendelea. Mfumo ambao unaruka miaka miwili miwili utakaosaidia katika kuendeleza vipaji hususan kwa vijana.

Aidha, ameushauri uongozi mpya wa ZFF uliopo madarakani kuhakikisha unaelekeza nguvu zao katika soka la vijana kwa kuanzia umri wa chini kabisa ili kuendelea kuwa na vijana hodari katika soka la Zanzibar.

# Ndayiragije chanzo kutemwa Chirwa Azam FC

**Na Mwandishi Wetu**

UONGOZI wa Azam FC umesema uamuzi wa kumtema mshambuliaji wao Mzambia Obbrey Chirwa, umetokana na mapendekezo ya Kocha Mkuu wa timu hiyo, Etienne Ndayiragije.

Chirwa na nyota wengine saba wa timu hiyo ya Chamazi jijini Dar es Salaam walitangazwa kuachwa na hivyo wako huru kujiunga na klabu nyingine za ndani au nje ya Tanzania.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Azam FC, Abdulkadir Popat, alisema jana kuwa ili timu yao iweze kufanya vema katika msimu ujao, itafuata mapendekezo na ushauri wa mkuu huyo wa benchi la ufundi na si vinginevyo.

"Tumemuacha Chirwa na wengine wameachwa kwa sababu hawako kwenye mipango ya kocha, na wala si kwamba tumeshindwa kufikia muafaka katika maslahi yake, haiwezekani," alisema Popat.

Aliongeza kwamba Azam FC imekuwa ikiheshimu maamuzi ya makocha wao ambao huwawajibisha mara wanaposhindwa kufikia malengo ya timu.

Wachezaji wengine ambao wamepewa mikono ya kwaheri na mabingwa hao wa Kombe la FA ni pamoja na Ramadhan Singano "Messi" ambaye aliomba kuachwa, Joseph Kimwaga, Hassan Mwasapili, Enock Atta Agey, Tafazdwa Kutinyu aliyetua Horoya FC ya Guinea, Steven Kingu na Danny Lyanga.

Kikosi cha Azam FC sasa kinaanza maandalizi ya kwenda kutetea ubingwa wa Kombe la Kagame katika mashindano yatakayofanyika kuanzia Julai 6 hadi 21, mwaka huu jijini Kigali, Rwanda.

# Michezo

Alhamisi Juni 20, 2019

Nipashe




Tofauti ya Argentina ya Messi na ya Maradona HABARI UK 30

HUKATIZI...



Kiungo wa Venezuela, Junior Moreno (kushoto), akihaha kumdhibiti mshambuliaji wa Brazil, Philippe Coutinho kwenye mechi ya Copa America iliyopigwa juzi na kumalizika kwa sare tasa. **PICHA: MTANDAO**

# PIGO STARS, MORIS BASI TENA AFCON

●●● Kufanyiwa upasuaji wa goti, Mwantika aitwa kumrithi, morali kikosi cha Amunike bado iko juu huku akisema...

**Na Somoe Ng'itu**

Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), imepata pigo baada ya beki wake wa kati tegemeo, Aggrey Moris, kubainika hataweza tena kukitumikia kikosi hicho katika fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon) 2019 zitakazoanza kufurukuta nchini Misri kesho, kutokana na kutakiwa kufanyiwa upasuaji.

Moris aliumia goti katika mechi ya kirafiki dhidi ya Misri iliyochezwa Juni 13, mwaka huu, mjini Alexandria na kumalizika kwa Stars kulala kwa bao 1-0.

Akizungumza na Nipashe kutoka jijini Cairo jana, Meneja wa Stars, Danny Msangi, alisema kuwa baada ya vipimo, imebainika kuwa beki huyo mkongwe wa Azam FC sasa atafanyiwa upasuaji na hawezi tena kuitumikia nchi yake katika fainali hizo.

Msangi alisema kuwa tayari Kocha Mkuu wa Stars, Mnigeria Emmanuel Amunike ameshamwita, David Mwantika kuziba nafasi ya nyota huyo.

**"Baada ya vipimo imebainika atafanyiwa upasuaji, kwa maana hiyo, hataweza kuwa sehemu ya kikosi hiki, tunasikitika kumkosa askari huyu," Msangi alisema.**

Meneja huyo aliongeza kuwa maandalizi mengine yanaendelea vema na kila mchezaji anasubiri muda wa mashindano ufike ili waweze kuipeperusha vema bendera ya Tanzania.

Mwantika anayeichezea Azam FC alikuwa miongoni mwa wachezaji tisa walioachwa kutoka kwenye kikosi kilichokwea pipa mpaka kambini nchini Misri kabla ya kuitwa tena jana.

Wachezaji ambao walitemwa katika mchujo wa mwisho nchini Misri pamoja na Mwantika ni Claryo Boniphace (U-20), Selemani Salula (Malindi FC), Abdi Banda (Baroka FC), Fred Tangalu (Lipuli FC), Miraji Athuman (Lipuli FC), Shiza Kichuya (ENPPI, Misri), Shaban Chilunda (Tenerife) na Kelvin John (U-17).

Taifa Stars ambayo imepangwa Kundi C ikiwa pamoja na Algeria, Senegal na majirani zao, Harambee Stars ya Kenya itaanza kutupa karata yake ya kwanza katika fainali hizo Jumapili dhidi ya Senegal.

Baada ya mchezo huo, itashuka tena dimbani Juni 27 kuvaana na majirani zao Kenya kabla ya Julai Mosi, mwaka huu kuhitimisha hatua ya makundi kwa kuvaana na Algeria.

Hii ni mara ya kwanza katika kipindi cha miaka 39 kwa Tanzania kushiriki fainali hizo za juu kabisa barani Afrika.

## Neymar: Nataka kurudi Barcelona




**PARIS, Ufaransa**

NEYMAR ameiambia Paris Saint-Germain anataka 'kurudi nyumbani', huku akibainisha kwamba hakupaswa kuondoka Barcelona.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil aliondoka Barcelona kwenda katika klabu hiyo ya jijini Paris mwaka 2017 kwa ada iliyoweka rekodi ya pauni milioni 198.

**UK. 29**

## Mourinho ageukia kuinoa timu ya taifa



**LONDON, England**

JOSE Mourinho amebainisha kwamba, anajiona atarudi kwenye kufundisha soka, lakini katika kazi ya kimataifa.

Mourinho bado hajachukua jukumu lolote la kuinoa timu tangu alipofukuzwa na Manchester United, Desemba mwaka jana.

**UK. 29**

## Atletico Madrid yamgeukia Xhaka

**LONDON, England**

KLABU ya Arsenal imejikuta kwenye wakati mgumu baada ya kuletewa ofa na Atletico Madrid wakimtaka, Granit Xhaka.

Atletico wanataka kumsajili kiungo huyo kwa ajili ya kuziba nafasi ya Rodri, ambaye anakaribia kutua pale Manchester City.

Kwa mujibu wa Gazeti la The Mirror,

**UK. 28**

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >